

**CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION**

**(CKRC)**

**VERBATIM REPORT OF**

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, KANGUNDO  
CONSTITUENCY AT TALA PRIMARY SCHOOL**

**ON**

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, KANGUNDO CONSTITUENCY, PUBLIC HEARINGS HELD AT  
TALA PRIMARY SCHOOL ON 17<sup>TH</sup> MAY 2002**

**Present**

1. Com. Mutakha Kangu
2. Com. Pastor Zablou Ayonga
3. Com. Dr. Charles Maranga
4. Com. Phoebe Asiyo

**Secretariat in attendance**

1. Peter Kanyi - Programme officer
2. Lydia Manyoni - Assistant Programme Officer
3. Jacqueline Nyumoo - Verbatim Recorder
4. Rose Ngina Kimeu - District Coordinator

**The meeting was called to start at 9.45 am with Com. Asiyo in the Chair.**

**Rose Ngina :** Leo tunafuraha kuwakaribisha katika siku ya leo, tuko na siku ya kutoa maoni, na ningependa tuanze kwa maombi. Na kama kuna mmoja wetu atuanzie mkutano wetu kwa maombi.

**Mr. Musyoka:** Asanteni sana. Fungeni macho tuanze na maombi ya Bwana.

Bwana na baba wetu uliye juu mbinguni tunakuomba kwa vile kila mtu umemkinga mpaka akaja kufika hapa bila ajali yoyote, na mambo yote yalioleta hapa sisi, tunaomba uyaweke katika mikono yako na yawe ya amani. Mungu wale waliokuja hapa nao pia tunawapa, tunawaomba wapewe mawazo mazuri katika mambo tunayofanya ya Katiba. Mungu utusaidie sana na wakimaliza mambo yote wasisahau kukurudishia amani. Twaomba hayo yote kupitia kwa jina la Yesu Kristo.

**Rose Ngina :** Kwa hivyo bila kupoteza wakati mwingine ningependa ku-introduce members of the three Cs wale members wa Constituency Constitutional Committee wenye wako. Tafadhali mukaweze kusimama, na kuanzia pale tuko na Chairman wa Constituency Committee Mr. Munyoli, karibu na yeye tuko na councilor Nicholas Chengo. Upande huu tuko na Lydia Nduko Henry, kuna Peter Musyoki na Kamene Muli. Hao ndio members wa Constituency Committee wenye wamefika wakati huu. Na mbele yetu kuna makomishona kutoka kwa Tume ya kurekebisha Katiba ya Kenya wenyewe watajitambulisha kwetu. Asanteni.

**Com Asiyu:** Asante sana coordinator kwa kutukaribisha kwa kikao hiki cha kupata mawaidha kutoka kwa watu wa Tala juu ya kurekebisha Katiba ya Kenya. Wale ambao wako hapa mbele, upande wangu wa kushoto ni Dr. Charles Maranga ambaye ni commissioner. Upande huu wangu karibu na mimi mzee mwezangu ni pastor Zablon Ayonga. Pale mwisho kuna Mutakha Kangu ambaye pai ni lecturer wa University ya Moi na pia ni advocate of the High Court na tena ile cheo kubwa yeye ako nayo kwa kikao hiki yeye ameo msichana wa hapa.

Kabla hatujaanza ningependa tupatiwe makaribisho na chairman wetu wa 3 C na chairman wetu wa County halafu ndio tuanze. Kwa maneno machache tu ili tujue mambo yako hapa namna gani, kazi inaendelea namna gani, halafu tuanze kusikiza maoni ya watu wa hapa.

**Munyoli:** Asante sana chairperson wetu wa mkutano wa leo na commissioners wale wamekuja. Yangu ni kusema ni shukrani sana mmepata nafasi kuja upande wa Kangundo na tulikuwa tunaongoja nyinyi na hamu sana, kwa sababu watu wa Kangundo kwa jumla wana maoni mengi, wanataka ku-contribute na watakuja. Najua wengi wako njiani wanakuja, na wakati tulikuwa tunatembelea hao huko na kule, wengi wameandika hata memorandum. Wengi wamesema leo watakuja watoe maneno yao kwa kusema na tumeshukuru kwa sababu wachache wamekuja na ninaona hii nyumba itafika saa nyingine itakuwa imejaa. Kwa hivyo mjisikie mko Kangundo, mambo yote ni mazuri na ingawa tulikuwa tunaendelea, iko shida kidogo kidogo hapa na pale. kwa sababu hii civic education ni extensive exercise vile nimejua sikuwa najua hivyo mbeleni, ni very expensive exercise. Kwa sababu saa nyingine unaingia pahali pengine, hawa watu wanahitaji transport, wanahitaji saa ingine hata lunch, saa nyingine wanahitaji hata wabebwe na gari kwa sababu Kangundo ni kubwa sana ni division mbili. Na kama ni division mbili ukifanya hesabu ni area kubwa sana, na tumejaribu tukisaidiana na hawa ma civic educators, wale facilitators. Wamejaribu nimeona report zao, nimekuwa na sign halafu waende Machakos ili walipwe.

Hata hiyo shida ya kwenda Machakos nilikuwa nachunguza nikaona ni very expensive. Mtu kutoka hapa na mia moja na kurudi na mia moja aende alipwe mia tatu that is nothing, anabaki na mia moja, it is very expensive. Kwa hivyo tulionelea hiyo ifikiriwe na ili watu wapeane, tuwafikie hili watupatie, mawaidha na ingawa muda tunaomba sana iongezwe ili tuwafikie kule vijijini. Kwa sababu tunaona wengi walikuwa bado kuelewa, kwanza waliona kama ni political meeting. Kwanza walielewa hivyo lakini sasa wameshajua ni kitu cha maana hawakuwa wameelewa what type of Commission Review is this one. Walikuwa wanafikiri labda ni kujenga mtu, nikufanya hivi na vile, lakini vile nimeona sasa wameshaelewa hii ni kuunda Katiba ambayo Kenya yote kila area ya Kenya mumezunguka na mumeona na sisi tunataka tuwe part and parcel kwa hiyo mipango, watu wa Kangundo. Kwa hivyo natoa shukrani na kamati yangu imefanya kazi usiku na mchana, tumezunguka kila wakati tunasikiza area zile bado kupata watu wa civic education, tunabakisha area kidogo. Kuna area moja inaitwa Kivani iko mbali sana huko chini, Southern Kangundo, kuna ingine inaitwa Kakuyuni, hatujawai kufika. Kuna area ingine iko Kinyui, upande huu hatujafika. Kuna nyingine inaitwa Cheleli. Ingawa civic educators wameenda lakini sisi watu wa district hatujawai kufika huko ili waone umuhimu wa huu mpango.

Kwa hivyo tunaomba muda ili tuweze kuwafikia sisi kama 3 Cs, tuongee na hao, tupate transport, tupate kuongea na wao mambo ya stationery, vitabu tupate zingine. Hivi vitabu vinasaidia sana kwa sababu watu tumeenda wanaangalia, tunaenda na hicho kitabu moja from page 1 to page 25 tunaenda moja kwa moja na ninaona kinasaidia sana.. tuongezwe vitabu zingine na stationery ili tuweze kufikia watu na tuwe na classrooms tuongee na hao mambo ya constitution. Kwa hivyo leo nashukuru watu, naona wanaendelea kuja, na wakati huu sasa nitauliza Chairman wa town council BwanaChengo na yeye aweze kuongea machache kwa sababu nimekuwa na yeye kila wakati na anajua shida zetu. Asanteni sana.

**Clr. Chengo:** Basi na mimi madam commissioner na wenzako na Wananchi wa Kangundo kwa jumla, jina langu naitwa Nicholas Mutii Chengo, ndio chairman Kangundo town council na pia ni mwanakamati katika Review commission Committee hapa Kangundo. Kwanza ningetaka kushukuru nyinyi sana kwa vile mumeingia hapa Kangundo ili kuchukua maoni yetu kuhusu mambo ya Katiba na muliingia mapema sana, hatukuwa tunatarajia nyinyi mapema namna hiyo, natulikuwa bado kujiandaa, tulikuwa tunafikiria mnakuja saa tano hivi, na inaonekana nyinyi ni watu washupavu ni watu ambao wanajua ku-keep time vizuri na hiyo ndio mwenendo mzuri, ni vizuri watu wawe wanakomaa kimasaa ama kikazi ndio tuweze kuendeleza nchi yetu.basi kama vile Bwana chairman amaesema amaongea karibu yote, civic providers wamefanya kazi yao, wamejiandaa, wametembea karibu kote katika constituency yetu lakini yenyewe ni kubwa na ninafikiria iko sehemu kama hizo Bwanachairman amaesema, hatujawai kuona kama imeangaliwa vizuri. Kwa sababu tunataka kila mtu awe anaelewa hii mambo ya Katiba ni nini, tunaomba haya masomo yasikome leo. Yaendelee mpaka watu waelimishwe kila corner, kila mahali ndio wawe wanajua ni kitu gani kinahusu mambo ya Katiba.

Kulikuwa na shida hapa na pale kwa sababu ya mambo ya transportation, mambo ya nini, na tungeomba, tulikuwa tumeomba tupewe mambo ya transportation ndio tuweze kufikia watu vizuri. Hiyo pengine haikupatikana hapa na pale, lakini hiyo sio hoja lakini tuangalieni mambo in future ndio tuweze kuendelea vizuri. Watu wa Kangundo, wengi wao wameandika memorandum zao, wale ambao pengine hawataweza kufika hapa wametumana, wameandika na ninatunaini leo ikiwa ni siku ya soko, pengine wameenda sokoni lakini watakuja hapa. Kwa hivyo I think we are quite comfortable with people watu watakuja.

Tumewai kuja na councilors wetu hapa, hiki ni kitu ambao councilors wetu wamehusika sana nayo na ningeeomba wale councilors ambao wamewai kufika wakati huu tafadhali msimame ndio commissioners waweze kuona nyinyi. Pale tuko na vice chairman wangu, anaitwa madam mary Mulu, kama madam vile nilivyokuambia sisi ni gender sensitive, tulionelea tukiwa na chairman mwanaume, tuwe na mdogo wake mwanamke ndio wanawake wawe wanafikiria wako sawa sawa. Pale tuko na councilor Kiilu, hapa tuko na councilor Mumu na wale wengine natarajia wako .... Sorry na pale tuko na councilor Catherine Munyao, huyu naye ndio chairman wetu wa education in social services, wale wengine wako kwa njia nafikiria wanakuja.

Mheshimiwa Ngutu ambaye ni waziri wa labour alikuwa awe na sisi hapa pia akaribishe nyinyi, lakini vile mnajua ako na kazi nyingi. Mambo ya kuhusu chifu, mambo ya nini, hata mambo ya kusemekana amefutwa Kangundo na nini, lakini hayo sio hoja,

alisema ataenda huko na akimaliza atakuwa na sisi. Kwa hivyo you have got his blessings. Na mkiwa hapa, mkiwa mumepewa blessings na Mheshimiwa Ngutu, na mimi kama mayor, mimi napatia nyinyi kifunguo, mkae hapa hata mlale hapa, mchanganye na watu wa Kangundo na hata tuende kwa shemeji huko tukale mbuzi halafu mambo inakuwa mzuri (clapping). Leo ni weekend, kwa hivyo hakuna haraka ya kurudi, sasa mtaenda kufanya nini. Basi madam Asiyu, si mnamjua mnasikia sasa mko na furaha mumemuona hapa mwenyewe live live, basi makofi kwa yeye. Basi madam karibu na utuendelezee mambo ya Katiba na tumefurahia sana. Thank you very much.

Kuna jambo, nataka kuomba msamaha kwa sababu tuli-change venue, tungekuwa Tala Primary School lakini tumeleta hapa Township kwa sababu iko huko michezo ya sports na tukaona kutakuwa na watoto wengi kwa hivyo we are sorry for that inconvenience, so tukaona hapa ni pa-fit tukapanga hapa.

**Com Asiyu:** Mlifanya vizuri, tuliona watoto wengi sana kule nilipokwenda huko kabla kufika hapa. Kwa vile tuko kwa shule hii ningependa kuuliza headmaster atukaribishe kwa shule yake halafu ndipo sasa tuanze kazi na tukianza kazi mpango itakuwa namna hii. Tumeulizwa na kina mama tukae na kikao chao na nimefurahia sana. Sasa tutakuwa vikao viwili, mimi na mzee Ayonga tutaenda kusikiliza maoni ya kina mama kwa mambo ya kubadilisha Katiba kado, na wazee watakaa hapa. Bwana headmaster, tafadhali uje utukaribishe kwako ili tuwe uhuru kama vile tumepewa ufunguo na Bwana mayor, na vile chairman wetu pia ametukaribisha na Mheshimiwa Ngutu pia. Sema majina yako yote tunanasa kwa hiyo machine (clapping).

**Jonathan Muli:** Kwa majina ninaitwa Jonathan Muli, mwalimu Mkuu wa shule hii ya Tala township, kwa wakati huu na kwangu ni shukurani nyingi sana kwa wageni na wahusika wote ambao waliketi na wakaonelea kwamba shule yetu itaweza kufaa, na itaweza kushiriki katika jambo hili la kuchukua maoni kutoka kwa Wananchi kuhusu jambo hili la Katiba. Tunafurahia na tunawauliza mtukubalie vile tulivyo katika hali yetu, na pengine tuko na sehemu mbali mbali za haja. Upande huu kwa watu wazima kuna nyumba ambazo mtaweza kutumia kwa wakati wa haja, lakini ukweli ni kwamba mko uhuru kukanyaga mahali popote katika shule hii ndipo tuweze kufikia kiwango kizuri. Kwa hivyo ma commissioners wale wote ambao mumefika na wageni wengine wote ambao wako hapa tafadhali mjisikieni mko kwenu, mko nyumbani na tunawakaribisha tena na tutakaa na nyinyi mpaka hata mkikaa kwa kikao hiki kwa siku mbili tatu hatuna neno. Karibuni sana.

**Com Asiyu:** Asante sana. Pia ningependa kuwajulisha kwamba Bwana Muli ambaye alikuwa Attorney General wetu hapo mbele ameingia, na yeye juzi alituletea document nyingi sana kule kwa headquarters ya commission juu ya haya mambo ya kubadilisha Katiba, najua naye pia atatupatia mawaidha ya maana sana maana alikuwa ndani ya hiyo mambo kwa miaka mingi sana. Kwa sasa nataka coordinator aniambie nitaenda wapi, kikao cha kina mama pamoja na pastor Ayonga, tuende tukae na ninaona kuna swali moja hapo nyuma. Je Mzee unasema nini?

**Speaker:** Kabla hatujaenda kwa kikao cha tofauti tofauti, ningeoonelea kama kuna mawazo mengine ama mazungumzo nyingine tunaweza kuwa sisi sote tunataka kuyasikia, ile inahusu kina mama na kina baba. Kwa hivyo kabla hawajaenda, kwa sababu

kuna vitu vingine inatuhusu sisi sote, ndio wakienda hawatajua, watakuwa wakituuliza, mumezungumza ile maneno? Sasa tunataka pengine ikiwa ni mtu mmoja kama tuseme mimi niko na kitu kinawahusu hawa kina mama na hawa kina baba wawe karibu wasikie at least ndio kiongozi mmoja wao ametaja vitu ingine ambao pengine wanaweza kukosa kutaja upia na wataanza kutuuliza. Hiyo nikusema kama ningepatiwa nafasi ya kwanza, ningezungumza, pengine wataangalia waone kama ni mzuri kwao, halafu kukiwa hakuna kingine pengine ndio mtaenda. Kwa sababu wakienda hawatasikia kile mumezungumza.

**Com Asiyu:** Ninashukuru kwa hayo mawaidha lakini unajua wote wanaongea leo ni sisi wanatuongelesha maana sisi ndio tutaandika hiyo Katiba. Hata wakipenda kuongea kwa camera mtu mmoja tutafanya vile wanataka. Sasa tumeulizwatuwe na kikao hicho kingine sio maoni yetu ni maoni ya watu wa hapa, kina mama wa hapa. Lakini kama wewe mwenyewe unaona una jambo fulani ambalo unataka kina mama wasikie nataka uje na sisi pia huko uongee. Na kama kuna mama pia anataka pia kuongea jambo lingine wazee wasikie, tena tufanye hivyo. Si hiyo itakuwa ni sawa sawa? Ndio. Yes Mzee.

**Speaker:** Mimi ile nataka kusema hiyo ya ku-divide haitakuwa mzuri kwa sababu iko makosa ambayo wanaume wanafanyiwa na wanawake, na ikiwa mtazungumza kule hiyo ugonjwa haitatoka kwa hivyo tuwe pamoja.

**Speaker:** Kwa mgeni muheshimiwa Asiyu, na commissioners wowote, sisi wanawake iko mambo ambayo hatuwezi taja mbele ya wanaume, tunawaogopa, tunataka kwende petu. Kwa sababu wanaume ndio kichwa na sisi ni shingo na ni lazima tuzungumze yale ambayo inatuhusu, Katiba irekebishe, Katiba ione makosa iko upande gani. Kwa hivyo sisi wanawake kando, wanaume kando.

**Com Asiyu:** Mnakumbuka kwa bibilia kuna wakati fulani wanawake wawili walisema mtoto huyu mmoja ni wao halafu shauri ikakatwa. Sasa nasema kwa maana kichwa ni kitu kikubwa sana ikae, na shingo iende. Asante sana. Sasa Bwana Muli pengine ungetuongelesha kidogo kabla shingo haijaenda kando.

**Muli:** Madam commissioner na commissioner wale wengine, ndugu zangu, kina mama na wengine wote nimefika nimechelewa kidogo kwa sababu ingine na nina furaha kuwaona tena hapa na haswa wewe maanake ndio ulifungua mkutano wa kwanza huko Kangundo na tuna furaha umerudi pamoja na ma commissioner wale wengine na facilitator. Nimekuta jambo linalosema la kugawanya. Ni sawa sawa, hiyo si kitu kigeni, tulianzwa na wazungu wakiita divide and rule. You can also continue to be divided and rule but I think this is a very important matter madam chair. My contribution to that, I know you have made a ruling which is perfectly correct is this, tufanye ile inaitwa.. nimekuta mwingine akisema na ninaona ni vizuri plenary, tusemo general na tukifika kwa hali ingine pengine, ili tugawanyike, ili tuende na mabo ya ndani ndani.

Tukiacha kusema kama wengine wanaogopa wengine hawawezi kusema hiyo tunaolewa, lakini plenary general ni important. Kila mtu ajue tunaenda wapi.

**Com Asiyu:** Okay, Mzee tumesikiliza maoni hiyo yako na tumeshukuru sana hayo mambo ya hekima, lakini demokirasia tunaifuata kila mahali na watu wakituuliza wangependa jambo fulani kwa kamati hii hatuwezi kukataa. Kuna walemavu walituambia wanataka kukaa kando na watu wasio walemavu na tulikubali tukakaa na wao. Kama kuna mama ambaye anataka kuongea hapa ni lazima apate nafasi ya kuongea hapa. Na kwa vile ulisikia wao wenyewe wakisema na wametuuliza, inatubidi sasa sisi kukubali na mawazo yao ya kukaa kado. But if there is any lady who really wants to talk here with everybody, there is no problem because the thing is this, sisi ndio tunaelezwa mambo ya kubadilisha Katiba. Watu wa hapa hawataandika, sisi ndio tutaandika maoni yenu, kwa hivyo ni vizuri sasa tukubaliane, kina mama wakae kando vile wametuuliza na umeona vile walipiga makono kwa wingi na vile ulipomaliza kuongea Mheshimiwa Attorney General wa zamani, ni wachache ndio wamepiga makofi. Sasa nafikiri tuende kwa mambo ya majority na mambo ya demokirasia ambayo watu wa Kenya wamezoea. Ni sawa? Haya.

Ninaona kuna wazee wawili bado wanataka kuongea, mzee hebu ongea halafu yule mzee.

**Jonathan Mulinge:** Mimi kwa jina ninaitwa Jonathan Mulinge. Ningesema kwa upande wa wanaume na wanawake. Kama mimi sasa nina jambo ambalo linahusu wanaume na wanawake, na wanawake wakienda mbali hawatasikia.

**Com Asiyu:** Sio wao wanaandika Katiba.

**Jonathan Mulinge:** Nyinyi ndio mnaandika lakini wanahitaji wasikie tunasema nini. Ikiwa imepitishwa kwa Katiba muandike hiyo ndio sawa sawa kwa sababu haiwezekanai waondoke hivi. Hiyo maneno yangu ya waume na wanawake nani atajibu? Nafikiri hiyo itakuwa vizuri mama, kwanza tuseme kitu very important kwa nyinyi.

**Com Asiyu:** Tusikilizane, tunaona kuna shida kidogo na pengine ingefaa sasa tuendeleo kusikiliza maoni ya the first 5 people ambao wanataka kuongea kwa mambo yanayohusu wanawake na haya mambo yatakuwa pengine juu ya kubadilishwa kwa family law na pengine mambo ya mashamba, si ndio hivyo? Na pengine mambo ya watoto maana ndio mambo hayo yanaumiza kina mama sana. So watu hao ambao wanataka kuongea haya, tuanze sasa. Mama na baba halafu tukimaliza kina mama vile wameuliza wanataka kukaa peke yao kikao chao, ni lazima tuwaheshimu na tuwapatie hiyo kikao. Asante.

Okay, we can now start with the first person who wants to talk about issues that concern both men, women and children, the disabled, the youth, mambo ya shamba na mambo ya uwakilishi wa kina mama kwa mambo ya Serikali ili tuanze. Tukifuata hii list, tuko na BwanaAnthony. Je BwanaAnthony uko hapa? Okay, kina mama wanataka kuongea muweke mkono juu wale ambao wanataka kuongea hapa mmoja, wale wengine wataongea kule. Na kina baba wanataka kuongea sasa, good. Tutaanza na huyu mzee halafu huyu mama, halafu yule mzee aliniongoza kwa njia nilipoingia hapa halafu basi tutaona tena. You can start, give us your full name and then we will start. Asante BwanaMaingi sasa unaweza kuanza kuongea na sisi halafu mama utafuata mzee. Na ni dakika tano tumekupatia mzee ili kila mtu apate nafasi hapa kama anataka kuongea. Najua watu wengi working with the police watakuja hapa vile hall yote imejaa.

**Jonathan Mainge:** Mimi jina ni Jonathan Mainge. Vile nilikuwa nikitaka kusema upande wa waume na wanawake ni juu ya watoto. Kwanza huwa kuna watoto wa kiume na wa kike na hao watoto wa kiume na wa kike wote wamezaliwa na mzazi mmoja, mama na baba lakini nilipo fikiria sana, nikaona kwa hakika kuna watoto wengi wanapata taabu kutoka kwa hao wazazi. Kwanza habari ya chokora inaingia kutoka kwa sisi wazazi na ndio tunafanya chokora wawe wengi zaidi. Kwa sababu ya kusema chokora ikiwa mama amezaa mtoto wa kiume na wa kike, mtoto wa kiume ana uruthi kwa baba yake lakini huyu wa kike ako out. Mimi vile ningesema habari ya huyu mtoto wa kike, mtoto wa kike yoyote, ule ashaolewa akaenda kwa Bwanana akapata watoto kule na akarudi kwa baba hapo iko write off. Aliwacha shamba yake au iliwachwa kule, haitaji kitu kwa baba. Na yule msichana ambaye hajapata mwanaume na akiwa hana mwanaume anazaa na ana watoto. Mimi baba ni mkatie sehemu akae pale maisha kwa sababu atasomesha watoto bila kuhangaika, wawe wanawake wanapewa shamba na mzazi. Kwa hivyo chokora hawataonekana, chokora anatoka huko nyumbani kwa sababu ya msichana kukosa mahali pa kukaa, watakalisha watu wapi.

Ile nyingine ninasema habari ya president, President ni mtu wa kuheshimiwa sana katika nchi na inatakiwa itolewe Katiba ya kwamba President akitoka katika kiti cha enzi alindwe bila mchezo. Si kama nchi zingine President akitoka ule anakalia anakuwa ndio afukuze yule alikuwepo mbele, hiyo si nzuri katika Kenya. ndio sababu ninalia kwa sababu nimeona nchi kadhaa. Somalia nimeona, Ethiopia nimeona, Uganda nimeona, Malawi nimeona, na hata zambia nimeona. President akitoka anatimuliwa na yule ambaye anaketi kwa kiti. Vile ingekuwa viziwi ni President mwenyewe akitoka awe mtu wa kupewa heshima katika nchi ile alisimamia. Kama mtukufu Moi, ana mwiaka thelathini na sita. Kumi na mbili Vice President na ishirini na nne akiwa President na ni heshima kwa sababu Kenya haijashikwa bunduki watu wapigane isipokuwa hao watu walishika bunduki mikora ya kuiba pesa na wao wanataka kuitwa chokora. Hapo mnasikia. Sasa President mwenyewe akishatoka apewe bodyguard ya kumchungu nyumbani kwake kwa sababu ni mali ya Serikali na amesimamia miaka mingi sana na asitaabishwe na mtu yoyote.

Ya tatu, ninasema habari ya minister. Minister wakati kuna financial year anapewa katika idara yake pesa kama milioni hamsini au sitini ya kutumika katika idara yake, na tulipo mchagua, tulimchagua akakae kwa Bunge miaka mitano. Na hiyo miaka mitano ile pesa alipewa yeye kazi yake ni kukaa ofisi, haangalii PS anafanya nini, assistant minister wake anafanya nini na officer mwenyewe yule anasimamia kule chini haangalii na zile pesa zinaliwa. Zikiliwa watu wakiuliza wanaambiwa Serikali hakuna pesa. Mimi nataka Katiba itolewe nzuti ki Kenya. tumechagua minister akakae kule miaka mitani, idara yake ikipoteza pesa afungwe jela miaka mitano.

Wakati commissioners wanakuja hapa sisi tunafurahi sana kwa sababu nyinyi ni macho ya Kenya na vitu vyote tunavyosema mna-record lakini kuna mahali pako kombo kidogo na ndipo ningetaka panyoroshwe. Maana yake kama sasa nimesema dakika tano hivi, kama hapa pangukuwa mtu wa TV, angenipiga picha wakati wa kutangaza maneno nionekane kule. Lakini mtu akisimama kama Attorney General anapigwa, anaonekana kule, kwani Katiba nani anatengeneza, ni yule au ni sisi. Kwa



hivyo tunataka tukisema tuwe tukionekana, wale wengine katika Kenya wajue tumesema nini. Kwa hivyo nafikiri dakika zangu zimekwisha, Asanteni sana na muendeleo hivyo hivyo.

**Com Asiyu:** Mimi nina swali moja tu, ulisema kwamba msichana akiolewa aende halafu apate shida kule, pengine Bwanayake ni mkorofi, ampige na amufukuze kabisa. Unataka afanyiwe namna gani, anaweza kurudi kwa baba yake kupata mahali kidogo ya kulima ama aende town na apotee huko?

**Jonathan Mainge:** Hiyo swali ni nzuri sana, nimefurahi nayo. Ikiwa kule anaolewa tunapeana nafasi ya arudi aje kwa baba yake na watoto na apewe shamba, hawatakaa kwa bwana. Akikosa kule akatafute shamba na hiyo ndio itakuwa vizuri, hakutakuwa na wanawake waliotoka kwa ma Bwana yao.

**Com Asiyu:** Lakini tunaona wanawake ambao hata mumeona juzi mwanamke alitolewa macho mawili yote na bwana, pia nasikia walikuwa wanagombana kwa mambo ya mali. Sasa huyu msichana kwa maana hawezi kuona baba yake anaenda kumchukua anasema mtoto yangu mimi ndio nilikuzaa, kuja nikulinde kwa maana umekuwa kipofu. Hapo tutafanya nini?

**Jonathan Mainge:** Sasa hiyo wakati kisa cha waanzane mpaka msichana atolewe macho, baba ako hapo na mama ako hapo, wao walikuwa wawili na huyu mama. Unajua kuna mama wana mdomo kama moto, alifanya Bwanayake akakasirika akamtoa macho ndio akae kwake kwa sababu anampenda.

**Com Asiyu:** Lakini huyu msichana ni wake alimzaa wewe pengine ulimpenda sana kwa maana alikuwa mtu mzuri nyumbani ukamuelimisha vizuri akaenda. Na huwezi kukata shauri katikati ya huyu Bwanana huyu mama ni nani mbaya maana mtoto ni wake na ametolewa macho kule, utamtupa?

**Jonathan Mainge:** Asante sana kwa vile unauliza. Mimi especially, wewe 1950s ulijuana na Bwana yako na wakati ulipotoka kwenu wazee waliketi chini wakakuambia mama uende, ukakaa nyumba hiyo, uliolewa kwa amani na hukuambiwa ukafukuze watu ukakosana na wale, uliambiwa ukakae na amani. Huyu mwenye kutobolewa macho yeye ndio alikuwa na mdomo kwa sababu alikuwa pale mbele, walikuwa wanaketi vizuri sana na iko kitu walikosania kwa hivyo hawezi kurudi bila macho ati arudi kule apewe shamaba, haiwezekani. Ana watoto pale, awache watoto na Serikali iingie katikati.

**Com.Pastor Ayonga:** Wa mama mpoe pengine sauti zimekuwa nyingi kwa maana mama moja alitobolewa macho. Nadhani ni lazima tuheshimu maoni ya mtu kama mtu hata kama amesema mbaya hayo ni maoni yake. Wewe wakati wako utakuja kusema maoni yako.

Mzee umesema idara ikipoteza pesa, minister afungwe miaka mitano. Hii si itakuwa ni ngumu sana isipokuwa minister awe alishiriki kwa kupoteza hizo pesa yeye mwenyewe as a person. Lakini ministry ikipoteza pesa, ni kwa nini minister afungwe na kuna wale ambao wataangalia mambo wapate who actually took the money.

**Jonathan Mainge:** Hiyo ni mzuri sana, asante sana kwa swali lako. Nafikiri pastor, wewe una watoto na wale watoto wote utajua kila mtu anasoma vipi, na wewe ndio unanunua nguo, ndio unatoa fees, ndio unatafuta chakula vile watakula. Kwa nini minister asiangalie kila branch ya laini yake, hii pesa inatumika namna gani? Kwa nini anataka kula?

**Com Pastor Ayonga:** Hebu nikuulize swali, wewe ni baba wa mtu? Unataka kusema kwamba mtoto wako akifanya makosa baba afungwe? Imetosha.

**Jonathan Mainge:** Mtoto akifanya makosa, umuwachilie Serikali.

**Com Pastor Ayonga:** Kwa nini ministry ikipoteza pesa minister afungwe?

**Jonathan Mainge:** Kwa sababu yeye ndio alipewa pesa kutoka kwa board, haikupewa yule mtu mdogo.

**Com Asiyu:** Tumeshukuru sana mzee kwa maoni yako ambayo umetupatia. Sasa tuko na mama ambaye tulikuwa tumemueleza atakuja nyuma yako. Tumeshukuru sana, tafadhali uandikishe jina lako kwa register yetu ndio tujue kabisa kwamba wewe ulipeana maoni hapa.

**Bernadette Muli:** Mimi ni mwenyekiti wa Maendeleo ya Wanawake wilayani Machakos. Ile point nitaongea, nitaongea juu ya watoto mayatima wale mama zao na baba wamekufa kwa sababu ya huu ugonjwa iko hatari wa ukimwi. Ninauliza kuwe na mpango, kwa kila division tuwe na orphanage au home ya kusaidia hawa watoto wapate elimu, wapate chakula, wapate nguo na wapate kila kitu. Kwa sababu wengi wao hata wale watu wa nyumbani wamewaachilia wakiwa peke yao na tukikosa kufanya hivyo watu wa Kenya, kesho hatutakuwa na commissioners kama hawa wako hapa mbele ama participants.

Ile mambo ingine ni juu ya mtoto msichana na kijana. Hawa watoto wote ni watoto, wapate elimu ya kutosha kutoka kwa wazazi wao na wapate kila kiti hata shamba, hata kila kitu kutoka kwa nyumbani na wote wachukuliwe kama watoto kwa sababu kuna wazazi wengine hawapendelei kusomesha msichana. Lakini ukisomesha msichana anaweza kukusasidia wewe sana hata kuliko kijana.

Ile mambo ingine ni ya ma barabara, tunauliza kwa ile Katiba sasa inatengenezwa mambo ya barabara ichunguzwa sana. For example we are here na kuenda Thika ni ngumu sana na tuko na mashamba pande ile na hatuwezi kwenda kwa sababu mabara bara ni mbaya sana.

Ile mambo ingine ni ya hospitali, tunataka kuuliza sisi akina mama, saa hii mkienda katika Kangundo hospital na Mwingi maternity ward hapo, mtaona mambo na nyinyi mshangae. Kwa hivyo tunauliza hospitali ziwe na madawa ya kutosha na

madaktari na kuwe na uangalivu kwa sababu wale madaktari wanafanya kazi huko wamejenga private clinic na wanaonekana kwa hiyo clinic zao. Lakini ukienda pale hospitali uwezi kuwaona. Saa zingine wanaenda kwa hizo hospitali usiku na mchan walikuwa kwa ile ma clinic yao. Sasa mgonjwa akiingia usiku anakuwa neglected na wengine wanakufa hapo hapo tu bila kuangaliwa.

Ile mambo ingine tunauliza kama tunaweza sisi kina mama tupate maji huko manyumbani, kila nyumba iwe na maji kwa sababu tunachota maji kila siku na tumechoka. Kwa hivyo tunauliza kama tunaweza kupata maji huko manyumbani kwetu. Niko na points zingine lakini hizo ningependa kuongea tukiwa sisi peke yetu. Asanteni.

**Com Asiyo:** (inaudible)

**Dr. Charles Kilonzo:** Jina yangu ninaitwa Dr. Charles Chalo Kilonzo kutoka hapa Tala ama Kangundo. Nitakuwa nikisoma maoni yangu kwa kizingu lakini sasa sijui nita translate haraka sana.

Tuko na wapigaji kura more than 60,000 ama elfu sitini na tuko na watu karibu elfu mia nne, hiyo inaweza kuthibitishwa kwa record na tuko na member mmoja wa parliamnt. Maoni yangu ni kusema Kangundo iangaliwe na serkali kabisa. Ionekane kama inaweza kupatiwa constituencies mbili kwa sababu tunaona saa zingine ma zonstituencies zingine, MP akiingia akiwa na kura elfu tatu. Hapa ma councilor wetu wanaingia na kura elfu tano, elfu sita. Mjumbe anaingia akiwa na kura elfu ishirini na kitu na wanakuwa watu kama nne kwa hivyo recommendation yangu iwe ikiwa kuna ugawanyo wa constituency, poluation, watu waangaliwe wakiangalia upana wa area. Hiyo ni kitu kimoja.

Ya pili ni Kangundo na Matungulu, iitwe Kangundo constituency, na Matungulu iitwe Matungulu constituency. Infrustructure ama ma bara bara. Ma bara bara yetu yote ni kama sehemu za kupitia ngombe. Communication iangaliwe kwa sababu communication ndio inasaidia raia kufanya business sawa. Kama mfano kama vile ule mwingine alisema, bara bara za Kangundo na Matungulu hazipitiki kamwe hata mumeingia hapa mumeona hii inakuja kwa shule. Tala Thika Road kwenda hapo ni 35 kilometers na hiyo bara bara kabisa haijafanyiwa gravelling for the last almost 10 or 15 years. Na huko bara bara kwa sababu tunaweka mkazo juu yake, ni kwa sababu iko na mashamba sita inaweza kufanya employment kwa wa Kenya na kuletea nchi hii mali ya kirasimi. Mashamba hii ni kama Mukamu, Chasavi farm, Matungulu farm, Kayatta farm na Kamatini na Matuu.

Hii mashamba kama Mukamu ndio shamba kubwa East and Central Africa lakini saa hii tunazungumza ilikuwa ina-employ watu karibu elfu tano lakini saa hizi it is grounded. Kwa hivyo tunaomba Serikali, ama tunaomba Serikali inaweza kutuhusisha na watu wengine wale wanaweza kuleta rasilimali hiyo shamba itupiliwe iandike watu elfu tano na hatutakuwa na chokora katika sehemu hii.

Hata agriculture, hapa katika sehemu ya Kangundo kuna furusa kukuza soya beans na flowers na very big projects which nimeshataja huk na zimeshafanyiwa na zikafanywa kama Mukamu na sisipoonekana zinafaulu kwa hivyo Serikali ikifanya hivyo itaongeza mapato ya watu.

Irrigation; hii sehemu yetu ya Kangundo inapita mto mmoja mkubwa sana unaitwa Athi River. Athi River ina-cover kama a distance of about 40 Km katika Kangundo lakini ukienda kamdo kando ya mto ya Athi River utakuta wale masikini hoe hoe ndio wanaishi hapo. Hawa watu masikini Serikali inaweza kujaribu kuangalia a policy inaweza kuchukua hiyo maji kuweka mahali ndio watu waanze kupanda hiyo mimea nilikuwa nimetaja hapo juu na watu watafanya agriculture na maneno itakuwa mazuri kwa mapato ya Serikali, mapato ya raia na hali ya maisha ya watu.

Ile ingine ni medical facility; Kangundo ndio hospitali ya kwanza ile iko hapa, inatoa watu kutoka Yatta division, Matuu na mahali kwingi sana. Inatibu watu mia tatu out patients na Kangundo iko na ward mbili mbili ya wanaume na wanawake, na watu hawajali ni ugonjwa gani wanaweka kwa hiyo ma ward. Tunashukuru Serikali kwanza kwa sababu ime-upgrade Kangundo ikafanya Nyayo ward lakini bado hatujakuwa kamilifu. Kwa hivyo tunahitaji Serikali iangalie ukubwa ya watu na ukubwa ya area na iwe inaweza kujenga ma hospitali kulingana na population of a particular area. Kama hapa Kangundo kwetu tungetaka hospitali kubwa kama kiasi ya Kangundo ijengwe kama Durisabuk moja iwe uko ingine iwekwe kama Kepkeroni. Kepkroni ni about 40 KM na ingine Kakuyuni dispensary ia-upgrade-we, Kitui, Kangundo ni kubwa sana. Huko nataja taja area zile za mwisho mwisho zile zinaleta wagonjwa Kangundo. Kwa sababu ya hospitali ya Kangundo ikiwa peke yake unakuta madawa za hospitali haziwezi kutosha watu hata ile dawa inaweza kutibu ugonjwa kama maumivu, panadol, haiwezekani kupatikana huko kwa sababu wale wanatumia ni wengi sana. Lakini tukiwa na health centers huko tunaweza kusaidia.

More hotel industries ama ni jua kali sector. Ikiwa lazima uwe na mahali kuna utulifu ama security, lazima vijana wetu watafutuiwe njia wanaweza kusaidiwa ndio wapate mapato yao. Vijana wakipata mapato, security lazima iwe kwa area na wazazi waendele. Ikuangalia kama upande huu tunataka tusaidiwe juu ya corporative societies. Vile maneno inaweza kutengenezeka, corporative societies zikuje upande huu tutengeneze si zile za coffee za coffee tukitengeneza tutakuwa tumefaulu sana. Lakini hapa tuko na sand harvesting, tandarau yote ina bebwa kutoka inaenda Nairobi inabebwa kutoka hapa, kama mawe ile inaenda Nairobi yote inatoka upande huu. Ukienda hapa kama kilometer mbili tatu hapa hivi utakuta sehemu moja tabarare, yote imejaa mawe na hawa vijana wanachukua hiyo mawe hawana tools hawana anything na hiyo ukienda hapo utakuta wanatuimbia vitu nduni kwa kutoa hiyo mawe. Wakifanyiwa njia yoyote ya usaidizi wapatiwe vitu ya kutoa hiyo mawe hawa vijana wanaweza kufanya kazi mingi sana. Tena hapa tuko na sculpt metal na tuko na electricity vijana wanaweza kuhusishwa na vitu ya jua kali kama vile tunaona kikomba. Kwa hivyo hiyo ni vitu tunaona ni kama inaweza kuangaliwa vile inawezekana ndio vijana wapate.

Education, mahali pa masomo ya primary school; primary school education should be free ama iwe ni ya bure kwa Wananchi sana sana kwa wale Wananchi wanatoka mahali hakuna mapato. A good policy ama utaratibu mzuri wa Serikali kwa kuangalia

vile masomo inaendeshwa inatakiwa kufanyika. Kama hapa kwetu Matungulu tuko na shule 64 na watoto mia nne kwa kila shule, na wanaendelea kuitishwa mapato kama unasikia kuna activity fee imeingia ya 40 shillings. Ninataka kusema mzazi hatakiwi kuitishwa pesa kama activity fee ile ambayo Serikali imesimamisha, kama levy, kama sijui ni gani kutoka standard one. Mtoto wa standard one kulipa activity fee ya shilling hamsini na hachezi hiyo tunasema kama Serikali iangalie hapo, iangalie kama ikiwa imeruhusu sasa iendelee kulipwa, lakini ikiwa haijaruhusu sehemu zingine zisifanye namna hiyo.

Na mwishoye nasema provincial administration ni mzuri, iendelee kwa sababu iyo ndio inafikia ma sub chiefs ndio wanawafikia raia. Majimbo ya Serikali, majimbo ile tunasikia inatakika, majimbo hatujakuwa tayari na majimbo kwa sababu sehemu zingine zetu haziko tayari, hazina mashule, kwa hivyo ikisemekana majimbo ifanyike sehemu zingine ambao hazijakuwa tayari zitaendelea kubakia nyuma. Life ya Parliament saa zote inasikia kuwa miaka tano, na MP ikiwa presideint anaambiwa akae term mbili, naye MP anatakiwa kukaa term tatu tuseme 15 years. Akimaliza term tatu hata akiwa mzuri aambiwe aketi.

Various appointments za Serikali, appointments za Serikali, zinaweza kufanywa na President lakini apatiwe list kubwa ya watu kama hamsini ikiwa anataka wawili either kutoka kwa Parliament ama kutoka kwa makanisa. Ikiwa ni Permanent Secretary, tuseme anataka ku-appoint Permanent Secretary, apatiwe majina kama kumi na tano na kutoka kwa Parliament ama kwa makanisa, ndio atachagua mtu mmoja kwa sababu ya hawa watu. Akifanya namna hiyo, kutakuwa taratibu mzuri sana. One-man one job, kazi moja mtu moja, saa zingine tunasikia mtu mmoja ako na makazi kumi, unamsikia director wa electricity, unamsikia director wa hii, unamsikia director wa university, one man one job, hiyo ni recommendation.

Wanawake wanatakiwa kulindwa kwa marriage. Ukioa bibi ukienda kuzungumza na wazazi na wamekukubalia kukupatia msichana wao, mwanaume anatakiwa kulinda huyo msichana kwa vile wamesema watalindana mpaka kifo. Inheritance, ikiwa msichana atarudi ama mama atarudi, mama ako na haki ya kupatiwa sehemu kama wale wengine kwa sababu ni mtoto. Mama anatakiwa kulindwa kuhusu mara masilahi ingine kama kupigwa, kupiga mama ama kumtoa macho, ama kum-rape ile kushika yeye kwa nguvu, hiyo inatakiwa kuangaliwa kwa ngumu sana kwa sababu hiyo ndio inatumiza, inaumiza familia mzima. Wanawake ndio kiini ya family mzuri, bila wanawake hakuna familia. Na kwa hayo machache ni meshukuru sana nimesema asante.

**Com Asiyu:** Asante sana. Kuna wale watu ambao hawakuuliza kuongea tukiwa pamoja na ninaona wakati umefika tugawe makao mara mbili vile ilipendekezwa hapo mbele, wale amabo sasa wataongea, wataongea hapa wengine wataongea kule ni lazima sisi tuchukue maoni ya kila mmoja ili tuweke pamoja tufanye analysis na tuandike report yetu na hiyo itatuwezesha kufanya hivyo kwa njia mzuri. Kuna mtu anaitwa .... You will be able to give your presentation sir but because it is written you only address us on very important issues for five minutes and then we take all the documents with; us. So can we now have the ladies have their separate meetings like they had requested and leave the Wazees to carry on with theirs na mtueleze tutaenda wapi. Thank you very much.

**Com Maranga :** Sasa mimi nitaita majina hapa, na please tutakuwa na dakika tano kila mtu anatoa ile maneno yake muhimu

ndio tuendele. Anthony Wambua Msebwa, hayupo? Henry Waema okay kuja hapa mzee wangu una dakika tano.

**Henry Kilata Waema:** Kwa majina ninaitwa Henry Kilata Waema. Ninazungumza juu ya pensioners association Kangundo Matungulu SACCO Societies Limited. hapa tumeandika memorandum ambayo nafikiri mna-copy na hapa ningewauliza mnikubali niende brief halafu niongezee kitu kidogo ambacho hakipo.

**Com Maranga:** Lakini una dakika tano, wewe ndio utajua vile utazitumia.

**Henry Kilata Waema:** Bwanacommissioner sijui kama hata hii dakika tano nitaweza kumaliza hata nikisoma kama machine, kwa sababu dakika tano ni kidogo, pengine kwa wale ambao hawana memorandum au ikiwa unafikiri. ...(interjection)

**Com Maranga:** Wewe soma tu lakini usisome yote.

**Henry Kilata Waema :** First item mimi ni mzee kama muonavyo nywele zangu, I am a retiree. Kwa hivyo kile nilikuwa nikisema sana ni habari ya pension ambayo tunapewa mpaka wakati huu. Pension structure ambao inaendelea sasa ilianzishwa wakati wa ukoloni. Hii pension ni after 37 or 27 years and 10 months, unapata your half salary. Kile ninasema juu yake ni hiki, ile scale tunapewa kama sisi, iko outdated kabisa sasa. Utakuta ninapewa shilling elfu moja na wale wamekuja nyuma yangu wanapata elfu kumi na tano. Siwezi kununua hata mkate, kwa hivyo hapa utaona kuna ... tunajaribu kuwapatia hapa mtasoma kutoka kwa nini kwamba lazima iwe revised tulipwe kulingana na present structure of economy au the purchasing power, we don't have the purchasing power because it is already outdated.

The other thing zile scale tulizo nazo, tulikuwa tukilipwa wakati wa ukoloni, wakati American dollar ilikuwa shilling saba na sumuni. Sasa iko 1998 or something like that. Kwa hivyo hata kile tunapewa ni kitu ambayo hatuwezi kujua, tufanyiwe conversion table, wale wazee wa zamani ili tuje in line with the present structure of salary, the lowest form of salary in Kenya Government. Kule tukilipwa, ninajaribu kwenda upesi zile important halafu mtasoma zile zingine, zile tukilipwa sisi civil servants, nikifa leo, bibi yangu atalipwa miaka mitano halafu pension inakwisha. Tunaomba mimi nikifa bibi yangu apewe pension yangu mpaka atakapokufa. Na ikiwa kuna mtoto yuko shuleni under 18, asomeshwe mpaka 18 years. Ikiwa kutakuwa na mwingine yuko university asomeshwe na Serikali mpaka amalize university course. Hii inaonekana kuna ubaguzi kidogo maanake ma bibi ya wale wako kutoka kwa watu wa Armed Forces, mpaka sasa wanalipwa, pension yao haisimamishwi ma Bwanayao wakifa. Hiyo kwa ufupi nitaiwachia hapo.

Kuja kwa children, tunaonekana state yetu au Kenya inaendelea na kupata orphan children kwa sababun ya ukimwi. Nafikiri tukiingilia katika either sub location or location, utakuta kuna watoto wengi sana wamewachwa na ma baba zao na mama zao hawana watu kwa hivyo hao ni orphans. Lazima Serikali ichukue hao watoto, iwalishe, iwasomeshe mpaka wafike 21 years. Hiyo inaongeza free education, caring for them and so on. Kuna hao watoto au watu wetu wanaenda kusoma ngambo vijana,

wanapata elimu ya juu sana na akipata elimu ya juu sana anakaa huko, we don't benefit from the education one gets. Tunataka Serikali iweke kama Sheria ya kwamba ukimaliza masomo yako ngambo upewe kukaa huko miaka kumi tu, ile ingine uje ufanyie hapa kwetu tupate faida yako.

Upande wa Serikali; tunaona sisi mwambao tunayo sasa inatutosha, hatutaki majimbo hiyo iendelee kama vile ilivyo. Katiba yetu majority ile ya ku decide iwe 65% kama vile ilivyo, hatutaki ibadilishwe, tuona vile iko hivyo ni sawa sawa.

Presidential powers should be reviewed to avoid favourism, nepotism na vitu kama hivyo. Nafikiri vile vingine ma commissioners mtasoma isipokuwa constituencies ni large kwa representation it is out of the way. Kwa hivyo lazima ziwe minimized ili minister au representative awe anaweza ku reach watu wake wale wamemchagua awafanyie kazi with ease. Kwa hivyo tunakubalian na hiyo. Nafikiri kwa hayo machache Asanteni sana.

**Com. Mutakha Kangu:** Mzee umesema watoto wakienda kusoma ngambo wasikae huko warudi. Na tumekuwa tukisikia watoto hata wale wamesoma hapa wanaambiwa waende watafute kazi huko. Mara ingine tunauliza hata ile university loan how do you recover, tunaweza kuwa na njia ya kusema watu wakifanya kazi huko nje, iwe kampuni fulani ambayo itarudisha hizo pesa hapa.

**Henry Kilata Waema :** asante sana, kwa maoni yangu binafisi, nilikuwa nikisema tuna specialized education. Science technology tunaikosa hapa. Elimu ambayo hatuna hapa tunaweza kuweka condition kama hiyo nimesema. Kwa employment tunajua hakuna employment, wakienda kule tunakubali waende wakafanye kazi. Lakini hiyo umeonelea walipe uchumi kidogo hata dhamini kabisa. Lazima mtoto akienda nje hata wakati tulikuwa tunachunga ngombe, tulikuwa tukileta maziwa nyumbani na inakunyiwa na watu wetu kwa hivyo huwezi kulima na ukatupa chakula iende na bahari. Kwa hivyo lazima watoto wetu wawe wanatukumbuka na wanatuletea na hii inaonekana sana sana wakati kuna michezo. Ukiwa unachezea club ya uko nje kama siku hizi au wakati huu ikiwa wewe ni footballer mzuri unaitwa unakuja ku-defend your country na sio sisi peke yetu. Kwa nini hao watoto wetu hawawezi kuja kutu-defend, we are old enough to do anything. Kwa hivyo nafikiri hiyo si mbaya.

**Com Maranga:** Asante mzee, nakuomba uende ujiandikishe kwa kitabu chetu rasmi. So thank you very much for your views. Sasa wacha ni muite aliyekuwa mkuu wa Sheria, Justice Matthew Gai Muli apatiane maoni yake kwa sababu inaonekana anaomba anataka kuenda kortini.

Huyu zamani alikuwa anaangalia Sheria ya Kenya wacha tusikie anatuambioa namna gani. Karibu.

**Matthew Muli:** Asante sana mwenyekiti commissioner. My names are Matthew Muli. I must be grateful for commissioners and the commission to visit Kangundo once more to receive views. I am addressing the commission, those behind me may



listen. Those I taught during the civic education may have known what I want to say and many of them who have given me views are all incorporated in my memorandum. It is not complete and that is why I ask for permission so that I may be given time to go in my office, it is not very far and see whether I can have it prepared. In Nairobi we have also some papers which I submitted, you know what Kangundo is, geographical, historical and other aspects which have been spoken very well by presenters particularly Chalo who was here as the first man.

Now what I want I to say is this and I am not saying it for Kangundo alone because what is coming out is not the Kangundo constituency alone but we will have a Constitution. We are talking about the Constitution of Kenya and the Constitution of Kenya this will be the fifth or the sixth Constitution starting with the colonial people. You have the many Constitutions which have preceded this but I will like to concentrate I don't want to start with little tone constitution, Lencovoy Constitution and Maclausse Constitution because it is the pinnacle of the Lancaster house conference Constitution 1960-63. That is the Constitution I am talking about. I saw it being made and I would like to see it demised. I have looked at it for 40 years and I know nothing about it then I am a fool.

Now I want to start off with a few observations; the first one will be technical and those I will leave to the technicians, where the technicians will be the legal draftsmen like my self who will correct me or correct themselves. I would like to see our Constitution being a supreme law of the land. Supreme law of the land both in name and in appearance and in practice. Having been a Member of Parliament, legislative Assembly and so on. But the Constitution is above every law and I would like it to be, the sections of it to be called articles, articles of the Constitution as opposed to sections and chapters, those endowed to Parliament.

The language used in the Constitution must be a simple straight forward English or Swahili whichever, I know both of them are national languages so that every one can read and understand, what is the Supreme Law of the land is. I have heard people talking about it, we would like to have the powers of the President looked into. The powers of ministers looked into, my question is by whom? You are here to look after those powers and say what they are now or forever keep quiet. It is very important to realize we are making a Constitution of the people by the people of Kenya not by the colonial masters.

So you are the ones to revise the powers of the President and when I am talking of the President I am not talking of honourable Moi or minister I am not talking about honourable Ngutu, I am talking about the main office people and they are people who are afraid of mentioning this because they think they are being looked at by those people. I don't care whether they head an office like the one I was heading because it doesn't bother me, Kenya must have a Constitution which is clearing all the colonial ridicules in it. If I were to do it I would only retain one sentence of the Constitution and that is Kenya is a sovereign democratic state, and cancel all the other sections up to the end and revise it (clapping) because 40 years I have been in pain in looking after this document. Because you are amending (inaudible) and once you amend this milk you bring it out of balance and it is quite easy that we are being ruled by a document which is dead. Tell me who knows about except those who perhaps have



seen it. So whatever we do the language must be understandable by everybody. We have a very high percentage of illiteracy among us. Who is going to read it? We would like someone to be able, even if he can't read well his children can tell him in a short form. The sentences must be understandable. There is no question of saying let there be a Parliament whose body whereas and so on unless and otherwise. These words must be gone, why can't you say there shall be Nicholas Chengo whose powers shall be this and finish. That is exactly the Constitution we want. Not things going in and out, we go ahead.

Now people have been talking about Preamble ; we no there is a Preamble to bills of Parliament and we know there are other Constitution which have got there Preamble , that is alright. Your Constitution, this one is just merely 40 years, you are talking of Constitutions which perhaps are much older and they have perhaps been, the ones around us have been scrapped from the same Lancaster house and Marlboro House, and we have been late in trying to revise this, and that is why we have difficulties. So the Preamble is meaningless. Why is it meaningless, it is meaningless because you cannot cover the contents of the Constitution? If you were to do so, you will have to buy a blanket as big as Kenya and cover it. You cannot do that, there is no need for a Preamble, it has no legal basis, you cannot use it for interpretation of a constitution, it is purely a statement, and why waste words to confuse people. There is no need to draw this Preamble, it doesn't help at all and if it is to draw it, it must be a very short Preamble. I can perhaps give you an indication; if you want to remember how you came about to get your Constitution it is easy to say *this Constitution is a remembrance of our struggle for self determination to obtain our independence or self rule*. Matter connected therewith incidental thereto. You don't need anything longer than that and if you do well then try to cover as much as you can in order not to look confused. So as a Preamble to me is meaningless without legal basis, and if it is you need something, I will recommend the marginal notes which are there at the moment to remain. For instant, in this section you can say, if it is a bill dealing with money you say, appropriation at to withdraw money from the consolidated fund or something to that effect. So there is no need to form any Preamble and there are many reasons as to why I say that.

Let me come now to one very important point; this Constitution is arranged wrongly. It is arranged in such a way that it does not give priority to where it should be. Why? You cannot put the cart before the horse, which is too near. Why are we putting the cart before the horse? First of all you must know the subject for whom you are making the Constitution, and I consider this to be very important and to be born in mind when those who are drafting the legislation should be that priorities must be heard. There is one more important point which I want you to take and that is, each article of a Constitution speaks by itself. It must be stand or fall by itself, you cannot use other articles to explain it. There is no cross reference, "it is there by established the national assemblies of Kenya subject to sub clause 90 of this constitution". What are you talking about? Have you seen section 90 before you define that? You have not seen anything. So you have no cross reference for the Constitution to other articles of the Constitution, it must stand and if you want to explain a little more it must be done within it and that is either by a provision (provided that) or interpretation of certain important strange words within that articles. You can't go to any other.

The other aspect I will mention is, we know we must have a head as madam chair said. You do not need for instance once you say Kenya shall be a sovereign state, it shall have a seal and so on" resolved. The next thing of course is the head the Executive

**Stephen Elijah:** You know there are checks and balances for everything. If a child does not request when they want to be born, and I don't think somebody because there are immigration laws that guarantee you to come to the country, then I think there should be some restrictions there. If you are just coming here expressly to benefit.

**Com Mutakha Kangu:** They won't tell you that they are coming for that. Assuming those Tanzanians traveling through Kenya and then Uganda, then labour pains come and she gives birth in Nairobi, will that child automatically become a Kenyan?

**Stephen Elijah:** That is why when they talk about the Constitution, it is you I know who will come out with the final draft but my strong sentiments are that somebody born here, even if it is a refugee should have that option because they came here because there was no security at home.

**Com Maranga:** Thank you very much Elijah. Now you sign our official register that you have appeared before the commission. Now I want to know whether these people are there. Joseph Malio, okay it is your turn five minutes and I can see you have a memorandum give us the main points Mzee. Utupe ile maoni yako ya muhimu halafu memoranda utatupa.

**Joseph Malio:** I am Joseph Motu Malio. Ningetaka kusema juu ya muundo wa Serikali yetu. Serikali yetu nataka iwe na Bunge mbili. Bunge ya kwanza iwe ya Rais na achaguliwe wazee watatu, retiree officers kutoka kila mkoa ambao atakuwa akiwasiliana na wao. Bunge la pili litakuwa na Waziri Mkuu ambaye anafanya kazi na baraza la mawaziri na wabunge. Hapo ndipo itakuwa civil secretary na ili uwezo ufikie mwanachi tuwe na Serikali ya mikoa. Yeye atakuwa hatoki nje anatoka katika katika area yake tarafa yake na atakuwa akifanya kazi na Mbunge wake. Hapo chifu atakuwa akiitwa Zultan. Ili uwezo wa Serikali ufikie mwananchi, hapo nchini iko mzee anaitwa mwaamuzi. Huyu mzee anafanya kazi ya Serikali mara mbili. Anafanya upande wa utawala na anafanye upande wa judicial department, anafanya kesi kama vile mwahakimu inafanya. Ningetaka huyo mzee awe akilipwa ili uwezo wa Serikali ufikie mwananchi. Ningetaka kila watu elfu arubaini wawe na constituency yao, wawe na Mbunge wao ili uwezo wa Serikali ufikie mwananchi.

Upande wa uchaguzi; rais achaguliwe peke yake, Rais kwanza awe Mbunge. Uchaguzi wa Mbunge na wa ma councilor ufanywe siku moja na Rais afanyiwe uchaguzi siku yake pekee. Kura ziwe zikihesabiwa kwenye kituo cha kupigia kura.

Upande wa elimu; primary iwe free education na university maan watoto wa masikini ndio wanapita vizuri nayo fee iondolewe

na ile ya secondary school irekebishwe iko juu sana. Iwe chini, kwa mwaka wawe wakilipa less than ten thousand shillings. Ningependelea kila wizara iwe na Tume kama vile mumeangalia barabara yetu kutoka Machakos kwenda Kangundo ilianza kujengwa miak na miak hata sasa haijamalizika na kama pangukuwa na Tume si wangeangalia wajue ni kitu gani inafanya barabara isimalizike. Tume ile ya corruption ipatiwe uhuru.

Upande wa mahakama; mahakama ipewe uwezo wa kuhukumu yeyote ambaye amekosea Serikali yetu hata akiwa ni nani, hata akiwa ni Rais apelekwe kortini na ningetaka mahakama yapewe waziri sababu Chief Justice ni mfanyi kazi wa Serikali na Mbunge akitaka kumchafua anachafua bure kwa magazeti. Na kama kungekuwa na waziri ndio angekuwa nasema Bungeni habari ya mahakama. Si Chief Justice aende kule ama AG, hawa ni wafanyi kazi wa Serikali.

Nikimalizia ni mengi lakini nilikuwa nimeandika utakuwa ukisoma kama unataka. Asante.

**Com Maranga:** Thank you very much and God bless you. Ongoja kidogo kuna swali, kabla ujaenda kuna swali.

**Com Mutakha Kangu:** Umesema Rais awe Mbunge na huo ndio utaratibu tuko nao sasa. Lakini swali ni kwamba kama kwa sahihi unaweza kuwa Rais kama wewe ni Bunge. Na huwa ninajiuliza kama tungeenda kwa kura na wakenya wachague wewe kama Rais lakini watu wa Baringo Central wakatae kukuchagua kama Mbunge, ungefanya namna gani?

**Joseph Malio:** Kwanza atakuwa Mbunge na aombe kura ya uRais akiwa Mbunge.

**Com Maranga:** Thank you very much Mzee, weka sahihi na utuwachie hiyo memorandum. Mwingine ninamuita ni pastor Matoyo, Benedict Muiya. Wakati ni wako dakika tano, uanze kwa majina yako.

**Benedict Muiya:** My names are Benedict Mbithi Muiya and I have come from Nairobi Principally to be with my people here at home because this issue of constitutional Review is very important for our country. Just to start I want to give the principles of governance which I think will do a lot in helping arrive at a good Constitution but it should be made complete. The principle and Government should be the system be complete in structure, give a perfect proportion and balance to bestow the powers to other parts, and the powers you will give it will never affect your security. This is the challenge of this honorable body for constitutional review as a whole as well as the individual members of the commission, because we hear some of them visit the President without informing their chairman, compromising the integrity of the commission. In a nutshell I want just to name or rather give the main points.

The problem of the Kenyan Constitution is that it doesn't give a proper definition of the system of governance which should be exercised in the country. At the top in the Kenyan Constitution or system of governance is presidential with an Executive head of state, Executive President being the head of state as well as head of government. At the bottom, the Kenyan system is

Parliamentary and it was essentially supposed to have been a Parliamentary and that is why Kenyatta became Prime Minister in 1<sup>st</sup> June 1963. How Kenyatta became the President of Kenya I am not sure and I think the 1<sup>st</sup> Republic on 12<sup>th</sup> December 1964 was fraudly done.

**Com Mutakha Kangu:** He was declared President by an amendment of the constitution.

**Benedict Muiya:** Yeah you can say that but without changing the law below.

**Com Mutakha Kangu:** I get your point.

**Benedict Muiya:** Now I will support a Mzee who was here that we should, whatever system we choose, we should have a separate presidential election and a separate Parliamentary, and civic elections. As far as the qualifications of the electable members to public offices starting with the councillors they should have a minimum of O level because a mayor who happens to come say in the cities, now we have three of them, is principally a councillor, and as the head of Government runs a Government, the central Government, a mayor is supposed to run the Local Government so we cannot afford to have an illiterate running a Local Authority because unlike the

Members of Parliament whose work is either support or oppose the Government policy, which the Government might choose to ignore, a councillor is directly involved in the running of the Government, a state activity.

The other issue is on the Government formation. Whatever system we choose and in the present Constitution say for example we have the President forming the Government from members of Parliament I would propose that if we elect people to represent us in Parliament they should not accept ministerial positions and if they do, they should cease to be members of Parliament otherwise they will be tied by the collective responsibility and no one will care for the interest of the people.

As far as the issue of we are going to be African, we cannot adopt what is happening in other countries we are in a new era. An era of information technology and free market economy and we must have a good team to lead us to be able to compete internationally.

I would conclude by saying that we must have a Preamble which will lead the country to a ripper in essence making it possible to separate completely the issue of the current or the coming election, from the repeal of the Constitution, because we were not reviewing the law to go for the elections. We were reviewing the law because of the flaw in the current Constitution. So the constitutional Review commission should continue with their work, we should continue with Parliamentary and civic elections. Moi should remain in office until he retires when his term expires after which either Parliament or the Parliamentary Select Committee together with the Ufangamano Group they will come together and appoint an interim President to run a Government for two years awaiting this commission to complete its work and implement the Constitution as per the letter as

would be requested by Kenya. Otherwise we don't have to rely on the politicians to give us the Constitution, because like now, when we talk of reducing presidential powers we are asking for a presidential system.

The Parliamentarians are already arranging themselves in what will appear they want a Parliamentary system. So I think also this interim Government, will have to ask for something special, because we don't want a situation whereby the Members of Parliament will take it upon themselves to try to impose on Kenya the system of governance which we have not yet agreed on. So we will have to hold a referendum, so I will ask this commission to prepare three different draft constitution. One on presidential system as the people have been proposing, another one on Parliamentary constitution, a pure one like the British one, and the third one mixed as the former AG said.

**Com Maranga:** I thank you very much Benedict, you are beyond time thank you and give us your proposal; please sign our register. The next person in Joseph Nzuki Kasyoki. Hayuko, then we have Mutistya Kangera, kuja. Haya nataka kujua kama hawa wako. Philip Munguti, is not there then we have Wambua Kiani is not there, then we have John Ngovi Kithuka, Muthama Kithika. Basi wewe you will be the last person before we go for lunch. Sasa tuna huyu anaitwa Mutisya Kangera, anza kwa majina yako mzee una dakika tano.

**Mutisya Kangera:** Mimi ninaitwa Mutisya Kangera. Mimi kwa wakati huu maoni yangu kwanza kabisa ni ya hospitali. Sisi kwanza walemavu tunapata shida sana kwa hospitali wakati mtu mlemavu anakuwa mgonjwa. Pesa tunapewa za kupimzwa, wakati tunafika kwa hospitali daktari akikuta wewe hauna pesa za kutosha anakupita, anakupita mpaka jioni unarudi bila kutibiwa. Sasa kwa hii Tume ya marekebisho ya Katiba hatujui ni njia gani wangetumia mlemavu awe anapata huduma ya kutosha katika hospitali.

Ingingine sisi walemavu kwa wazazi tuna shida sana, si wengi wana mashamba akapata title deed, shamba kutoka kwa baba yake. Kwa vile wanasukumwa na wenzao wenye kusismama. Akisema shamba anasukumwa ni ya nini, wewe mama wacha kumpea, wewe baba wacha kumpea. Kwa hivyo walemavu tunataka huduma ya kutosha hata kwa Serikali.

Hata kwa biashara sisi walemavu tuna shida sana kwa Local Government town council. Tukiuzia ikiwa ni nyanya tunanua, tukiuzia pande hii, mwenye kusimama, yule mama anakatisha receipt ya town council anakuja anaambiwa wewe kwenda pewa pale. Wakati anaambiwa, "pewa pale" mimi nikimwambia "bado kuuza" anaambiwa anazo. Sasa anakuja kupiga nyanya yangu teke. Chifu ndio anasaidia, hata makaa, chifu ndio anasaidia. Tuna shida sisi walemavu. Wakati ministry ya local Government kama country council wanagawa vibanda vya kuuzia, sisi hatupewi nafasi ya kwanza. Wakati huu ninasema hii hakuna mtu ninashtaki, tunatengeneza marekebisho ya Katiba tupate nafasi, tunalilia nafasi.

Ile ingine ni...

**Com Maranga:** Malizia hiyo ni ya mwisho.

**Mutisya Kangera:** Ninabakisha mbili, hakuna mlemavu mwingine alisema hapa, ni mimi tu. Ile ingine ni watu wa health, ministry of health nikikomboa hotel mimi ninapata shida kwa vile sina pesa ya kumpatia akija. Hata nyumba ikiwa ni mzuri ananiambia hiyo funga, hakuna nyumba na hata hii ya mwenzangu ni kama hii yangu na mtu wa health ananifungia ndipo huyu mwingine awe anapata customers wale walikuwa wake na wale wangu. Hata ikiwa ni wiki moja, hajali anasema amepata, hizo ameingiza na mimi yangu kifuli. Wakati anakuambia funga ukija kufungua uje kwa ofisi yangu, anakuambia ni pesa fulani ukienda kwa ofisi, elfu mbili na hizo elfu mbili wewe hupata kwa hapa hata ukifungua mwiezi mzima wewe hupati faida.

Ile ingine iko kwa primary school; nilisikia watu wengine wakisema ati Chokora ni watu wa kina mama ambao wasioolewa. Wengi wao ni wa walemavu, ni kwa nini? Yeye hana nafasi ya nyumbani, na yule mtoto wake hana pesa, kwa maana hajui kujufanyia kazi na hana nafasi, haoni karo ya kulipia huyu mtoto na ile tunaita yellow, h iyo inaleta shida sana kwa mtoto wa mlemavu, inaleta shida sana kwa mtoto wa mlemavu, na nimlemavu awe kiziwi, awe kipovu, awe mlemavu wa mkono kama ama mguu kama mguu kama mimi.

**Com Maranga:** Pendekezo yako ni nini sasa?

**Mutisya Kangera:** Mapendekezo yangu ni haya ingawe, iteremushwe, ifikie kiwango cha chini anapofikia, inakuwa wasitani.

**Com Maranga:** Umemaliza?

**Mutisya Kangera:** Ninabakisha ile moja sasa. Ninarudi upande wa kura, hapa sisi Kangundo tuna shida ya kura. Watu wa Kangundo wale wanataka kura wanajua hesabu ya kura na hawajui hesabu ya walemavu. Ukimuuliza mlemavu awe kiziwi, awe nini, hajui, lakini hesabu ya ile kura ina mlemavu anajua. Hesabu ya kura kwa ma councillors ama ma ministers ama nini Kangundo wanajua lakini hesabu ya walemavu awe kiziwi awe kipovu hawajui na Kangundo hii yetu haina harambee ya walamevu ama nini lakini tunaisikia kwa radio. Harambee ya walemavu na harambee ya walemavu iko Nairobi, iko Kisumu, iko wapi lakini Kangundo walemavu hawana, na hawajulikani. Kwa hii Tume ya kurekebisha Katiba tunauliza tutajulikanaje sisi wa Kangundo.

**Com Maranga:** Unataka wewe tufanyaje, tupe mapendekezo.

**Mutisya Kangera:** Ninataka tujulikane namna hii; huduma ya kwanza mlemavu ajulikane inaweza kutoka kwa councillor. Wa pili kujulisha Serikali ni Chifu ama assistant chifu, tukifika kwa DO, kwa minister kwa maana ndio wako kwa hii ward wanajua na wanajua kila mtu ako hapo.

**Com Maranga:** Asante sana Mzee wangu Kangera. Weka sahihi kitabu chetu rasimi kuonyesha kuwa ulifika mbele ya Tume. Asante na ninakushukuru kwa maoni yako. Yule ambao tunataka sasa akuje hapa ni Mthama Kithika.

**Mthama Kithika:** My name is Gabriel Mthama Kithika. I will start with the Constitution it self.

**Com Maranga:** You have five minutes.

**Mthama Kithika:** You can give me an extra minute. Most of us don't know the old Constitution and I will suggest that copies of the old Constitution be availed in all public offices and schools so that people are able to see what the old Constitution talks about.

Secondly is that as we get to the new Constitution we should have mechanism where elements of the Constitution are taught in schools may be both primary and secondary so that future voters know what is required of them.

My second point is on public offices or public bodies. We have so many public bodies including schools, universities, parastatals. I think the Constitution should be very clear that any monies which is got from the public must be accounted to the public, because we are paying school fee, we are paying university fees we are paying. Local Government taxes and no body knows what happens to that money except the people involved. So any money which comes from the public I think there should be an annual balance sheet which is given to the public so that they know how there money has been spent and they can question it if they need to.

Then the third point is on Local Government.

**Com Maranga:** I want to interrupt you, imesemekana nyinyi mnaongea kimombo sana akina mama hawaelewi. So rudi kwa Kiswahili kidogo.

**Mthama Kithika:** Nitaongea Kiswahili. Hii ni Serikali ya mitaa; juzi Bunge ilipatia wana Bunge, pension schemes medical schemes; Kwa sababu wanachaguliwa na wananchi, tungetaka hiyo pia ipatiwe madiwani kwa sababu pia wao wanatumikia wananchi. Kwa hiyo hatutaki pale inakuwa anatomia pesa yake ili ahudumie wananchi. Kwa hivyo wapatiwe hiyo mshahara, wapatiwe pension kama inawezekana. Kuna hii timetable, hawa madiwani wanakutana mara kwa mara, wananchi hawajui mikutano hiyo ni ya nini na ningetaka kuwe kama Bunge. Kama kuna mkutano ya local authority iwe inawekwa kila mahali, kila mtu anajua kuna mkutano wa ma councilor leo na hiyo hall iwe open, inafunguliwa wananchi ili wajue vile ma councillor wao wanafanya kazi kwa sababu sasa iko kama closed house, ni wao wenyewe wanajua vile wanafanya, ni wao wenyewe wanajua vile wanatumia pesa na hii pesa ina toka kwa wananchi kwa hivyo ningetaka ikuwe open na kama ni zile minutes wanaandika



zikuwe uhuru kusomwa na kila mtu kwa sababu sasa hazisomwi, you have to struggle to get them. Pia ningetaka wawe wakifanya budget kama ile Serikali kuu inafanya annual budget, wanafanya na iwe wakaazi wa sehemu hiyo wanaandikiwa wagawe namna gani sababu akiitisha kodi kama ya wafanyi biashara wangetaka hiyo pesa inatumika namna gani, mambo ikikwisha waambiwe tulifanya hivi na hivi. Wakitaka kuongeza waseme wataongeza sababu gani au wana reduce with reasons.

Then ile kitu ingine ni corruption; mtu yeyote ambaye anapelekwa mahakamani kwa sababu ya corruption anataka aondolewe kwa kiti yake amara moja. Juzi tulikuwa na waziri anaenda kwa corruption case na yeye still ni waziri. Kwa hivyo mtu wowote anaenda kwa mahakama ya corruption a-vacate the seat I don't know what you call orphans in Kiswahili.

Mayatima na widows, tuko na mayatima wengi sana na wajane kwa sababu ya hii, may be sababu ya ukimwi au tofauti nyingine. Hawa mayatima ningetaka Katiba iwatambue, wawe wanapatiwa elimu ya bure kutoka primary mpaka university kama wanaweza kwa sababu hawana baba hawana mama, na wanawachiwa wale relative wengine. Kwa hivyo ningetaka Katiba iwatambue wawe wanapatiwa eleimu ya bure na baada ya elimu ya bure kuwe na reserved jobs katika public sector na pia ningetaka hiyo kazi iwe reserved kwa wajane kwa sababu kuna kina mama wanaumia sana Bwanawao akifa wanaumia wanaumia na kuna kazi inatokea kwa mpublic sector na wengine ni qualified. Kwa hivyo ningetaka wapatiwe nafasi ya kuingia hiyo kazi on the basis of being an orphan or a widow.

Land...

**Com Maranga:** Na hiyo ni yako ya mwisho.

**Mthama Kithika:** Land huyu commissioner wa lands ako na uwezo mkubwa sana na ndio ameleta corruption Kenya. Hiyo uwezo anapatiwa wa kugawa land uondolewe kabisa kutoka kwake na kama land iko Kangundo wananchi wa Kangundo ndio watajua vile watagawa hiyo land, kama ni ya Serikali. Kwa sababu ikigawa na mtu wa Nairobi, hajui ni nini inaendelea huko kwa hivyo kama kuna land huku in any particular area, wenyewe waamue vile watafanya na hiyo land kama wanataka kugawa otherwise ikae kwa public trustee.

General elections ningetaka kama candidate anakufa wakati wa elections, between nominations and elections, huo uchaguzi uhairishwe. I think there is a vacuum right now.

Na katika uRais ningetaka Rais achaguliwe na watu 50% ya voters. Kama kuna watu kumi wanapigania uRais na hakuna mwenye anapata 50% wale wawili wako juu waende wapigania hiyo kiti ya uRais kwa sababu kutakuwa na mtu ambaye ana-represent watu wote, sio ana-represent quarter na pia ningetaka Katiba iweke mechanism ya hand over or take over. Hii kwa sasa iko na electoral commission ipatiwe uwezo na time frame. Kama election ya leo wepatiane majibu kesho, kesho kutwa Rais akuwe sworn in seven days or whatever, kwa sababu sasa inategemea na yule mwenye hiyo ofisi. Kwa hivyo



ningetaka hiyo iwekwe ikuwe clear kwa Katiba.

Ya mwisho ni appointment ya public officers; Serikali ina uwezo ya ku-appoint here and there. Hii kitu tungetaka iwekwe kwa constitution. Ijulikane Rais anaweza ku-appoint nani, minister anaweza ku-appoint nani na kama anafanya hiyo appointment ipelekwe kwa Bunge, ifanywe ratification, kwa sababu sasa tuna shida kila mtu anakimbia kwa Rais akitafuta kazi. Hiyo ma kazi ya public ikuwe kazi yake in the public wajue ni nini inaendelea. Ni hayo tu.

**Com Maranga:** Thank you very much for your presentetation.

**Com Mutakha Kangu:** This 50% yenye tunasema President apewe, kwa nini tuiseme hata wa Bunge, hata councillor kwa sababu tunasema kwa sasa unapata President akipata 30% na wale walipia opposer walikuwa wengi. But the same things happens even with the MPs. Ukipata pengine 10 candidates yule mwenye ameshida pengine amaepata three thousand votes na wale walipiga against him ni a total of ten thousand, kwa nini tusiwekee hii hata kwa wa Bunge na councillors.

**Mthama Kithika:** Hiyo ni kweli, sioni kwa sababu gani isiwekwe.

**Com Maranga:** Okay asante, nina kushukuru sana sasa wewe ninakuuliza utuwekee sahihi na utupatie memorandum. Kuna akina mama wawili hapa hata ingawa hiki kilikuwa kikao cha akiina baba tunataka akina mama wawili, inaonekana akina mama walikuwa wengi sana kuliko akina baba. Sasa kuna mama moja anaitwa Christina Muindi, kuja uzungumze maneno yako halafu atafuatwa na Veronica Suambwa, ukae karibu hapa. Halafu tutafungiwa na chairman wa county council, councillor Chengo, haya kuja, kuna mzee mwingine hapa nimewacha ambaye alikuwa anataka kuongea kwa hivyo mimi nimeona wazee wawili nitawapa dakika moja moja mtoe maoni. Unaongea lugha gani, Kiswahili ama Kikamba?

**Christine Muindi:** (in kamba dialect) Ninataka Kusema Kuhusu watoto yatima: na watoto yatima wanapata shida ya fees sana. Baada ya kusoma hadi class ya nne mtoto anakosa fees na hata kupata barua kwenda nayo akatafute kazi ajulikane amepata nini baada ya elimu. Ninahitaji msaada, watoto kama hawa mayatima wasaidiwe ndiposa waweze kuwa na elimu ya kuwawezesha kupata kazi. Hiyo tu ndio maoni yangu ninataka kusaidiwa.

**Com Maranga:** Asante sana mama. Enda uweke sign kitabu chetu na hiyo ni mzuri. Haya huyu mama mwingine Veronica Suambwa.

**Veronica Suambwa:** Jina yangu ni Veronica Suambwa, Peter Nguli. Maoni yangu vile nataka kusema ni hivi, watoto yatima wale ambao hawana mama wala baba na wengine wale ambao wako na mama peke yake ambao ni watoto wetu. Watoto hawa wako na shida zaidi kwa sababu wanahitaji chakula, wanahitaji school fees ama Karo na wanaitaji uniform. Watoto hawa ukiangalia sana wale watu wa kijiji hawawasaidii, hawa watoto wanawachiwa mama au baba au pengine hawana wazazi.na

wale nimeona hawana wazazi ama babu na wamewachwa namna hiyo hadi wanaendelea na kuranda randa humu humu.

Jambo ingine nitaongea ni kuhusu kilimo ya kahawa. Kina mama wale ambao hawana ma Bwana walikuwa wanajisaidia na kupikia kahawa na hiyo kahawa imekosa bei kwa hivyo tunaangaika hata kina mama wengine karibu wafe kwa ajili ya jaa, wanakaa hivyo. Na ukienda kwa factory ukauliza pesa unaambiwa enda. Hata wengine wamezeeka zaidi kwa sababu hawaoni chakula. Ni nauliza Serikali iangalie zaidi.

**Com Maranga:** Wacha nikuulize, unatakaje, una njia yoyote ambayo unataka kusema tufanye kwa sababu hiyo serikali imejua hiyo maneno hizo siku zote, sasa unataka tufanye je?

**Veronica Suambwa:** Mimi ninataka Serikali iangalie hao watu wazee au vikongwe maana hawana pahali wanaweza kupata usaidizi.

**Com Maranga:** Thank you very much. Enda uweke sahihi. Haya ule mzee wangu wewe mimi sina jina lako hapa, wewe ninakupa dakika chache hivi utoe maoni kwa sababu hata wewe sio official haupo kwa hii list yangu. Wewe sema majina yako.

**Boniface Mutuku:** Mimi ninaitwa Boniface Mutuku Kisule. Kwanza mimi ninatoa shukurani kwa hii Tume. Kwa maoni yangu ningetaka kuona Serikali moja mabyo ina Rais na makamu wake na Rais ambaye hana uwezo isipokuwa ni mkubwa wa nchi. Katikia hiyo Serikali kuwe na Prime Minister ama waziri mkuu. Waziri mkuu ndiye ambaye atakuwa na uwezo wa kuchagua, kuweka cabinet minister akiwa pamoja na parliament. Tena vile vile ulinzi katika Kenya umedhoofika zaidi. Kwa mfano uliwacha kusikia President fulani ameuliwa mahali fulani na wale wenye kufanya hao maovu hawatashikwa kwa hivyo ulinzi katika polisi umedhoofika.

Tena vile vile mkuu wa majeshi asiwe Rais, jeshi liwe na mkuu wake.

**Com Maranga:** Endelea Mzee.

**Boniface Mutuku:** Tena vile vile kuwe na korti ya Katiba. Tena vile vile kuna wale mashujaa ambao wamepigania uhuru wa Kenya na hawakupewa kitu na serikali yetu, waangaliwe. Utabibu katika Kenya uko katika hali mbaya maanake masikini anaweza kufa bila usaidizi wowote. Akienda katika hospitali anaitishwa kitu fulani. Kwa hivyo utabibu uwe free kwa kila mwananchi. Elimu ipeanwe bure kutoka primary mpaka form four.

Mashamba ya Kenya, kusikubaliwe mtu kuwa na 100 ama mia moja heka na kuna wengine ambao hawana kitu. Tena vile vile, utawala administration, cheo cha PC hakifanyi kazi. Kuwe na minister wa administration na cheo cha PC kitolewe tuwe na DC na kuwe na minister wa administration.

**Com Maranga:** Malizia oni lako la mwisho.

**Boniface Mutuku:** Kwa hivyo mimi ninasema ni asante kwa vile umenipatia ruhusa hii.

**Com Maranga:** Asante sana Mzee Kisula. Haya mzee mwingine ni huyu. Maoni fupi kama ya huyu mzee dakika mbili tu kwa sababu unaona nyinyi ni watu wa ziada. Machine yetu hapa, I hope it is working.

**Paul Muthama Kimomo:** Paul Muthama Kimomo.

**Com. Maranga:** Kimombo?

**Paul Muthama Kimomo:** Kimombo.

**Paul Muthama Kimomo:** Anza maoni yako Mzee. Hebu tusikize huyu Mzee. Ya kwanza ni ukulima Kangundo. Wacha mahali pengine, Kangundo.

**Com. Maranga:** Hii ni Katiba ya Kenya, tunaelewa.

**Paul Muthama Kimomo:** Weka Katiba ya Kenya lakini mimi nasema Kangundo. Sisi wakulima wa Kangundo hasa tuseme Kenya yote ni wakulima lakini Kangundo, sisi hatuna mtu wa kutuangalia tunafanya nini. Ukulima yetu yote ni bure.

Number two, clan. Unajua *Mbayi*?

**Com. Maranga:** Mbayi najua. Hiyo ni kali sana, unataka?

**Paul Muthama Kimomo:** Mimi naingilia hapo. Clan ni kitu tulikuta kama wazee wetu hata wa mbele wanatengeneza maneno kwa clan, na siku hizi tulikaa chini tutengeneze maneno kwa clan na sisi ndio tunajua hawa ni wezi, huyu ni mjeuri, huyu ni nini. Clan inajua namna hiyo na haipendelei. Kama sisi tunakaa chini tufanye hiyo, mtu anakimbia anakwenda kortini ule tunafanyia kesi, alipiga mamake, aliiba ng'ombe alifanya nini, tungeeka clan. Ule mtu sisi hukalia tufanyize maneno yake, anakimbia Kangundo, anashtaki sisi, sisi wote (inaudible), tunaingizwa ndani ya jela. Mimi sikuona ukiandika hiyo?

**Com. Maranga:** Nimeandika (inaudible). Unataka iwe kwa Katiba? Na hujasema *Kithitu*.

**Paul Muthama Kimomo:** Kithitu mimi nitasema.

**Com. Maranga:** Endelea.

**Paul Muthama Kimomo:** *Kithitu* ni mapatano ya wakamba sana na kivotu tunalisha yule mtu, anashindana anasema hajui maneno hii kabisa na sisi tunajua yeye anajua. Na tukikaa kwa mbaia, tunasema leteni ng'ombe tutengeneze *kithitu* huyu akule na tukimuitisha ng'ombe, akikataa kulete au alete, tule na tufanye kithitu anakwenda kushtaki sisi kwa Serikali. Halafu sisi tunasumbuliwa wote na Serikali hapana uliza sisi mlikuwa mnafanya nini. Ah Ah, ukifika kortini, line. Nyinyi nyote mko na hatia. Hiyo umeandika?

**Com. Maranga:** Eeh. Mzee, ama unataka kuangalia. Sawa.

**Paul Muthama Kimomo:** Sawasawa. Ya nne ni Bunge, Wabunge tuseme. Na ukisikia lugha yangu wewe angalia mimi.

**Com. Maranga:** Najua. Nasikia maneno.

**Paul Muthama Kimomo:** Ongoza lugha wewe. Wabunge sisi tunastaajabu na sisi tunachoka. Afadhali Serikali ifunge kabisa. Halafu waandike watu huko reserve wa kutengeneza maneno. Kwa sababu Bunge sasa ni miaka ngapi? Wanafika Bungeni na mdomo prr prr prr. Hiyo wanaandika bure, sijui inaandikwa, sijui inafanya nini. Huwezi kuona Mbunge anakuja kuuliza watu ile maneno tulikuwa tunasema, hii ni mzuri au ni mbaya. Na hii inanyamazia hapo kabisa. Kama sisi sasa, wewe tunasema, sisi tunasema na wewe, wewe unaandika na hii maneno itakwenda kutongomea sijui baharini, sijui wapi.

**Com. Maranga:** Itarudi hapa.

**Paul Muthama Kimomo:** Itarudi hapa. Tuyasikie. Sasa sisi tunataka muunde namna hiyo.

**Com. Maranga:** Shida tu ni wengine wanataka...

**Paul Muthama Kimomo:** Bunge sisi tunataka namna hiyo.

**Com. Maranga:** Mwisho.

**Paul Muthama Kimomo:** Inginge. Nipe nafasi kidogo. Pesa inaletwe mpaka kwa skuli iletwe watoto na bursary inapeanwa na mwalimu peke yake. Anaambiwa ndiye anajua watoto wale maskini. Kwa kweli anajua lakini atampa ile yao. Pesa yeye analetewa na yeye anatengeneza nitampa nani na si yake, ni ya Serikali. Wazee waitwe, wa-commit. Waambiwe tuangalie watoto maskini. Walipwe bila kubishana.

**Com. Maranga:** Endelea.

**Paul Muthama Kimomo:** Ile ingine ni station ya polisi. Station ya polisi sasa yote inakuwa korti tupu. Inataka fine. Ukiingia hii fine, ukifika hii fine, ukifika kortini, wewe hoi. Mahali wewe unapelekwa unatoa fine. Sasa hii korti itakuwa ngapi ya kutosha fine? Ya mwisho.

**Com. Maranga:** Hata mimi nashukuru, endelea. Lakini....

**Paul Muthama Kimomo:** Mimi nasema...

**Com. Maranga:** Hiyo ni ya mwisho.

**Paul Muthama Kimomo:** Ya mwisho.

**Com. Maranga:** Okey. Fine.

**Paul Muthama Kimomo:** Ya mwisho. Mawaziri wanachaguliwa Bunge halafu wakifika huko, Serikali inampa mtu waziri. Sisi tunataka kujua. Yule Waziri alipewa Waziri wa Kisumu, anafanya kazi Kisumu. Je ni Waziri wa Kenya au ni wa Kisumu? Kwa sababu wako watu walichaguliwa tuseme kwa mfano, kama Waziri hapa kwetu, hawezi kujulikana Waziri ni wa Kenya yote. Waziri akiwa ni wa labour, akiwa nini, akiwa nini. Si Kenya yote, kwa nini hawatembezi? Hapa kwetu Waziri wa Health hata wa nini hakuna mmoja anafika hapa kuchukua shida zetu. Hakuna. Sasa yangu inakwishia hapo.

**Com. Maranga:** Asante sana Mzee. Nafikiri kutakuwa na swali kutoka kwa Commissioner Kangu, lakini yangu ya kwanza nataka kukuuliza. Hii Kithitu, sasa tukiiweka kwa Katiba, hawa vijana wetu hawa, hawa ambao wako shuleni saa hii primary, secondary na wengine wako University, wanajua haya maneno? Kila mtu anajua? Hata hawa wanafunzi?

**Paul Muthama Kimomo:** Ah ah. Wanazaliwa na wazazi hapa Ukambani.

**Com. Maranga:** Lakini wanajua?

**Paul Muthama Kimomo:** Hawajui.

**Com. Maranga:** Kama hawajui sasa tunaweka Kithitu ya nini, baada ya miaka kumi, kumi na tano, hakuna mtu atasaidiwa nayo.

**Paul Muthama Kimomo:** Sisi (inaudible). Kwa nini hautwambii? Kwa nini hautwambii ni mbaya, kufanya hii hatia hii. Tukipikiwa Kithitu, tutakufa.

**Com. Maranga:** Sikiza swali langu. Tutaweka Kithitu kwa Katiba lakini watoto wetu wote kama wale msichana wako na kijana yako, wote wanakaa Nairobi. Hakuna wakati wamekuja nyumbani hapo waambiwe, hii ndio Kaiti ama hii ndiyo Kithitu. Sasa, ni wakati gani watakuja wakiwa wazee kama wewe. Ni wakati gani watakuja kufanya hayo maneno? Na tumeweka kwa Katiba.

**Paul Muthama Kimomo:** Sasa hiyo inawezekana kama watu wanaulizana.

**Com. Maranga:** Unataka iwe hivyo kwa ile tabia ya kikamba na makabila mengine, watoto waelezewe. Hivyo?

**Paul Muthama Kimomo:** Mimi naondoka...

**Com. Maranga:** Ngoja kwanza unaulizwa swali ingine.

**Paul Muthama Kimomo:** Ngoja kidogo. Ngoja Baba. Mimi nauliza habari ya Bunge. Nakwenda Bungeni, sasa siku hizi, na uandike hiyo yangu sawasawa. Sasa siku hizi, wanasema tuangalie watoto sawasawa. Na wanawake wale wanapewa madaraka, si wanakuwa na bwana, sasa akipewa madaraka na sasa mnampa yeye hukumu ya kuhukumu sisi, si tutafungwa sote.

**Laughter from the audience.**

Wana DC wanaoa wana DC. Unaoa DC na wewe si DC. Sisi akikwambia amri yake utakataa. Hata mkiwa nyumbani mnalala, anakwambia, 'utashika adabu hiyo'.

**Com. Maranga:** Sawasawa Mzee, tuachie hapo. Maneno ya mbayi tumeyasikia kwingi. Hata kule Coast, watu wanalia ile sehemu ya chini ya wazee, ihusishwe kwa maneno ya utawala (Governance) na vile unasema kweli naelewa. Mimi nimekuwa kortini nimeona unapata watu wamejaribu kuamua maneno nyumbani kufuatilia vile walikuwa wanatumia mila zao, lakini wanapelekwa kortini, wanashtakiwa assault and so on na watu wakisema, na mimi nimekuwa huku Ukambani najua kweli, mbayi ikitoa uamuzi, hakuna yule anacheza. Lakini siku hizi tuko na makorti, unapeleka huko mtu, mtu hajali. Unabeba mtu unapeleka kwa DO, ana-ignore. Unapeleka kwa Chief ana-ignore, lakini ikifika mbayi, wakipaka yeye ile kali sana. Anasikia maneno. Sasa, mimi ningeuliza, na ni jambo hata kama Mzee hana jibu saa hii, mfikirie sana. Mtupatie hata kama ni written memorandum.

Ni njia gani, hiki kiwango cha wazee kinaweza kuingiza kwa Governance structure ndio iwe wakichukua hatua, ionekane wamechukua hatua kisheria nao wasipelekwe kwa korti kusemekana wako na makosa? Na ikiwa tutakuwa na utaratibu kama huo, wengine wameshatoa maoni hapa na kwingine wengi wakisema, kuna sehemu ya wazee wa kijiji. Inaitwa village headmen. Wamesemekana wanafanya kazi nyingi na hawapatiwi mishahara.

Watu wanalia wapatiwe mishahara, sasa ikiwa tutaongeza hii kiwango, pia tuwe tunajua tunaongeza kiwango itawekwa kama sehemu ya Serikali na hata hawa wapatiwe mishahara fulani na wawe na utaratibu fulani wa kufuata ama tunasema wazee wenye watawekwa, tena iwe wameachwa bure bila mishahara. Sasa iwe wakiita kesi, wanaanza kuitisha pesa kwa watu. Ningependelea mfikirie, mpeane utaratibu wa haki. Kwa sababu vile unasema mimi najua, hata hii mambo ya ufisadi. Watu wanalia corruption, corruption, ikifika kinyumbani, watu wanaweza pata discipline. Lakini kuenda juu inaonekana hakuna discipline na watu. Watu wana-ignore. Unafikiria tupange utaratibu wa aina gani?

**Paul Muthama Kimomo:** Kwanza hawa watu wa County Council na ma Assistant Chiefs, hawa hiyo ni kazi ya kujitolea. Kujitolea tu. Kwa sababu ukikataa, hakuna mtu atafunga wewe. Hakuna mtu ataita wewe kwa kesi. Unaweza kataa, useme huwezi kusema ya bure, uende shambani kwako. Sasa hii ya mbayi, yenyewe, sisi unajua wako Machairmen wa Division, wako wa Location, wako wa sub-branch, wako wa District. Na hawa wote wanafanya kazi bure. Tunajitolea kuona watu, nyumba hii iko makosa, huyu mtu anasumbuliwa na watoto wake. Mama huyu anasumbuliwa na watoto wake an sisi tunaingilia pole pole. Hapana kimbia. Pole pole, tukaite wale watu wakae hapa. Wewe ulifanya hii na hii na hii. Sasa mtu akienda kukataa kabisa, sisi tunapeleka jela, korti tunafanya kesi naye. Sasa makosa iko wapi?

**Com. Maranga:** So, tuseme, kitu unachosema ni kwamba kuna wale wanasema kwa Kiingereza ile inaitwa 'alternative dispute resolution'. Yaani kiwango fulani ya kuanzia kutatua maneno. Kama imeshindwa hapo, ndio iende kwa kiwango ya kortini na namna hiyo. Inatakikana mfikirie, ikiwa tunaweka mbayi kama hiyo, ni maneno aina gani inaweza pelekwa kwa mbayi, ianzie huko na ni maneno ya aina gani itatakikana ianzie kwa korti juu. Sitaki ujibu saa hii lakini ni maneno mnatakikana mfikirie muandike sawasawa mtume maoni.

**Paul Muthama Kimomo:** Hata nyinyi mfikirie haya maneno ni wazi, inakuwa saa nyingine ya Chief, saa nyingine itapeleka mtu kwa DO, saa ingine tutampeleka kwa Chief. Sasa makosa iko wapi? Akishinda sisi huko, tunapeleka kwa Chief, ukitoka kwa Chief, unakwenda kwa DO, akitoka kwa DO, sisi tunapeleka kortini mpaka anahukumiwa asikie.

**Com. Maranga:** Asante Mzee Kimomo, sasa nakuomba uende ueke sahihi. Asante kwa maoni yako.

**Paul Muthama Kimomo:** Asante na nyinyi.



**Com. Maranga:** Sasa kuna Mzee mwingine mmoja ambaye nataka kumpa nafasi. Na tafadhali nawaambia sisi, tunataka tu kumaliza maliza ili tuone.....wacha huyo Mzee akuje aketi hapa. Mimi nakuona wewe mzee, nitakupa nafasi na useme kwa ufupi kabisa. Na uanze kwa majina yako.

**Wilson Kibayi Masuki:** Majina yangu ni Wilson Kibayi Masuki.

**Com. Maranga:** Sema maoni yako.

**Wilson Kibayi Masuki:** Mimi maoni yangu ni kama vile huyu mzee amekuwa anaongea hapa Mr. Kimomo. Habari ya bursaries.

**Com. Maranga:** Habari ya bursaries.

**Wilson Kibayi Masuki:** Serikali yetu tukufu inajaribu sana kusaidia wale watoto ambao wazazi wao hawajiwezi. Lakini ikija katika mashule, mimi maoni yangu nilikuwa nasema ile board inakalia hiyo bursary, igawanywe. Afadhali iwachie ma headmaster ama Serikali itafute njia ya hiyo pesa ifikie huyo mtoto ambaye hajiwezi. Sababu hii bursary, hii board inaikalia, pengine wanapatia watoto wao na yule mtoto anastahili bursary, hawezi kupatiwa.

Ya pili, mimi nataka kuongea habari ya mashamba yetu. Tulipopata uhuru, haja yetu ni kuchukua yale mashamba ilikuwa inakaliwa na wageni, lakini sasa, tunaomba ile Katiba ambayo mtatengeneza, Serikali tukufu itatengeneza, iangalie wale watu tunaweka kawa mashamba yetu, wakikula hiyo mali yote, tunawaacha tu. Hawawezi kupelekwa kortini. Akipelekwa kortini, anachukua zile pesa ambazo zingefikia mwenyewe, anahongana huku sijui kwa Judge, sijui anahongana wapi, halafu anawachiliwa free. Hapo ndio nilikuwa nataka Katiba ambayo mtalete, muangalie mtu wa kuua watu milioni moja na ni mtu mmoja, atafanywa nini. Hiyo ndio ilikuwa maneno yangu.

**Com. Maranga:** Thank you very much. Asante sana. Nakuomba uweke sahihi kitabu chetu rasmi na eti umefika mbele ya Tume ya kurekebisha Katiba. Asante. Huyo Mzee mwingine. Maoni mafupi kabisa na unaona saa ndio hiyo imeenda kabisa. Anza na majina yako.

**Patrick Matolo:** Mimi jina langu ni Patrick Matolo Mwariri: Maoni yangu ni katika Rais. Raiskama anachaguliwa, anakaa kwa kipindi cha miaka tano. Akimaliza miaka mitano, aondoke, aingie mwingine.

Ya pili, ni machifu. Machifu badala ya kuchaguliwa na Serikali, wachaguliwe na wananchi. Ile nyingine ya tatu ni elimu. Elimu ya Primary iwe ya bure. Ile nyingine ya nne ni katika ardhi yetu. Siku ile tulinyakua uhuru, kuna watu walichukua mashamba makubwa. Ikiwa ni mtu mmoja, anachukua shamba kubwa. Kama ekari elfu ishirini na tano. Na maoni yangu, hiyo ekari elfu

ishirini na tano, atoe elfu kumi igawiwe wale maskini. Kuna watu ambao hawana kitu. Hayo ndio maoni yangu.

**Com. Maranga:** Asante Mzee Matolo Mwariri. Asante kwa maoni yako, na mimi nakuomba uchukue hiyo memorandum, uende ukajiandikishe huko na utuachie. Asante. Ni nani mwingine alikuwa anataka kuongea. Kuja mzee wangu. Dakika tatu hivi, utoe maoni yako. Ufuatwe na yule, halafu nampa Chairman amalizie.

**John Mumo Mulwa:** Asante Bwana Chairman. Maoni yangu nilikuwa nataka kutoa.

**Com. Maranga:** Anza na majina yako.

**John Mumo Mulwa:** Mimi naitwa John Mumo Mulwa. Mimi nilikuwa nataka kuzungumza maneno ya mbayi yaani clans. Ningeuliza, sijui kama ni kuuliza ama ni kusema. Ningesema mambo ya mbayi namna hii. Kama hii Katiba ambayo inatengenezwa, au tunaambiwa tutoe maoni yetu. Tungeuliza kama mambo ya mbayi, watu wa mbayi wakubaliwe. Ikiwa ni nyumba ya ile familia ya hiyo mbayi, ikiwa kuna matatizo upande ile au upande huu.

Kwanza mbayi ikubaliwe, izungumzwe kutokea grassroot mpaka kiwango cha division. Na mbayi kuna mahali pengine inaonekana inafanyiwa makosa. Sasa kama kwa mfano, mimi nina pesa, na yule mwingine hana pesa. Na nikiwa kama mimi napeleka maneno kwa mbayi, yule mtu ako na pesa au ana kesi na ndugu yake au familia yake, yeye kama watu ambao wanakuja kwake, au wanaandikia yeye barua waje huko kwake, huyo jamaa anakwenda kortini, anaenda anashtaki yule chairman wa mbayi. Halafu unapelekwa kortini. Kama ingewezekana, watu wa mbayi wakubaliwe waanzie kutoka mashinani mpaka division. Na ikikosea hapo, ipelekwe kortini. Wawe ni watu ambao wanafuata utaratibu sawasawa, kutoka nyumbani, location, mpaka division. Iwe ikifanyika namna hiyo. Ile ingine ya pili, ni ile ya ma Assistant Chiefs. Ma Assistant Chiefs kama inawezekana tukubaliwe tuwe tukichagua watu kama Wabunge na Councillors. Kwa sababu tukifanya hivi, tunafikiri labda watu watafanya kazi nzuri.

Kitu kingine ni hii society, ambayo sisi kama wazee tunategemea. Mimi nina kahawa na yule mwingine ana kahawa. Lakini inakuwa taabu. Wale watu ambao wamechaguliwa kwa society. Sasa pesa zinakulwa huko zote na hakuna mtu anashtakiwa. Kwa mfano, sasa wale ambao sasa wako kwa viti, wataondoka na iko madeni huko, wanatuachia mzigo mzito huko. Kwa hivyo kama inatengenezwa sheria ambayo mtu akila pesa, watu wa societ, hawa wa committee, washtakiwe ingekuwa bora. Hayo tu ndio nilikuwa nataka kutoa kama maoni yangu.

**Com. Maranga:** Asante Mzee John Mumo. Thank you very much. Nakuomba uweke sahihi kitabu chetu rasmi. Yule mwingine. Kuja mwenye sweater. Baadaye utafuatwa na Chairman, halafu nitawaomba kabisa tufunge kwa sababu hata sisi tumekaa hapa muda mrefu. Unless kuna mtu mmoja kabisa anataka kuzungumza lolote. Haya, majina na kwa ufupi kabisa.

**Richard Kyalo Ndunda:** Richard Kyalo Ndunda. Yangu nilikuwa nataka kusema kuhusu wale wafanya kazi wa Kenya Army (Armed Forces). Wakati hakuna vita, hizo equipment ambazo huwa kwa hiyo Army, zitumiwe kwa watu. Kuchimba dams badala ya kukaa huko bure. Ya pili ni kuhusu Land Act. Wale watu ambao wana mashamba makubwa makubwa, Serikali ijayo, wawe wanalipa kodi nyingi na kama si hivyo, mashamba yagawiwe watu ambao hawana mashamba. Kwa sababu mashamba mengine unapata mtu ana shamba kubwa. Inatoka hapa Maili kumi na hakuna kitu inaendelea. Kama hakuna taxation zipewe watu.

Ya tatu, ni ya mbayi, hizi clans za Wakamba. Nataka kuongea juu ya zile punishments wanapea watu. Ni vizuri kupeana punishment lakini kuna zingine zinavunja haki za binadamu. Wanaweka mtu kwa gunia na anatupwa pale anakaa kama mbwa. Sasa hizo tunasema...they should be punished but let that punishment be moderate.

Ile ingine.

**Com. Maranga:** Wanafanya hivyo?

**John Mumo Mulwa:** Wanaweka kwa gunia, kwa (inaudible) ile magadi bag.

Ya mwisho kabisa, ni uchaguzi wa Ma Councillors, tunataka Katiba inayokuja, iwe Ma Councillors wale wanataka viti wawe wamesoma kidogo. Wawe wamefika form two ama form four. Lakini sio mtu ambaye hajaenda shule. Asante sana.

**Com. Maranga:** Thank you very much Richard Kyalo Ndunda. Thank you very much. You go and register with us there. Sasa wacha nimuulize. Kuna mtu mwingine tumeacha nje kabisa yule ambaye anasema kuna kitu angesema hata kama ni akina mama? Kuna mtu yeyote? Hajasema neno moja, hakuna. Sasa mimi namuita Chairman wa County. Mzee wewe nimekuita zamani ukasema huna maneno. Kuja useme hiyo kitu moja halafu nitaita Chairman kwa sababu ndiyo atatimalizia. Haya, useme jina lako. Nimekupa dakika moja. Kwa sababu nilikupa wakati wako, ukakataa.

**Francis Wambua:** Jina langu ni Francis Wambua. Jambo langu la kwanza ni kuwaambia Commissioner, kabla ya kuchagua mawaziri, wachague mawaziri ambao wanalingana na kazi yao. Kama ni Mwalimu, alikuwa Mwalimu, awe Mwalimu. Si kumchukua mtu ambaye hakusoma awe Minister wa Education. Hiyo ni moja.

Ile nyingine ni natural resources. Iwe mikononi mwa County Council kwa sababu ndio wako karibu na sehemu zinazoangaliwa. Si Governmentiwe huko na hawawezi kutoa kitu. Kwa hivyo Local Government, County Council ikiwa karibu, iangalie. Basi.

**Com. Maranga:** Asante sana Mzee wangu.

**Francis Wambua:** Iko ingine huko niliandika.

**Com. Maranga:** Hiyo ni ya mwisho?

**Francis Wambua:** Hiyo ndiyo ya mwisho.

**Com. Maranga:** Asante sana Mzee wangu. Nenda uweke sahihi kitabu chetu rasmi. Thank you very much kwa kuongea. That's okey. Sasa Chairman wa County Council, wewe ndio utatufungia leo na uwe kwa ufupi kabisa. Unajua tumekaa hapa kwa muda mrefu.

**Francis Wambua:** Yes. Basi ni shukrani sana kwa nyinyi Ma-Commissioners.

**Com. Maranga:** Start with your full names again.

**Nicholas Musili Kyengo:** Majina yangu naitwa Nicholas Musili Kyengo, chairman Kangundo County Council. Mengi ya yale ambayo ningesema yamesemwa lakini niko na haya ambayo imebakia. Kama President wa nchi awe na running mate. Wakati wa uchaguzi, pawe na President, na Vice wake. Na wakishinda waende kwa kipindi cha kwanza na pia kipindi cha pili. President awe anaweza kuenda kwa vipindi viwili. Kisha astaafu.

Katika muundo wa Serikali, ningependelea tuwe na Prime Minister. Prime Minister pia awe ndio Commander-in-Chief of the Armed Forces. Na Prime Minister awe anachaguliwa na Wabunge. Ndio awe na Wabunge kwa sababu ndio wanaweza kujua ni mtu gani, asiwe Prime Minister ni mtu wa watu, ama ni mtu wa mtu. Awe independent, mtu ambaye anaweza kutoa mawaidha bila uoga. Pia ningependelea hii mambo ya mbayi. Hiyo ni kitu ya zamani, hata Serikali kabla ya kuingia hapa mkoloni, kulikuwa na mambo ya clan. Ilikuwa inahudumia wananchi na hiyo ni kitu ambacho kinatakikana kiwe cha maana sana. Na sana sana ile kithitu kiapo. Saa zingine inakuwa ngumu sana, ikiwa mtu aliibiwa na anataka kuangalia mali yake kwa hiyo kithitu, inakuwa shida kwa administration kupewa barua. Ndio wafuate mali yake, kwa sababu hiyo ndio uamuzi wa Mkamba ikiwa amefanyiwa madhara.

Saa zingine kuna kazi za muhimu sana, kama zile zinafanywa na Judges, Controller and Auditor General. Hawa watu wanafanyiwa appointment na President. Na kama vile wengine wamesema, tungependelea hao, hizi kazi ambazo ni za muhimu, zifanyiwe elections by Parliament. Bunge iangalie ni nani anatosha kuwa Judge, ni nani anatosha kuwa Controller and Auditor General. Ni nani anaweza kuwa Attorney General na kadhalika. Zile kazi za muhimu, na hata pia Public Service Commission. Watu wa Public Service Commission, waangaliwe na Parliament. Ikiwa Mbunge ama Councillor, tumechagua Councillor ama Mbunge na ameenda, na hatumuoni, ingefaa tuwe na ile referendum yaani pawe na Commission, ije iangalie kwa hiyo

constituency ama ward kwa sababu watu wamelalamika, wachukue maoni ya watu, na ikiwa huyu mtu ameshindwa na kuhudumia watu kazi au Bunge ama Councillor, aondolewe, watu waweze kuchaguana tena.

Ile nyingine ni mambo ya Local Authorities. Inaonekana Central Government imekaa sana huko juu na ikiwa ni pesa wanapeana huko juu na hawajui ni kitu gani kinaendelea hapa chini. Ingefaa Central Government, itume pesa chini kwa mwananchi ndio mwananchi awe anaweza kujua ni kazi gani ambayo inaweza kuendelea. Kwa mfano hii mambo ya latiffs\*. Hii pesa ambayo Serikali inatuma kwa Local Authority, Local Authority ndio wako karibu sana na mwananchi, ndio wanaweza kujua ni barabara gani ambayo ni mbaya. Ni shule gani ambayo iko na shida na hivyo wanaweza kuhudumia haraka kulika Central Government kwa hivyo wateremshe finance kutoka Central Government ifikie mwananchi wa kawaida.

Ikiwa ni hivyo, basi Provincial Administration wawe ndio watchdogs. Wawe wanaangalia Local Authorities wanafanya kazi gani. Nilisahau kusema ya kwamba President asiwe na constituency. Kwa sababu atahudumia watu wote wa Kenya, hata kikani kuwa na constituency awe anahudumia Kenya nzima. Council ziwe na uhuru, zisije zikawa under control of Minister of Local Government na hata saa zingine ana-dissolve councils bila hata kuwa na jawabu ambayo inatosha. Ikiwa nimesimama na tikiti ya Kanu kutafuta kiti, halafu nikianguka mlolongo. Sistahili kwenda kusimama na tikiti ya DP, nitafute pia kiti. Yaani ikiwa nimesimama na hicho kiti, na nimeanguka, basi maneno yangu iishie hapo.

Natural resources: Mambo ya misitu na kadhalika. Hizo misitu ama forests ndio kitu ambayo ni ya muhimu sana kutuletea mvua na inaonekana misitu imeharibiwa sana. Tungependa kuwe na special permit. Ikiwa mtu anataka kukata mti, afadhali apewe barua ama ruhusa. Kwa sababu inaonekana tukiendelea hivyo tutamaliza misitu yetu na tutakuwa na shida ya mvua. Kuwe na ...ikiwa atapitia kwa Local Authority, apewe idhini ya kukata miti. Kwa sababu wengine wanakataa ovyo ovyo. Hata forest ya council, hata forest ya Serikali inaharibiwa kabisa, inakuwa hakuna (inaudible) wa mvua. Na pia pesa ya natural resources, ikiwa ni kama ya misitu, ni kama ya wildlife. Hizo pesa ziwe zinarudia hiyo Local Authority ndio mwananchi awe anaweza kusaidika kwa njia moja au nyingine.

Ningependelea State iwe ndio iko na jukumu ya mwisho ya ardhi. Lakini Local Authority iwe inaweza ku-control development. Iwe inaweza ku-control ni kitu gani ambacho kinaweza kujengwa hapa. Kwa sababu tukiachilia hivyo, hata mabarabara na nini. Majengo itakuwa imejengwa ovyo ovyo na hatutakuwa na nafasi nzuri za kuishi. Nafikiria ni hayo kwa sababu mengine yamesemwa. Lakini ile ingine ya mwisho kabisa ni mambo ya agriculture. Kenya is primarily agricultural lent, na tunaona Serikali yetu haija-exploit kabisa ukulima. Na sana sana tuko na mito, tuko na Lakes kama L. Victoria na hiyo maji inafaidi watu wengine kama huko Egypt. Ni kwa nini Kenya isije ikaweke mkazo sana mambo ya irrigation katika Kenya? Ndio tuweze kufaidika na hata tunaweza kuuza bidhaa nchi zingine.

Kwa hayo, ningependa kusema ya kwamba tumefurahia, na tumeona utulivu wenu, vile mmehudumia watu wa Kangundo. Hiyo ni shukrani kubwa na tunafikiria mmetosheka na yale ambayo tumepea nyinyi na kama vile tuliulizwa hapo zamani,

tungependelea, hii isiwe ndio mwisho. Watu bado hawajapata elimu ya kutosha. Tuendeleo na kuelimisha watu wenu ndio waweze kujua Katiba ni nini? Na inatakikana tufanye nini ndio watu wetu wasaidike. Kwa hayo machache asanteni sana.

**Com. Maranga:** Basi. Ngoja kidogo, inaonekana kuna swali.

**Com. Kangu :** BwanaChairman. Ukisema tuwe na Rais na tena Prime Minister na sisi wewe wa kwanza. Kuna wengi wamezungumzia mambo ya Prime Minister, hata wengine wakasema President awe ceremonial naye Prime Minister ndiye atakuwa na nguvu za Serikali. Sasa swali langu ni kwamba, ikiwa President ceremonial, mnataka achaguliwe na watu through elections. Naye yule ako na nguvu za Serikali, Prime Minister, achaguliwe na Wabunge.

How do we rationalize? Ikiwa yule mwenye ako na nguvu za Serikali, hachaguliwi na watu directly, lakini yule mwenye hana nguvu ndiye anachaguliwa directly. La pili, umesema President akienda kura awe na running mate na tena wengi wamesema Vice President achaguliwe na watu directly. Swali langu ni kwamba, nikienda kwa kura na mimi niwe ninatafuta URaisna nimechagua wewe as my running mate, napigiwa kura, wewe unapigiwa kura. Nishinde, wewe ushinde, iwe kwa mtu mwingine ndiye ameshinda. Nitachukua huyo kama Makamu wangu ama nitafanya nini?

Sheria iko namna hiyo na hii sheria ndio mnataka mubadilishe. Kwa hivyo kama mnataka maisha ibadilike lazima mubadilishe nini? sheria. Na kama tunauliza nyinyi kujeni mubadilishe sheria na hamko sasa nani atabadilisha hiyo sheria? Kunaye mtu? Kwa hivyo hii maneno hata kama kuna mtu amefungiwa nje ukisikia kuna watu wanakaa upande wa Embakasi kimbia huko na utoe maoni yako kwa sababu hiyo ndio njia tutatumia hili tuweze kubadilisha nini, Katiba na Katiba mumesikia ndio sheria kuu ya nchi. Ukiona ile sheria ya Koran, sheria ya bibilia ambao ni ya mwenyezi Mungu, ile sheria nyingine kubwa sana ni nini Katiba. Tunaelewana?

Wakati munaona yule waziri anatembea na bendera hapa ile sheria inampa hiyo awe na bendera ni Katiba. Kama unaona mtu anatoa amri hapa na pale anatumia nini? Katiba. Hata nyinyi hamuwezi mkaona hii sheria kubwa sana kwa sababu hata mtu alitoka mahali alitoka kama mimi hamjui nimetoka wapi. Lakini kwa sababu iko sheria mnakaa hapa mbele mnanisikiza, ni kwa sababu iko sheria. Si ni hivyo? Mimi sio kijana wenu hapa, si mumeniona mara ya kwanza? Lakini sasa mnakaa kimia kama maji baridi nikisema kaa kimya mnakaa kimya, si ndio? Kwa hivyo hii Katiba ni namna hiyo. mkisema mtakula vizuri, mtakula vizuri, watoto wasome bure, watasoma bure tupate matibabu ya bure lakini msemi nini, njia ya kikatiba, tunaelewana. Basi Asanteni na tunaomba chairman utufungie kwa maombi.





# WOMEN'S SESSION

**Com. Phoebe Asiyo:** Now we can start. Sasa tutafanya hivi. Ebu tunyamaze tusikilizane tumeaanda mkutano huu wa Katiba, naona kuna viti vinakunja itakua vizuri kwa wale wanaosimama, wapate nafasi ya kukukaa hapa, wale wamekaa kwa meza make tu hakuna shida, na wale ambao bado wamesimama karibu mtapata viti mkae chini. Naona mko wengi sana ni vizuri mkae ndio msikilize vizuri. Mlete vitu hapa mbele hapa mbele, kuna nafasi, lete viti hapa mbele. Mpango wetu leo, itakua hivi mtu akisha ongea hapa, ataenda kule andike jina lake na aweke kwa register kwa maana ni muhimu sana sisi kukaa na majina yenu kwa register ndio tujue nani aliyeongea. Mchukue viti pale. Iko viti pale. Hapa mbele kuna nafasi, kila mtu aje na kiti yake akae nayo hapo. Mama kaa hapo, namuwambie tumetosha viti sasa.

**Com. Pastor Ayonga:** Funga mlango.

**Com. Phoebe Asiyo:** Sasa funga mlango tunaanza mazungumzo yetu. Funga huo mlango mama. Tulikua tumeomba Mungu, tumeongea pamoja kwa ule mkutano mkubwa, nyinyi mmetuuliza tuakae peke yetu kama kina mama, mtueleze vile mnataka Katiba mpya itengenezwe. Ningependa kuwajulisha kwamba sio lazima muongee mambo ya kijamii peke yake. Mtuambie, je mngependa Serikali ijayo iwe namna gani. Mambo ya shamba mtueleze. Mambo ya watoto, mambo ya kina mama kwa uongozi. Mambo ambayo inahusu kina mama sana na jamii mzima. Na jambo lolote lile ambalo litakua la muhimu kubadilisha Katiba, kwa maana ni kama Kenya inajenga nyumba mpya sasa. Na nashukuru kina mama wako wengi, kwa maana ili mtu aningie kwa nyumba mpya kwa Kiafrika mpaka mwanamke awe hapo na atengeneze hiyo nyumba. Naomba mko tayari kutusaidia kutengeneza hiyo nyumba mpya ya Kenya. Iwe nyumba safi na iwe nyumba iliyo na heshima na iwe nyumba nzuri. Tunaweza kuanza, sasa yule ambaye yuko tayari aweke mkono wake juu. Tutanza na wewe, halafu wewe, halafu Vice Chairman na yule nyuma na huyo hapo. Ukinja hapa unasema jina lako, hata kama tumekujua kwa maana hii mashima mpaka ishike jina lako. Tukirudi Nairobi hii mashini ndio itatufanya tujue ni nani huyo sasa anaongea. Ndio tuandike mambo sawa sawa. Haya yule wa kwanza aje. Kama umeandika vile huyu msichana ameandika yake, hatasoma hata kidogo, kwa maana tuko wengi na wengine wanatoka sokoni. Naona tuko hapa wanawake karibu mia moja. Si ndio? Kwa hivyo tutaongea dakika tano tano kila mtu isipite hapo, ndio kila mmoja apate nafasi maana kila mmoja wenu ana hekima yake anajambo linamsumbua kwa roho, anataka kuona kwa Katiba. Tumpatie kila mwanamke nafasi ya kuongea. Asante. Hebu mama anza. Tutaweka hapo tu. Wewe utaongea ikiwa hapo.

**Awa Katile Velenzi:** Kwa jina naitwa Awa Katile Velenzi, na ningependa kusema kuhusu uchaguzi ule ambao kwamba utakuja. Tunaomba uwe wa kama vyama vitatu hivi, visiwe vyama vingi na President akae miaka kama kumi halafu ndio ambadilishwe na akitoka apewe security. Ile inengine nitazungumza nitazungumza mambo ya korti. Wanawake wanashida sana wale maBwanazao wamekufa. Na wakija kupata kama ni pension ya Bwanazao, kama wakienda Nairobi wakipata hawapewi, mtu anaweza kukaa kama miaka hata nane, ama kumi anaangaishwa anapelekwa hivi, anapelekwa hivi. Kwa hivyo korti ijaribiwe irekebishe hiyo kitu. Mambo ile inengine ningependa kusema, Makadhi wa Kiislamu, wapewe mamlaka zaidi kama vile judge wako na mamlaka. Ni hayo tu.

**Com. Phoebe Asiyo:** Tumeshukuru sana, kwanza utaenda kule nje uone umeandika jina lako vile ulivyotwambia hapa kwa ile register, ndio tutasikia sauti yako tukifika Nairobi. Asante sana mama Awa, kwa maoni hayo mazuri. Hii kiti tutaiacha hapa ndio kila mtu akija anakalia. Hebu tueleze majina yako.

**Rebecca Thiaka:** Mrs Rebecca Thiaka, Ningelipenda kuongea juu ya uchaguzi. Wanawake sana sana huku kwetu Afrika ni kama warudishwa chini sana, na tungependa wanawake wakati wa elections, wapewe security na wakubaliwe na wanaume na watu wale wengine wote. Kwa sababu, ni kama mwanamke akisimama ni kama anarudishwa chini. Kwa hivyo tungelipenda wanawake wapewe security na wapewe nafasi ya kuji-express, na kusikue na kutukanana kwenye elections. Kwa hivyo wale watu wanatukanana wachukuliwe sheria ndio wanawake wawe na strength also in candidature.

Ile ingine ningeonea ni kwamba, tulionelea mwanamke akiolewa asikae zaidi ya miezi tano bila kuolewa customarily, kwa subabu miezi tano ikiisha mapenzi inaanza ku-fade, kwa hivyo within this five months aolewe customarily. Naye mwanaume yeyote mwenye atachukua msichana wako na akae naye kwa nyumba yake, hata kama ni wiki mmoja. Amuo, ama huyu msichana akipata mimba achukue responsibility juu ya huyo mtoto. Kwa sababu hauwezi kuletewa shida, na huyo mwanaume anakuletea shida na amamuoa hata kama ni wiki moja tena aende free, na msichana wako ateseke wewe urudi kua na shida. Kwa hivyo tumeonelea ni mzuri huyo msichana aolewe.

Na kwa customary yetu ya Kikamba, mtoto ni wa mwanamke. Hiyo tena tumeonelea si vizuri, mtoto ni wa mwanaume. Kwa hivyo kila mwanaume hata ukifugua bibi yako lea hao watoto, uwasomeshe na uwapee kila kitu. Kupigwa, wanawake sana tumepigwa sana. Sijui kama ni huku kwetu Ukambani. Tena tunataka Serikali ipee wanawake security, kwa sababu wamepigwa, na wapewe mahali pa kwenda kushitaki kama Fida ni mbali sana na hapa kwetu Kangundo. Saa zingine hatuna tikiti ya kwenda huko kwa hivyo tuletewe karibu. Ndio kama unashida uende kusema.

Tumeona tena wanawake waingizwe sana wengi, managerial areas, Assistant Ministers, even Attorney General, kwa sababu hata wanawake tunataka hata sisi tuinuliwe. Tungetaka hata kua President. Tungelitaka hata kua Vice President. Ma-chiefs, kwa hivyo Serikali iangalie sana kwa sababu tunaonelea ni kama we are discriminated or side lined in some ways. Am not criticizing lakini tumeonelea the other time, kulikua na election, and it was only one woman who was chosen. Kwa hivyo tungelitaka wanawake wakue wengi. Even in the political parties. We would to equality, kwa sababu wanaume wakiwa wengi, kama ni hao three quarters, ama more than three quarters na wanawake ni wachache. Then it means tutakuka na shida. Kwa hivyo equality would be very good.

**Com. Phoebe Asiyu:** Mimi, ninaswali nataka kukuuliza. Sijui kama unafahamu kwamba majira wetu hapa Africa, kama, Ethiopia, Tanzania, Uganda, kila mahali, wanakitu waita affirmative action kwa wanawanke na wanafanya hivyo. Kabla ya uchaguzi mkuu wanawake wanakua na uchaguzi wao. Kila district inachagua mwanamke mmoja. Vile wanafanya, Political Party yote wana-nominate mwanamke mmoja. Kusimama kwa hiyo district, kama hapa Machokos. Halafu sasa hao wanawake watapigiwa kura na watu wote wale wenye kura. Yule amechaguliwa ataenda bunge kuwakilisha district hiyo kwa hao wanawake. Na hii imefanyika Uganda ikawa na wanawake arubaini na tano kwa bunge, kwa maana wako na district arubaini na tano. Tanzania imefanya hivyo hivyo. Sasa Afrika hata kama ni mbali kidogo lakini mwenendo yao ni kwamba, lazima kuwe na wanawake kama nusu ya vile wanaume walivyo kwa bunge na kwa mambo mengine. Na tumeona mwongozo kwa nchi hizo zimekua barabara. Huja sema kama unataka tufanye namna gani hili wanawake waingie kwa mambo ya uongozi kutoka kwa Local Authority hata mambo ya mashule, mambo ya provincial administration, Serikali kuu, utuambie ni njia gani tutaandika Katiba ili mtu asije akaaribu. Maana Katiba ni sheria kubwa kushinda sheria hii ndogo ndogo. Na kitu tunaandika ni lazima itatunzwa na wataheshimu. Uniambie ni njia gani wanawake wanaweza kufika kwa kiwango hicho cha kuchaguliwa kwa vile wanafanya kwa hizo nchi zingine jirani zetu.

**Rebecca:** Ningelipenda ya Uganda, lakini unajua watu wana different opinions. Yangu ningelipenda kuwe na mwakilishi wa wanawake. Kama provincial level, ama district level. At least kila district iwe na mwanamke representing that district.

**Com. Pastor Ayonga:** Mama Rebecca, nina maswali mawili kwako. Moja, unasema wanawake wanapigwa sana, hebu twambie tutafanya nini na hao wanawake wanao piga wanaume. Kwa maana inaonekana wewe unafikiri tu ni wanaume wanao piga wanawake. Kuna sehemu nyingi sana, wanaume wanapigwa. Na mwanaume anaona aibu kusema jana nimepigwa usiku. Kwa maana anajua watu wakijua itakua mbaya zaidi. Mbona usingefikiria kwamba wanawake wasipige wanaume na wanaume wasipige wanawake. Kwamba sisi zote to treat each other like human beings.

Rebecca: Hiyo ndio sababu nilisema zile laws zetu za custom zirudiwe na ziangaliwe vizuri, kwa sababu customarily there was discipline and there was respect. Haungepata mwanamke anapigwa na mwanaume na mwanaume anapigwa na mwanamke. Kwa hivyo ndio tunataka kabisa hizo customary laws zetu muangalie kabisa na wanawake wasipige na wanaume na wanaume wasipige wanawake.

**Com. Phoebe Asiyu:** Nina kitu kimoja inasumbua ya mwisho. Umesema kwamba mtu akikaa miezi mitano hiyo marriage itengenezwe. Lakini pia ungeweze kutwambia hivi, kwamba customary marriage ndio watu wengi sana hapa Ukambani na Kenya nzima wanaolewa. Watu wachache sana wanaenda kwa makanisa. Wengi wanaolewa kwa njia ya Kienyeji. Nje ungependekeza kua hii marriage iwe registered sawa sawa na ile ya kanisa, kwa maana ni marriage.

Rebecca: Inakuanga registered. Ya Kamba customary kuna mahali mnaandika. Kama hao watu wameoana.

**Com. Phoebe Asiyu:** Lakini hiyo si ya Katiba. Tunataka utwambie ya Katiba iseme kila mtu akioa msichana inaandikiwa ki Katiba.

**Rebecca:** Iandikwe, ndio wanawake wawache kusumbuliwa, ama mwanamke asisimbue mwanaume. Na vice versa.

**Com. Pastor Ayonga:** Swali lingine. Umesema unataka kuona wanawake wengi wako katika viwango mbali mbali, na kwamba election inapofanywa iwe fair na kwamba kungekua representation kama ile ambayo muheshimiwa amesema ya mwanamke mmoja toka from every district. Sijui kama mama mnajua nyinyi ni wengi kuliko wanaume hapa kenya. Na kama nyinyi ni wengi sana unajua one person one vote. Mnajua nyinyi ni 52% ya population ya kenya, bona nyinyi hamjiweki pamoja na kuona kwamba huyu mama ndiye tutapeleka. Bona ikifika wakati wa vote tena nyinyi wenyewe mnapigana halafu hamna vote, na sasa mnataka viti vitengwe vya kupeana.

**Rebecca:** Ndio ile nilikua ninaongea ninasema wanawake wanashituliwa, ukitaka kupiga kura, kama ni Bwanayako anakwambia utaenda kupigia Fulani, usiende kupigia huyu. Kwa hivyo kama ni mwanamke amesimama, tuseme kama ni ya

mchujo, hiyo tumekataa hiyo ya kusimama line, kwa sababu kama ulikula kitu ya mtu lazima line yake. Hiyo tumekataa kabisa.

Kwa sababu akitaka kukupatia akupatie, lakini si lazima umpigie ile kitu tunasema. Wanawake wapewe managerial areas na hata Assistant Ministers wako wangapi wanawake? Ama Minister.

**Com. Pastor Ayonga:** Minister tulikua na Mkamba mmoja.

**Rebecca:** Tulikua lakini hatuna. Kwa hivyo unaona bado hakuna mtu anatumajali.

**Com. Pastor Ayonga:** Asante, lakini ukumbuke unapoenda kule kwa debe, Bwanayako hayuko huko na hakuna mtu atakae juu kwamba (interjection)

**Rebecca:** Tunaogopa.

**Com. Pastor Ayonga:** Unaogopa aje na yeye hakuona. Wewe kwenda debe ifanye kazi, ndio maanayake inaitwa secret ballot. Kwa hivyo tunataka wanawake wengi. Na nyinyi mjiheshimu.

**Com. Phoebe Asiyu:** Asante sana Rebecca umeongea vizuri, nimeshukuru, tafadhali ingia pale nauandike jina lako. Hapana nilikua nimesema Vice Chairman, halafu yule wa mwisho. Tueleze majina yako.

**Mary Ndila Muli:** Mimi naitwa Mary Ndila Muli. Maoni yangu ni kuhusu mume na mke. Hao waty ndio chanzo cha kukaa dunia. Kwa sababu wakioana wanazaa watoto. Mwanaume ni lazima awe anaoa bibi bila kukaa na mwanamke ambaye ni kama contract. Wanakaa na miezi kadhaa mwanamke anaenda. Mwanaume anaona mwanamke mwingine analeta nyumbani, na huyu mwanamke ako na watoto. Shida ni kwa wanawake wengi ambao watoto wao wanarandaranda, walikua na mabwana. Walikua wameolewa na watoto wao wakifunguzwa watoto wanaanza kurandaranda mitaani. Sasa Serikali, ama customary iangalie, mtu akioa msichana wa mtu awe kabisa, si kukaa na yeye kama mtu wa kibarua. Awe pamanent kama bibi ya mtu. Kile kingine ni mwanamke akiolewa ajue kama huyo ni Bwanaamtii Bwanana Bwanaampende bibi. Hiyo ndoa itakua na itaishi. Kusema kweli wako wanaume wengine wanaanza kupunguza ile mapenzi yake na bibi yake, anaanza kupunguza na ndio mwanamke anaona ni nini inaanza. Bwanaanaweza kuja akute bibi nyumbani na akute bibi amekasirika. Mimi nauliza wakina mama warekebishe mwenendo. Wakati Bwanaanaingia usimwambie we, rudi mahali umetoka. Umpemeleze kwa sababu wewe ni bibi yake na mapenzi yako, mpembeleze make pamoja.

Na wanaume wasiwe kila wakati wanakuja wakiwa walevi na wanapiga mwanamke. Wanaume wengine wanaingia nyumbani bila sababu na wanaanza kupiga mwanamke. Kwa hivyo tunaonelea wanawake wangaliwe kabisa na maBwanazao. Hatukatai kuolewa, lakini ikiwa ni ya vita ndio inaleta shida. Kile kingine ni juu ya watoto kwa elimu. Iwe elimu ni sawa ya msichana na mwanaume. Na kazi ikiwa ni kuajiriwa kazi hata wanawake waajiriwe kwa sababu ndio wanalea watoto nyumbani wanakaa

na watoto na ndio wachukaji wa nyumba. Bila mwanamke akuna nyumba, kwa sababu nyumba ya mwanaume watu wanaongopa, kwa sababu mahali iko mwanamke watu wanatembelea na wanaenda kuona urafiki ambao uko, kwa sababu hii nyumba iko na mwanamke.

Kile kingine, mwanamume akishika mwanamke kwa nguvu afungwe maisha. Kwa sababu hao ndio wanaleta ile ugonjwa na mimba ambaye si halali, na kushika mwanamuke hiyo maumbile ya binadamu aikuumbwa mwanamke awe anashikwa kwa nguvu. Mwanamke ni wa kuulizwa, kwa sababu hiyo ni gift yake alipewa na Mungu lakini si ya kila mtu barabarani. Wanaume wajue hiyo ni gift Mungu alipatia mwanamke na ndio mahali pazuri ya kuleta watoto duniani.

Kile kingine ni juu ya Serikali. Raisawe anakaa kwa miaka kumi, akiwa President na wakati ambao ata-retire, awe na security mahali anaenda. Kile kingine, kwa bunge, wanawake wawe nominated wengi, kwa sababu wanaume ndio wenye nguvu. Kama vile nilivyosema mwanaume ni kichwa, mwanamke ni shingo na wakati wa siasa wanaume wako na kona kona nyingi za kupata pesa, kushinda wanawake, na mwanamke anaweza shindwa kwa election, kwa hivyo wawe nominated wengi. Kwa sababu sioni ni haja gani mwanaume anakua nominated na yeye aliumbwa maumbile ya Mungu. Yeye hiyo ni chuma stiff, anaweza fanya kila kitu chochote na kwa kusema kweli wanawake wawe nominated, hata ikiwa nominated wanaume wawili wawe wanawake wanne. Ndio nominated.

**Com. Phoebe Asiyu:** Huna swali kwa mama?

**Com. Pastor Ayonga:** La, mimi nampongeza ya kwamba amesema ki bibilia kabisa, bibi amtii Bwanayake na Bwanaampende bibi yake. Na hayo yote mawili yakifanywa hamna viti.

**Com. Phoebe Asiyu:** Ninataka kuuliza swali moja mama. Umeongea habari ya elimu, lakini hukutwambia kama unataka elimu itolewe ya bure kwa watoto?

**Rebecca:** Ndio, itolewe kutoka primary hadi form four.

**Com. Phoebe Asiyu:** Mambo hayo ni ya muhimu sana kutueleza hili tujue vile tutafanya. Tumeshukuru, sasa tupate, Nani yule alikua hajaongea?

**Interjection: Rebecca:** Naweza kurudia kitu kimoja muhimu?

**Com. Phoebe Asiyu:** Ndio.

**Rebecca:** Mambo ya korti. Iko korti inakaa miaka mtu akipeleka kesi kortini. Kama inaweza kua three months, six months,



kesi iwe imekwisha, hiyo ni mzuri na wako mabibi wengi wale maBwanazao walikufa na accident, walikufa na hii na ile kesi ilifanywa, na hizo kesi zote za wanawake mali yao yote inakaa na ma-lawyer, hawajui wanawake watasaidiwa na Serikali namna gani, kwa sababu hiyo ni shida moja, wanawake Bwanaameenda na yuko na haki ya kupewa hiyo mali na hakuna kitu ambaye anapewa. Na uridhi iwe ya mwanamke na mwanaume. Ile land, ikiwa wewe ni Bwanaya mtu na bibi ya mtu na wako na land, na uwe na bibi wawili gawanya hiyo kwa bibi wawili na kila mmoja awe na title deed.

**Com. Pastor Ayonga:** Mama nikuulize, bado unaongea juu ya wanawake wawili, hii uoni ni shida ya kwamba Bwanammoja bibi mmoja?

**Rebecca:** Nasema juu ya wale ambao walifanywa hivyo. Kwa sababu siku hizi hakuna hiyo.

**Com. Phoebe Asiyo:** Lakini ujue hii Katiba tunatengeneza itakaa na sisi miaka hamsini au miaka mia moja. Tunajua kuna dini zingine kama Kiislamu inaruhusu hiyo. Je miaka hamsini ijayo unafikiri wasichana watataka kukaa na mwanaume mmoja kwa nyumba moja?

Rebecca: Hawawezi kaa.

**Com. Phoebe Asiyo:** Kwa hivyo ungependekeza tuseme kwamba tufunge polygamy.

**Rebecca:** Bibi mmoja, Bwanammoja.

**Com. Phoebe Asiyo:** Nikusema tu-abolish polygamy.

**Rebecca:** Yes.

**Com. Phoebe Asiyo:** Nimeshukuru sana umesema hayo. Nenda pale ujiandikishe pale.

**Com. Pastor Ayonga:** Ngoja kidogo, ulikua na maandishi ya kutuachia?

**Rebecca:** Yes.

**Com. Pastor Ayonga:** Hii basi unatuachia.

**Com. Phoebe Asiyo:** Ataweka kwa register pale. Weka pale kwa register. Sasa huyu akimaliza ni wewe utaongea mama yangu. Mpatie nafasi huyu mama aje haraka haraka, kwa maana hakuna nafasi. Kama atachelewa kidogo, basi huyu wa hapa

mbele aanze huyu atakaa kwa hicho kiti chako. Twambie jina lako.

**Muelu Thiaka:** Jina langu naitwa Muelu Thiaka. Sasa mimi nauliza Serikali, kwa wale viwete. Viwete wako na watoto wengi sana. Wengine wanakua na nne, tatu. Na saa ile wanaenda shule nauliza Serikali hao watoto viwete wasomeshe bure, kwa maana wanataka elimu, walinde nyumba ya baba yao au mama yao.

Ile ingine ni pesa ya NSSF, wale walikua bibi Bwanaapofariki na ile pesa ilikua huko. Huyu bibi anaenda kuitisha ile pesa anakaa miaka kumi na ako na watoto shule na Bwanayake amefariki, hiyo pesa imekaa miaka mingi sana na hajui office za huko. Akaenda akarudi, akapotea Nairobi, akatangatanga, akauliza mtu akakula pesa yake. Akawacha kumpeleka uko. Serikali iangalie kama mtu amefariki na pesa za Bwanaiko uko. Huyu mtu alipwe haraka, apatiwe hiyo pesa asomeshe watoto wake. Ile ingine ni hii inaitwa korti, kama land: naanza hiyo kesi ya land, huyu mtu tulikua tunapakana na namna hiyo na anataka hii kicheka yangu na sio yake, na hiyo kesi nimepeleka kortini. Huyu mtu anatoa pesa na mimi sina pesa, nauliza Serikali iangalie hii kitu irudishwe nyumbani.

**Com. Phoebe Asiyu:** Unataka Serikali ifanye namna gani. Unajua hii mambo ya ardhi ni muhimu sana tunataka tuandike Katiba mzuri. Twambie kabisa kabisa maoni yako juu ya ardhi.

Mary: Naona ile kamati ya nyumbani ichague hao. Wangalie hiyo mambo ya vichaka. Ile ingine ya mwisho na sema ya wasichana. Kama ni Bwanayangu ama mtoto wangu alienda akaona kijana ya mtu na yeye ana bibi, akamzalia watoto wawili na akamwacha na hao watoto na akakuja kwangu. Huyu alee hao watoto mpaka waitimu. Kwa maana ameharibu mtoto wangu, na ako na bibi.

**Com. Pastor Ayonga:** Na kama singekua na bibi.

**Mary:** Amuoe, huyu mama atatoa land wapi?

**Com. Phoebe Asiyu:** Asante, tumeshukuru sana mama, utaenda pale uandike kwa register. Asante sana mama Muelu. Sasa Mutave kaa uongee.

**Mutave Ndunda:** Nayu nye ndiu nene Kikamba nundu nye ndisi Kiswali.

**Com. Phoebe Asiyu:** Atatafsiri sena tu. Jina yako halafu uongee polepole mzuri, huyu atafsiri sisi tutaandika maoni yako.

**Mutave:** Nayu nitawa Mutave Ndunda.

**Translator** : Anaitwa Mutave Ndunda.

**Mutave**: Ninena yulu wa kanzu.

**Translator** : Ataongea juu ya local authority.

**Mutave**: Yu naoka vaa ndunu naoa manyanya, kyona naoa ndoo imwe na ndoo isu niyalea uthela. Nikukatia umunthi ilee othela. Nisyoke ingi uniusu ingi nimiamukie ingi nisyoke nete. Yu naete ni kukata.

**Translator** : Anasema akinunua kama ni debe moja ya nyanya, anataka kuuza alete sokoni, siku ya kwanza atalipia hiyo kodi. Akiuza isipokwisha arudishe tena the following day kwa soko, analipishwa tena kodi.

**Mutave**: Na ndoo isu yuma maana eli.

**Com. Phoebe Asiyo**: Angependa tuandike namna gani?

**Translator** : Yu wenda itwike ata?

**Mutave**: Yu nenda itwike yuyu, ithie akina mama nituthinitwe muno ni kanzu.

**Translator** : Sisi akina mama tumesumbuliwa sana na local authority.

**Com. Pastor Ayonga**: Katika hizi nyanya zake angetaka ziwe namna gani?

**Translator** : Wenda ata?

**Mutave**: Yu nikwelesya nesa.

**Com. Phoebe Asiyo**: Hebu nikusaide. Ungependa tusema kwa Katiba kwamba wale masikini ambao hawana pesa nyingi wasikatwe ile kodi ya market. Ungependa kusema hivyo? Hebu sema sasa machini ishike hiyo.

**Mutave**: Yu nasya, ndiua manyanya ndoo imwe. Nienda atilili, Katiba kasyovye ethiwa ni naua ndoo na naona maana eli, kafaida konze kaoswa ni Kanzu kathele. Withiwe ndie kindu ninakwata vo. Yunuka kuta nitethye syana na yu faida woswa ni Kanzu nilie utethya syana.

**Translator :** Wenda ata?

**Com. Ayonga:** Tafadhali mnyamaze hii ni nafasi ya mama.

**Com. Phoebe** Asiyo: Hebu sikia kwanza Council inawafanyi kazi wake na inamuhimu ya kazi ya kusaidia watu wa area yao. Lazima watoe tax. Lakini wewe unasema wewe ni masikini, wanakulipisha ile kodi ambayo wewe hauna. Sasa utwambie unataka namna gani kwa wale masikini?

**Mutave:** Nenda tusyawe ethiwa mundu niwauka na kindu kinini, makasyasya undu matona kwika.

**Translator :** Kama mtu ameleta kitu kidogo sokoni wangalie ile kitu mtu ameleta walipishwe kulingana na bei yake. Wasilipishwe bei kali kwa kitu kidogo.

**Com. Phoebe** Asiyo: Okay na ingine?

**Mutave:** Undu ungi ni huu. Yu kwina ukimwi, na yu kwina ukimwi nitukwiwa tutangaze uvoa wa ukimwi, naye twewa tutangaze syana uvoa wa ukimwi, yu ukimwi usu twa matavya naibwa nyeninoka nakwata ni ukimwi, two ta kivisi, yu kivisi kii kiuka, yu nudu kina kitula kitakinya kingi kyose kikwatwi kikome na noo kikome noo kikome noo. Yu nenda atilili embwa mtu niwathi athimwa sivitali kutavanwe kila uwaite ukethiwa embwa mtu ni wakwa ewe ni kithoi nake awaite ukimwi. Embwa ninathi nathimwa, nathinathimwa nie niwe niwaite kina, kenda ikethiwa kimbwa ni kana nikomana mtu huyu okite awaite kina. Kana embwa musee wakwa ni watiwa nakwa, yu andu nimakwambia kukia musee wakwa nundu niwamanyika akwite ni ukimwi.

**Translator :** Anataka, because watu wanakufa sana na HIV/Aids, anataka kutangazwe yeyote mwenye amepima hosipitali apatikane ako na viruzi vya ukimwi atangazwe fulani fulani ako na hii ugonjwa ndio watu waache kuabukizana ovyo ovyo.

**Mutave:** Yu twina tuosiki twakite kuku musyi. Naye tuosiki tuu twakite kuku musyi, yu nitwosa tukaua twindu tunini tukauma ta point ikumi. Point ikumi ni faida wa silingi umwe umwe na yo kanzu naye nikuka ovo.

**Com. Phoebe** Asiyo: Hiyo tumemaliza, nenda kule nje mama kabisa, uandike jina lako kule nje. Haya sasa mama uje ukae kwa hii kiti utueleze jina lako na kila kitu.

**Teresia Mutua:** Kwa majina naitwa Teresia Mutua.

**Com. Phoebe** Asiyo: Ndio Teresia ongea.

**Teresia:** Nazungumza juu ya maendeleo ya wakina mama. Wakina mama hapo mbeleni walijenga manyumba nyingi, maduka wawe wanapata usaidishi na sasa wakajenga na zingine hazikuisha, sasa mini nauliza kama Serikali inaweka akina mama maanani, kwa sababu kama wakimaliza maduka yao hapo ndio wanapata faida ya kusaidia watoto wao huko nyumbani.

**Com. Phoebe Asiyo:** Nataka upendekeze. Unataka Serikali ifanye namna gani?

**Teresia:** Iwe inafanyia wakina mama harambee na wanatambulika, kwa sababu wakiwa pamoja walikua wanamsimamo moja.

**Com. Phoebe Asiyo:** Nasikia vile unasema. Pengine harambee hatuwezi kuweka kwa Katiba, lakini tunaweza kufanya hivi, kuna nchi zingine kama Bangladesh, na nchi zingine sote za dunia, ambazo ni masikini wanafanya hivi. Wanawake wakiungana pamoja wanapewa loan ambayo haina interest, na kama iko interest inakua interest kidogo. Wanamaliza hiyo manyumba yao, wanapata loan ingine ya kununua vitu sasa kwa hayo maduka au kama ni hoteli, au kama ni canteen au mahali ya kulala halafu hiyo loan wanawake wenyewe wanasimamia hiyo loan na wanarudisha, naimeonekana dunia mzima wanawake wanarudisha loan vizuri kushinda hata wanaume. Pengine ungependekeza mambo ya loan ingekua vizuri zaidi kuandika kwa Katiba kushinda kusema mambo ya Harambee.

**Teresia:** Asante sana hapo, ndio nilikua nataka kutarajia kidogo. Sasa hapo wakipewe hiyo loan, bila interest itakua vizuri. Wawe wanaenda wanafanya kazi kwa hiyo maduka zao.

**Com. Pastor Ayonga:** Alisema si loan bila interest, inaweza kua tu kidogo kuliko ile ya kawaida na mnapewa kulipa kwa muda.

**Com. Phoebe Asiyo:** Na kitu kizuri kwa hiyo loan. Haina ile wanaita security. Wanawake ndio security na wanarudisha hiyo. Na ndunia mzima wamerudisha vizuri sana hata kushinda wanaume.

**Teresia:** Twaomba watusaidie tu sawa. Pahali pengine nilikua nataka kusema ni juu ya watoto wasichana. Hapo zamani walikua wanapelekwa kwa toara. Natunauliza wawache hiyo manene ya toara kwa wasichana.

**Com. Phoebe Asiyo:** Unataka Serikali iweke sheria kwamba hakutakua na toara kwa wasichana?

**Teresia:** Hiyo itakua mzuri, kwa maana sio vizuri.

**Com. Ayonga:** Lakini nikuuliza mama, ni nani wanao tahirisha hao watoto wasichana?

**Teresia:** Ni wazazi wao.

**Com. Pastor Ayonga:** Mzazi gani?

**Teresia:** Yule alizaa mtoto msichana.

**Com. Pastor Ayonga:** Ndio lakini unajua wazazi ni wawili, lakini mambo ikifika ya hii kutahirisha, ni nani wanaofanya the job?

**Teresia:** Both.

**Com. Pastor Ayonga:** Okay.

**Teresia:** Parent ya mwanamume na mwanamke wanakua na mawasiliano moja.

**Com. Pastor Ayonga:** Lakini ni parent ya mwanamke?

**Teresia:** Both parent.

**Com. Pastor Ayonga:** Both parent, mwanaume anaingia maneno ya msichana toara.

**Com. Phoebe Asiyo:** Nafikiri hapo tunaweza kusema ni heri tu-abolish hiyo mambo vile umesema, lakini kuwe na elimu sana sana kwa wazazi, wajue ubaya na vile wanaumiza watoto wasichana, kwa hayo mambo ya toara. Ni elimu lakini pia lazima kuwe na sheria.

**Teresia:** Ile ingine ni juu ya, tumezaa watoto wasichana na wanaume. Na yako madawa haya ya kulevya. Wanaenda wanaleta hayo madawa ya kulevya watoto wetu wanapewa hayo madawa. Sijui mahali wanapewa, halafu wanaaribika kabisa.

**Com. Phoebe Asiyo:** Hebu pendekeza, tufanye nini juu hii ya mambo ya kulevya?

**Teresia:** Mimi napendekeza Serikali ifanye uchunguzi kali sana hapo, ndio yaishe hayo madawa.

**Com. Phoebe Asiyo:** Halafu nyumba ya uchunguzi?

**Teresia:** Nyuma ya uchunguzi ni kumaliza hayo madawa yaishe kabisa. Hakuna ingine. Asante.

**Com. Phoebe Asiyo:** Tumeshukuru sana tafadhali nenda kule ujiandikishe. Kuna mtu nilikua nimemuuliza ataongea nyuma ya huyu. Okay unaweza kuongea. Halafu nani mwingine yuko tayari kuongea. Haya wewe nyuma ya huyu wewe utakuja halafu huyu. Upande huu sijaangalia lakini nitaangalia.

**Lydia Nduku: Lydia** Nduku, Kwanza mimi nataka kuongea juu ya hao wato ambao hawajiwezi. Hao nataka watengewe special seat katika bunge ili wawe wakitetea wale wengine. Hata kwa Council watengewe hao viti. Katika nomination wanawake naona ni vizuri wawe nominated. MPs na Councillors. Pia nataka kuwe na free education kutoka standard one upto eight. Hata pia katika provincial administration naona Assistant chief ni wengi sana. Naona ni vizuri wapunguzwe na wazee wa vijiji wapunguzwe ni wengi.

**Com. Phoebe Asiyo:** Assistant Chief? Na Chiefs?

**Lydia:** Wakae hivyo hivyo hiyo chain ingine ni mzuri.

**Com. Phoebe Asiyo:** Na ma sub-location yavunjwe?

**Lydia:** Hayatavunjwa lakini yatakuwako, lakini assistant chief ni wengi wasaidiane na hao wazee wa vijiji na wazee wa vijiji washughulikiwe na Serikali hao wazee wa vijiji. Na naona ni vizuri kurudishe ile ya wakamba ile kithitu. Ukinyang'anya mtu kitu iwekwe hiyo kithitu. Na naona ni vizuri hao mayors wachaguliwe na wananchi, wasiwe wakinja huku kwa councils wanachaguliwa na councillors wenzao. Naona ni vizuri mayors ama chairperson wa council achaguliwe directly na wananchi.

**Com. Phoebe Asiyo:** Ingingine?

**Lydia:** President awe commander in chief of the armed forces. Lakini in case of emergency awasiliane na bunge. Na hii councils isiwe under central Governmentiwe independent councils. Na naona ni vizuri kila mwananchi wa Kenya awe na shamba kusiwe kuko na squatters. Kila mwananchi awe na at least shamba lake. Katika hii kungawanywa kwa constituencies. Naona ni kubwa sana igawanywe ziwe mbili. Katika Kangundo tuwe na Kangundo na Matungulu. Kwa hivyo ni kubwa sana. Hata hii wards za councils ni kubwa sana. Councillor mmoja anashikilia sehemu kubwa sana na sioni kama kila mtu atafikiwa na huduma ya huyo councillor. Nimefika hapo mimi.

**Com. Phoebe Asiyo:** Asante sana, tafadhali nenda pale ujiandikishe halafu yule nilikua nimemuuliza atakufata ndio aje sasa. Ni wewe nilikuambia utamfuata? Haya kimbua na kama uko ni mbali kufika karibu mapema na weza kuuliza yule aliye karibu. Kuja mama uanze saa ile huyu akifika.



**Mbeke Makau:** Mimi nataka kuongea kikamba.

**Com. Pastor Ayonga:** Ndio lakini majina?

**Mbeke Makau:** Mbeke Makau.

**Com. Phoebe Asiyo:** Haya endelea.

**Mbeke Makau:** Yu ni nena yulu wa kisomo undu Serikali itona ututethesya. Yu ivinda ya tene. Nyie ndyina na syana kusomethia lakini ni nena yulu wa aa anini. Undu tuna kusatiwa kumanza school fees, undu twamanzaa tene.

**Translator :** Wasya ni kwikwe ata?

**Mbeke Makau:** Yu nasya undu Serikali itona ututethesya yulu wa kawa usu witu ukethia nukuka mbesa undu waukaa tena.

**Translator :** She is saying that they have problem in paying school fees and proposes that the Government should be able to assist small scale farmers.

**Com. Phoebe Asiyo:** Kwa njia gani? Unataka watoto wasomeshe bila malipo na pia mashamba unataka usaidiwe kwa njia gani? Input ya farms au loan au nini?

**Mbeke:** Yii nitwanengawe loan yu twinengawe. Loan itungwe ingi undu twanengawe.

**Translator :** Serikali iwe inaweza kuwapatia loan na kufanya kama kitambo.

**Mbeke:** Yu vethina ungi tu kwenda tutethesye syanani.

**Translator :** Weta undu ukwenda Katiba kandikwe.

**Mbeke:** Tuenda Katiba ethiwa ni vatoneka woni wakwa tutethesye yulu wa ndawa ii sya kulevya.

**Translator :** They have problems with drug abuse.

**Com. Phoebe Asiyo:** Tufanye nini mambo ya drug abuse.

**Mbeke:** Katiba kasye syindu isu ithele vyu na ula ukukwatikana na syo ainengwa discipline ni Serikali undu vatoneka. Ayovywa.

**Translator :** She is proposing for stiff penalty for those who are drug trafficking.

**Com. Phoebe Asiyo:** Tafadhali msiongea tuko na mashini hapa haiwezi kushika sauti ya huyu mama vizuri kama kuna watu wanaongea hapo nyuma.

**Translator :** Wina woni ungi?

**Mbeke:** Aiye.

**Translator :** Amefikisha hapo.

**Com. Phoebe Asiyo:** Stiff penalties for drug peddlers, asante sana umesema vizuri nenda pale nje uandike jina lako kwa register yetu.

**Easher Kalundu:** Kwa jina naitwa Easher Kalondu na ninamesema juu ya pombe na sana sana pombe ya chang'aa. Chang'aa ndio mbaya inaharibu wazee wetu hata watoto wetu, watoto wadogo, watoto wakubwa wale wanaume wote wanaharibu na chang'aa. Sababu mzee yangu hana kazi na anaenda kuingia kwa chang'aa asubuhi na mtoto akamfuata wakakunywa chang'aa, watakuja usiku bila kufanya kazi. Hiyo chang'aa ikapigwa marufuku ndio mzuri sana.

**Com. Phoebe Asiyo:** Okay mama umeseme vizuri tumalize mambo ya chang'aa. Lakini kuna hizi vinywaji vingine ambavyo vinatangazwa kwa radio, kwa TV na pengine ni mbaya kushinda hata chang'aa. Na vina tangazwa. Ungependekeza namna gani kwa jambo hilo.

**Easther:** Hiyo chang'aa si mzuri, na hiyo madawa ya kulevya si mzuri. Na ile inaitwa bhangi. Vitu vyote ya kunywa ni mbaya sana.

**Translator:** Wiwa ni Commissioner ve matangazo matangazawa radioni na TV-ni makwonanya oki sya mithemba sitangazwa. We utona kwasya hata ovoo wa matang'azo asu. Nimaile kwendeiwa?

**Esther:** Maile kwendeiwa ni maseo.

**Translator :** Matangazo ala matangazaa uki iwa ni nzeo ni uki museo wa muthemba muna na ni mbuki ingi nthuku ona kwi

chang'aa. Wikulwa nu kuitikila kana nukwenda Katiba kuleane na matangazo mamuthemba usu.

**Easther:** Yi ona Katiba kaitangaza kana Serikali yiose atua kuveta unywi wa chang'aa. Syonth syindu sya unywa.

**Com. Phoebe Asiyo:** Kwa hivyo, there should be no advertisement of any alcoholic beverages on television or radio.

Easther: Kila kingi, ninena yulu wa wiimi witu. Ithie twima kahawa na kahawa kaitu ni twaikie kwona mbesa. Niasya yulu wa thina tosu nundu musee uu wakwa ukwaiwa nundu ukwika nundu mbesa ni syaie kuu mwiundani. Yu vatoneka muiimi anewe mwanya aiteia kahawa tuteuthi utewa nandu tutesyi. Nundu twisyi katewa kuya kenda utewa nuu.

**Translator :** (Inaudible)

**Com. Phoebe Asiyo:** Okay anaingine?

**Translator :** Wina unduungi?

**Easther:** Ninena ouu.

**Com. Phoebe Asiyo:** Asante sana, nenda huko nje ujiandikishe ndio tujue ulikua na ukaongea na sisi. Wacha huyu mama aje kwanza. Na huyu ndiye alikua aongee kwanza. Wacha aje aongee wewe ukae pale. Halafu akija na wewe utafuata yeye. Jina lako?

**Frakfedith Nzisa Wambua:** Kwa jina naitwa Frakfedith Nzisa Wambua, ningependa kuongea juu ya wasichana wetu ambao wasichana wanakuja unalea wasichana wako vizuri na vijana au watu wazima ambao wamekomaa wanakuja wanadunga wasichana wetu mimba, na ikiwa msichana alikua katika shule hiyo imekatika na kijana anaendelea na kusoma na msichana wako amerudi kwa nyumba. Tungetaka hao wasichana wetu ikiwenzekana huyo kijana alee huyo mtoto kwa miaka kumi na nane. Kutoka kuzaliwa mpaka miaka kumi na nane, na ikiwezekana huyo msichana akiwa hajapata Bwanahuyo kijana ampeleke course ndio ajisimamie.

**Com. Phoebe Asiyo:** Miaka kumi na nane? Na ingine?

**Nzisa:** Na ikiwa msichana hakujaliwa kupata bwana. Huyo kijana aendelea kumpatia course ili huyo mtoto wake ajisimamie. Upane wa hospitali tungependa tuteuliwe committee ambayo inaweza kuangalia masilahi ya wagonjwa. Kwa sababu wangojwa wakienda hospitali wengine wanakufa kwa line, bado kuonekana na daktari na ukiangalia upande, unaona daktari wanatembea tu au wale wasaidishi wako kwa hospitali. Tungependa kama kunaweza kua na committee ambayo inaweza

kusaidia wagonjwa mtu akikosa msaidizi aende kuongea na committee ambayo imeteuliwa kuangalia masilahi ya wagonjwa kwa hosipitali. Tungetaka tena clinic za wenyewe ziwe kidogo kwa sababu hao ndio tunafikiria wanachukua madawa kutoka kwa Governmentkwenda kwa clinic zao. Nimeshukuru na nimesema asante.

**Com. Pastor Ayonga:** Wacha nikuulize swali mama. Umesema msichana alidungwa mimba pengine alikua anasoma na msichana si anafukuzwa? Singelipenda kusema kitu juu ya huyu kijana aliyedunga msichana wako mimba na yeye anawachwa shule. Hiyo maneno unayaona aje. Unaona habari hii ya kwenda kutunza mjukuu, ndio tu ina maana au kijana huyu atadhibishwa yeye namna gani.

**Esther:** Huyu kijana ataadhibishwa kwa sababu atalea huyu mtoto. Kwa miaka kumi na nane.

**Com. Pastor Ayonga:** Na kama bado yuko shule hana pesa ni nani atalea mtoto.

**Esther:** Hapo tunataka iwe wazazi, kwa sababu itakua discipline.

**Com. Pastor Ayonga:** Okay umesema wazazi. Tulikua tunagojea useme hivyo.

**Com. Phoebe Asiyo:** Haya asante sana nenda ujiandikishe. Nani anafuata huyu? Ni wewe nilikuuliza na ukachelewa kuja. Ni huyu halafu wewe sasa, halafu wewe councillor. Kaa, wewe bado umechelewa tu. Tufanye haraka haraka maana kuna watu wengi na ni lazima leo kila mwanamke aongee.

**Monica Mueni:** Kwa jina mimi naitwa Monica Mueni. Na mimi naongea juu ya wanawake kwa sababu ya wale walikua wanalima. Sisi wanawake wengine ni wakulima, na sisi tunalima kahawa na kahawa yetu imeteremshwa chini. Kwa sababu hapo mbeleni tulikua tunalima tukapata pesa kutoka kwa kahawa. Na sasa kutoka siku zimepita hivi, kahawa imeteremshwa chini kabisa. Haikukua na kitu, naukienda huko, majani iko juu, ukienda mahindi juu, ukienda huko marangwe juu na sisi hatupati kitu. Mimi naongea, wakienda huko bungeni wale walienda kufanya kazi huko bungeni, waenda watufanyie pesa tupate mapato kwa kutoka kwa shamba. Wanawake wengi ni wakulima, hatuendi ofisini. Tunaenda kwa shamba, natukienda kwa shamba hatutoi kitu, mahindi tunatoanga kidogo kwa sababu shamba yetu yote tumepanda kahawa. Ama sivyo? Ama hii inakua mbaya?

Kwou mathi kuya mbungeni maende mamathe undu motwika kahawani nundu kahawa witu ni watheie nthi vyu vai kindu tukwataa.

**Com. Pastor Ayonga:** Mama endelea na ile lugha ulikua ukiongea.

**Nzisa:** Niendelea na Kiswahili? Mkienda huko bungeni, muende mkatuangalie mambo ya kahawa. Tunalima kahawa hata mtoto yule anatoka nyuma yetu ukienda kwako umpatie shamba, level nne, unamwambia lima hapo upate mapato kutoka hapa kwa shamba. Na huyu mtu ukimpatia hiyo hakutoa kitu kwa hiyo shamba. Na hatupandi mahindi, shamba yetu yote tumejaza kahawa kabisa. Mimi nakomea hapo.

**Com. Phoebe Asiyo:** Asante sana, tumeshukuru sana nenda uandike. Sasa mama safari hii usiache mtu akae kwa kiti kabla uja ingia. Halafu Councillor atongea.

**Rose Mwanza:** Mimi naitwa **Rose** Mwanza. Ningependa kuongea juu ya mashamba. Ningependa sasa Serikali iweke mashamba iwe na title deed, iwe kama vile marriage certificate inawekwa watu wawili. Bibi na bwana. Sababu sasa, saa ingine unakuta Bwanaanaenda anachukua loan na na ile title deed unakuta sasa mnaambiwa muondoke. Na bibi hana habari. Sasa ningependa mukeke maanani iwe watu wawili. Kama vile certificate ya arusi. Sasa ingine ni habari ya mali ya umma. Sasa nataka Serikali iweke maanani ile watu wanasimamia vitu za watu, tuseme kama wakulima wa kahawa wale watu tunawachagua ama watu wale wanasimamia mali ya watu. Wenye kusimamia na mtu anaaribu awe anapelekwa kortini. Sababu sasa, kama wengine tunawachagua wanaenda wanakula pesa ukiwauliza wanasema, hawajali ni mali ya umma na hakuna mtu atamuuliza. Sasa tunataka wachukue maanani wakiaribu wapelekwe kortini. Ingene ni habari ya wasichana wetu. Wasichana wetu sasa tunataka wachukuliwe, sasa kama mtu anaolewa, mwenye kuoia ama ile boma imeoa msichana ipelekwa mali ya huyu msichana haraka.

**Com. Pastor Ayonga:** Ile ya mbuzi tatu.

**Monica :** Sababu wanakaa, kama msichana anazaa watoto tano, na bahati mbaya msichana afariki, sasa itakua kesi wenye kuolewa wanasema msichana si wetu hatujapeleka ile mbuzi tatu. Sasa, mimi mwenye msichana nasema huyu ako na watoto na simtaki, sasa hiyo inakua kesi na hapo shida inaingia hao watoto wanakosa mahali. Hawawezi kukaa huko, hawawezi kuja kwangu, sasa hiyo ni shida na hiyo shida imeletwa sababu ya kukosa ile mbuzi tatu.

**Com. Phoebe Asiyo:** Kwa hivyo vile tulisema mbele ni kwamba customary marriages lazima ziwe registered, sawa sawa na ile ya kanisa au ile ya DC. Hiyo mbuzi tatu lakini iwe na certificate ya marriage ile ya Serikali.

**Monica :** Hiyo mbuzi tatu ndio sasa certificate yetu.

**Com. Phoebe Asiyo:** Hapana, mbuzi tatu ni lazima ikae hapo lakini Katiba haiwezi kuandika mbuzi tatu ndio certificate, certificate ni lazima itoke kwa hivyo mbuzi tatu zishalipwa.

**Monica :** Iwekwe sasa.

**Com. Phoebe Asiyo:** Iwe registered kama marriage. Kwa maana ni marriage. Si ndio?

**Monica :** Ndio.

**Com. Phoebe Asiyo:** Asante sana mama umeongea vizuri. Sasa councillor. Yes madam councillor give us your name again.

**Catherine Syombua Munyao:** Kwa majina naitwa Catherine Syombua Munyao. Sasa yangu ilikua ya kusema uridhi wa wajane. Sasa ikiwa Bwanana bibi wako hai ni vizuri sana kugawanya shamba. Shamba iwe imegawanywa na wamepewa title deed. Kwa sababu saa ile Bwanaamekufa inakua kitu ingine. Majane anataabishwa upande huu, na upande ule hata aoni vizuri na ana watoto. Sasa hii uridhi ikigawanywa mbele sana itakua akikufa hakuna taabu.

**Com. Phoebe Asiyo:** Unasema uridhi mzee aongea kabla ajafariki juu ya mali.

**Catherine:** Juu ya mali yake, na bibi huyu wake kwa sababu akifariki hata kakazake wanataka kila kitu cha huyu mjane amewachwa na anapata taabu sana.

**Com. Pastor Ayonga:** Lakini ataongea wapi?

**Catherine:** Aandike will.

**Com. Pastor Ayonga:** Aandike will, sawa.

**Catherine:** Tena sasa, taabu zingine zinapatikana na wajane, wakiwa wanaenda kuchukua pesa za wale wamekufa ama Bwanayake, anaenda mbali sana. Uko kwa trustee ni mbali sana na akienda kwa wakili anapata hii, anapata huyu, anataka hiki anataka huyu mama. Hata saa ingine anataka mama awe rafiki, na hiyo ikiletwa katika division hatapata mambo mabaya mengi. Hata saa ingine anaambiwa lala hapa nitakuja na hiyo si mzuri na hasa hasa siku hizi kuko ugonjwa mbaya.

Sasa naongea tena kwa watoto wasichana. Wasichana ni wazuri, msichana akipewa shamba. Ikiwa anaweza kupewa shamba na baba yake, akiwa bado kuolewa ni vizuri awe amekaa mpaka miaka arubaini. Kwa sababu hapo mtoto wa miaka arubaini kuolewa ni gumu. Sasa hapo anaweza kugawiwa shamba. Kwa sababu wengine anagawiwa akiwa mdogo kama miaka ishirini. Akiolewa anataka hiyo mali iwe yake. Na unajua watoto wavulana wako hapo wanaangalia ndio saa zingine mnasikia ama mnaona wakibishana kwa sababu ya hayo.

**Com. Phoebe Asiyo:** Na hii miaka arubaini atakua anaishi kwa baba yake? Na kama wazazi wamefariki, nani atapeana hiyo.

**Catherine:** Wazazi watasema mbele, kwa sababu wakifariki yeye bado kuolewa, hata akiwa na 35 years, si atasemea watoto wengine. Ama mtoto yule wa kwanza akiwa ni mwanaume aseme huyu mtoto lazima apewe hiki ama wamgawie.

**Com. Pastor Ayonga:** Mama bona usingeweza kusema pia kwamba watoto wanapogawiwa mali, wapate title deed zao, hata kama mzee atakufa itakua mtu ana title deed yake.

**Catherine:** Sasa siwanaweza kupatia mtoto yule ataolewa.

**Com. Pastor Ayonga:** Na akiolewa unataka hii mali ifanyweje?

**Catherine:** Unajua hiyo ndio experience, wakigawiwa wakiwa wadogo wakiolewa wanasema hiyo mali ni yangu, nilipewa na baba yangu na hiyo ndio ghasia inaweza kuigia between wale wanaume.

**Com. Phoebe Asiyo:** Na kama ni udongo iko kwa town. Kama amejenga nyumba yake ghorofa hapo. Unataka akiolewa hiyo nyumba yake iende.

**Catherine:** Hapana ikiwa ni yake ni yake. Lakini yule anaweza kupewa akifikisha miaka arubaini si yule ni afadhali hawezi kuolewa.

**Com. Pastor Ayonga:** Endelea.

**Catherine:** Ingingine hiyo circumcision ya wasichana iondolewa ni mbaya. Sasa nataka ingine ya administration, PC, DO, DC, Chief, Sub-chief na headmen, iwe line kama hiyo na sasa headmen wawe wanapewa mshahara hata ikiwa ni kidogo.

**Com. Phoebe Asiyo:** Hao ni clan members.

**Catherine:** Sasa kama MPs, wawe wanakaa miaka kumi, councillors miaka kumi, wards za councillors zimepunguzwa ziongezwe. Na sasa tena hizo dawa za kulevya zimefanya watoto wawe wenda-azimu, hata kama mwingine amesema, mimi naongezea hiyo. Vyama vya siasa view chache sana kama tatu. Hayo tu.

**Com. Phoebe Asiyo:** Asante sana kwa kuongea na sisi, utaenda pale kule tulikotoka halafu uandike jina lako. Nani alikua atongea nyuma ya huyu. Sasa wewe ukiongea huyu atafuata halafu huyu halafu yule yuko nyuma. Wewe ndio sasa umetoa mkono uja toa tangu uingia hapa kwa hivyo utakuja nyuma zaidi. Haya tueleze jina lako.



**Margret Mwikali Mutua:** Naitwa Margret Mwikali Mutua. Mimi naongea juu ya assistant chiefs. Assistant chief ni mtu ameandikwa lakini nikienda ni kushtaki kama niko na kesi kwake akikuja kwangu mpaka anaitisha kitu kidogo na yeye ameandikwa. Sasa na mimi nimepeleka kesi kwa sababu yeye ameandikwa, ameandikwa juu yangu. Sasa hiyo kitu kidogo kama sina, hio kesi yangu hawezi angalia. Kwa hivyo ningependelea wasiitisha hiyo kitu kidogo. Na headmen wako huko ndio wanawafanyia kazi. Nao wawe wameandikwa, wawe wanapewa mshahara. Inginge mimi naongea juu ya mwalimu. Mwalimu ameandikwa na akimaliza kazi yake anapewa retirement. Sasa hiyo retirement tuna ile kamati iko inarudi tunaambiwa nyinyi wazazi mpaka mtoe kitu tupatie huyu mwalimu na sasa kama hiyo kitu hakuna mtoto anatolewa kwa skuli.

**Com. Phoebe Asiyo:** Unataka tufanye namna gani?

**Margret:** Inataka wawe wakitoka tu bila kuitishwa tuwafanyie party ya retirement. Kwa sababu ameandikwa na mzazi hana kitu na hiyo party mzazi ndiye anafinywa anatoa hiyo pesa tumnunulie zawadi. Hiyo wazazi wanafinywa hiyo ndio ningependelea wawe wasifinywe. Inginge ni juu ya title deed. Title ningependelea iwe iko ya wazazi wawili. Mwanaume na bibi yake. Hiyo title deed iwe imeandikwa majina mawili kama vile marriage certificate inaandikwa. Hiyo ningependelea hivyo.

**Com. Phoebe Asiyo:** Asante sana, nani yule alikua atakua ataongea? Mama wewe umeingia saa hii hauwezi kuongea. Kuna huyu alikua nyuma yako msichana atakuja hapa. Wale wameongea pengine muwapatie nafasi wale hawajaongea ndio wapate viti. Haya, sasa tutafanya hivi. Watu wamekuja wengi, pengine wengine hawataki kuongea, wengine wanataka kuongea. Kama mtu amesema habari ile ulikua unataka kusema na umetosheka hakuna haja kuongea, lakini kama hajasema lazima uongee. Sasa huyu mama anasema jina lake na anasema habari yake. Naona tumefika hata mia nne saa hii. Na wale waliomaliza wanaweza kuacha viti kwa wale ambao wamekuja wapya. Hebu sema jina lako mama na uendeleo dakika tatu.

**Stelamaris Nthule Mutisya:** Jina langu ni Stallamaris Nthule.

**Com. Phoebe Asiyo:** Hebu tusikie tusilize huyu mama hatuwezi kumsikiliza kama mnaongea. Nyamazeni tafadhali tusikie yule anaongea sasa. Hii mashini haiwezi kishika sauti yake mkiongea namna hii vile mnafanya.

**Stelamaris:** Mimi naongea hali ya uchaguzi ya mwaka huu.

**Com. Pastor Ayonga:** Jina nini?

**Stelamaris:** Stelamaris Nthule Mutisya. Mimi naongea hali ya Raiswetu angao wakati huu akiwa amemaliza miaka yake ya kukaa kwa kiti, atachaguliwa mwingine, tunaongea apewe heshima kwa sababu tukianza uchaguzi tutaanza matuzi na tunakaa naye miaka mingi tunaanza kutukanana na mimi naonelea hiyo si mzuri. Kwa sababu hata kama mtu amewaongoza miaka tano anatoka panapewa mwingine hali ya matusi iondolewe.

Ya pili, wazee wetu wapewe wasichana wao heshima. Kwa sababu mzee anazaa msichana wake na ana gari yake utaweza kuona msichana wake anabebewa hapa mbele na anaende ana baba yake na hamjui wanaenda wapi. Mtoto anabebwa na baba yake, anabebewa hapa mbele na wewe mama haujui hao watu wanaenda wapi. Na huyo ni baba yae na yule ni msichana wake. Mimi naonelea wazee wapee watoto wa kike heshima. Ile heshama ya zamani ilikua mtoto msichana hawezi kuguza babake na nguo zake, na siku hizi sijui ni kama kizungu gani hiyo. Unaona baba mtoto kama huyu anaanza kubusu msichana wake. Hiyo kweli, ni ukweli anu ni mambo gani hiyo. Hiyo inaleta wa mama wengine wafuguzwe ndani ya nyumba zao ni wasichana wao. Hayo ndio nilikua nayo.

**Com. Phoebe Asiyo:** Asante sana mama Mutisya kwa mambo yale umeyatoa nenda pale chumba kile kingine uweke register kwa jina lako. Sasa ni wewe halafu wewe. Na wewe ulikua umesimama saa zile?

**Rose :** Si ndio.

**Com. Phoebe Asiyo:** Basi ongea. Rose jina lako lingine ni nani.

**Rose :** **Rose** Mumbe Mutua.

**Com. Phoebe Asiyo:** Sema kwa nguvu ndio watu wasikie.

**Rose :** I want to say, yale yamesemwa na Kalondu. She said about the chang'aa and I want to support her.

**Com. Phoebe Asiyo:** Yule alionge juu ya chang'aa, unataka uende kule upande wa wanaume.

**Rose :** I want to support her. Because I came here to say that.

**Com. Phoebe Asiyo:** You want to support her. Unataka imalizwe kabisa.

**Rose :** Imalizwe kabisa.

**Com. Phoebe Asiyo:** Chang'aa?

**Rose :** Ndio.

**Com. Phoebe Asiyo:** Nani yule nimemwambia aje? Wacha aongee halafu wewe uje.

**Anastasia Ndinda Kioko:** Kwa majina naitwa Anastasia Ndinda Kioko.

**Com. Phoebe Asiyo:** Huyu anaongea sasa ni Anastasia Ndinda Kioko. Haya ongea sasa.

**Anastasia:** Mimi naongea juu ya hao watoto wamewachwa na wazazi wao. Sasa hao watoto tuseme mzazi mama ameaga dunia. Tunakaa mwaka mmoja ama mbili na yeye baba anafuata, na hao watoto ni wadogo na wako shule. Sasa wakienda shule wanafukuziwa school fees. Sasa tena hana chakula ya nyumba.

**Com. Phoebe Asiyo:** Unataka tuandike Katiba hili hao wasaidike kwa njia gani?

**Anastasia:** Sasa hao watoto wasaidiwe na school fees, wawe shule hawafukuzwi sasa wakifukuzwa watatoa pesa wapi, na chakula wawe wanatafutiwa wanakula, sababu kama hawana chakula watatangatanga huku nje tu, wakitafuta chakula na hakuna mahali wanaweza toa.

**Com. Phoebe Asiyo:** Chakula peke yake.

**Anastasia:** Chakula na school fees, wawe wanasaidiwa.

**Com. Phoebe Asiyo:** Hiyo inatosha, nguo hawataki?

**Anastasia:** Na nguo.

**Com. Phoebe Asiyo:** Na matibabu hawataki.

**Com. Phoebe Asiyo:** Wakiwa wagonjwa.

**Anastasia:** Wanapelekwa hospitali. Kama karibu kuna assistant chief anaangalia hao watoto. Anawangalia anawasaidia.

**Rael:** Unatukanwa mpaka una-loose confidence, halafu unatoka huyo mwanamume sasa naye anajipeneza, kwa sababu yeye can stomach abuses and everything that is bad. Kwa sababu mwanamume hana haya. Lakini mwanamke akitukanwa anaona haya na anatoka anaanza kulia, hicho kiti sasa kinaenda na wanaume. Sisi hatutaki hivyo. Kwa hivyo, tungeuliza Katiba ikitengenezwa itengeneze mambo ya wanawake katika siasa, wanawake wasitukanwe. Wawachwe mtu akiongea maongozo yake ndio yatamtoa hapo lakini sio kutukanwa. Kile kingine ingawa ni watu wengi wameongea juu ya hiyo, ni juu ya wasichana wetu. Wale wanadunga wasichana wetu mimba, awe ni wa shule au si wa shule lakini msichana ambaye ako under 18 years. Awe analindwa wakati amedungwa mimba na mtu. Huyo mtu achunge huyo mtoto, alee huyo mtoto na wakati mtoto atakua mtu mzima, huyo mwanaume atakua amemzaa apatie huyo mtoto shamba na mali yake ingawiwe huyo mtoto. Na kama ni wasichana huyo mtoto asomeshwe mpaka amalize shule kama wale watoto wengine. Na huyo mwanamume alazimishwe.

Kile kingine ningeeongea juu ya machifu na assistant chifu. Ningependekeza machifu wawe wanapatiwa transfers na assistant

chifus kwa sababu hao machifu wetu na assistant chifus ndio wameleta mambo mabaya hapa. Sisi ni wabaya na watoto wetu ni wabaya lakini hao ndio wabaya zaidi. Especially tunakuja wakati tunatengeneza hii pombe hasa pombe ya chang'aa na hiyo pombe mbaya sana. Hao machifu kama ni mini ninatengeneza pombe na huyu mwingine anatengeneza pombe na huyu mwingine. Chifu anakuja na assistance chifu anakuja na ananiambia wewe usijali bora uwe unanipatia pesa. Nitakua nikija kuchukua pesa kwako. Shilingi mia mbili kila 15<sup>th</sup> ya kila mwezi. Assistance chifu anakuja kuchukua, naye chifu kwa sababu anaona haya anamtuma mtu mwingine for the same amount or bigger. Anaenda kwa yule mwingine, hivyo hivyo. Katika hii mwezi katikati 15<sup>th</sup>, anazunguka anazunguka na kwa hiyo sub-location watu wamelewa kabisa na yeye amepewa pesa. Sasa anaaza kuuza kwa ile makosa amewekwa alinde. Anaanza kuchukua mshahara kutoka kwa hao watu, wenye kutengeneza pombe na anakimbilia ile mshahara ya Serikali. Kwa hivyo watoto wetu wamearibika na hiyo mambo ya kutengeneza pombe haitaisha kwa sababu ya chifu na assistance. Kwa hivyo ningependekeza hao watu wapewe transfer huyu akikaa muda huu paletwe mwingine ndio tuwafuate.

**Com. Pastor Ayonga:** Lakini mama transfer itasaidia nini na mtu huyu akipelekwa transfer ataendelea na hayo na huyu anayeingia pia ataendelea na nayo.

**Rael:** Sasa akipatiwa transfer, atakua anapatiwa transfer kama punishmental transfer. Kwa sababu ya hii makosa. Na sasa amejulikana anafanya hivi. Sasa akirudia hii makosa akienda kule siafutwe kazi basi.

**Com. Pastor Ayonga:** Bona asingepolekwa kortini badala ya kujukua transfer?

**Rael:** Wakati anafuguzwa kortini atafuguzwa na korti kwa sababu huko atapelekwa kortini. Basi korti itaamua yeye afutwe kazi. Point yangu ya mwisho ningengea juu ya advocate. Ningependekeza hao advocates wetu sisi clients wao tuwe tunalindwa sana. Kwa sababu advocates wamekua watu wengine wanatunyanyasa sana, unaona mtu ambaye sio mwenye elimu, hata na wengine ni wenye elimu na hawaelewe na sheria, sasa huyu advocate anakua na firm yake hapa. Ako na watu wengine wanamsaidia, ako na makarani. Anamwachia karani awe akipokea claims na huyu karani ndiye anatoa malipo na hawaandiki. Nikija ananichukua kama client, na ananiambia hiyo kesi yote itachukua elfu ishirini na tano. Na hiyo ndio mwisho, tumesikilizana na hataki kuandika hiyo, anakwambia hiyo verbally, sasa nikimpatia hizo pesa, kesho nikija ananiambia nimpatie pesa za transport. Kesho nikija anataka hivi, na hiyo kesi kabla ya kuisha nimekua nimemlipa pesa nyingi sana, ambazo hatukusikilizana na ninatoa hizi kwa sababu zina kitu kingine nataka anisaidie. Kwa hivyo ningetaka clients walindwe kutoka kwa advocates wao. Kama ni advocate, afanye kazi na kama ni payment ndio atauliza apatiwe hizo pesa, lakini sio makarani. Na wawe wakiandika receipt na advocate akikosa hayo ashtakiwe ndio huyo client arudishiwe pesa zake tena.

**Com. Phoebe:** Asante, sasa nenda huko.

**Rael:** Nitaenda kuandika wapi?



**Com. Phoebe:** Kule kwa wanaume, kitabu iko huko. We kaa sasa uongea.

**Monica** Musyoki: Mimi naitwa **Monica** Musyoki.

**Com. Phoebe:** Endelea **Monica** .

**Monica** : Sasa nauliza Serikali, kwa nini tukienda dukani tukinunua viti yule ameajiriwa ananunua viti. Na yeye anapata maelfu ya pesa, na mimi niko nyumbani na mzee wangu na sisi hatupati kitu. Hata watoto wetu, tumesomesha na hatupati kazi, tuko hapo nyumbani na huko dukani tunaenda kununua vitu pamoja na yule ameajiriwa na anapata pesa nyingi. Sasa tunauliza Serikali itusaidie tufanye nini.

**Com. Phoebe:** Haiwezi kua bei ya tajiri na bei ya masikini, vile mama nasema ni kwamba zamani kulikua na price control. Kama walisema mkate ni shilingi kumi na tano ni shilingi kumi na tano kwa kila mtu sidio. Siku hizi mtu anaweza kusema mkate yangu ni shilling ishilling wengine ishilling na tano. Au mtu aseme hiyo unga ni shilingi hamsini mwingine aseme ni hamsini na tano. Unataka turudishe price control ya vyakula?

**Monica** : Hapana, nataka Serikali kila chifu awe anajua kwangu nyumbani, yule ako na family, anajua na anajua nyumba yangu, watoto wangu, mzee wangu na mimi. Na anajua sisi hatuna kitu ya kutusaidia. Sasa huyu chifu apeleke report ya nyumba yangu huko kwa Serikali.

**Com. Phoebe:** Sasa apeleke jina yenu kwa Serikali mpate usaidishi?

**Monica** : Tunaweza kupewa na Serikali kwa sababu hatuna kitu na tumesomesha watoto ile sasa nilikua nayo nimeuza mtoto apate elimu.

**Com. Phoebe:** Ni vitu gani unataka mpewe na Serikali?

**Monica** : Ni kama zile tunaenda kununua. Sasa tutafanya nini, au wakikosa kutupatia watutafutie mahali watupelekee watoto halafu tupate kitu.

**Com. Phoebe:** Watoto waende wafanye kazi.

**Monica** : Wafanye kazi halafu watusaidie.

**Com. Pastor Ayonga:** Yaani mama ungependa ukienda kwa duka upewe sabuni, sukari, maziwa vitu namna hiyo?

**Monica :** Ndio.

**Com. Pastor Ayonga:** Na sasa nikikuuliza, kama hiyo duka ni ya huyu mama, yeye alienda akaleta vitu kutoka Nairobi ameweka kule. Ameuza ng'ombe zake amepata pesa anaenda ameleta vitu ameweka, sasa wewe unaenda unachukua bure?

**Monica :** Hapana sitaki hivyo, nataka Serikali ingalie hapa kwa nyumba yangu, ichukue watoto wawili au watoto –

**Com. Phoebe:** Kama hawawezi kufanya watoto wapate kazi walishe wewe?

**Monica :** Ndio. Na ingine kutoka huko kwa utoto wangu nikiwa shule, nilisikia mzazi wangu akisema tulikua tunaenda baraza huko, tumeitwa na chifu huko. Tukawauliza machifu wanawaitia nini? Machifu wanasema Serikali inataka tupatiwa maji tuwekewe huko kwa boma zetu kila mtu awe na maji. Tukamuliza hiyo maji itatoka wapi? Akatwambia tumeambiwa na DC itatokea hapa kwa mlima huu unatoka Machakos halafu ije kila mtu apate maji. Sasa mimi nimekua mzee na hayo maji ninangojea na niSerikali ilikua ikisema namna hiyo. Sasa hiyo ni Serikali ya namna gani?

**Com. Phoebe:** Unataka tuseme namna gani?

**Monica :** Nataka kuuliza Serikali ilete maji itusaidie vile walisema.

**Com. Ayonga:** Enda uko juu.

**Com. Phoebe:** Asante sana, wewe unaitwa aje?

**Rose Mueni Mukio:** Kwa majina naitwa **Rose** Mueni Mukio.

**Com. Phoebe:** Sema machache sana.

**Rose :** Yangu yale yanafinya ni kuhusu school fees, kwa muda na kwa wakati huu tunataabika sana, sana sana watu ambao wanamapato ya chini sana. Na school fees inakua to maximum, ukienda kama Matungulu Girls, kama ni thirty shillings wale wako na pesa ndio watalipa wale masikini wataangamia.

**Com. Phoebe:** Wewe unapendekeza aje?

**Rose** : Napendekeza kama itawezekana hiyo school fees iwe imewekwa kwa kiwango ambao kila mtu anaweza kulipia mtoto wake. Na ya pili, ningepomba kama ingewezekana hao watoto wakimaliza shule kuwe na mradi wa kuwasaidia. Kama kunaweza kuwa na project moja iwekwe Matungulu division. Hao watoto wawe wakiingia hapo wapate course bila kulipa kitu. Ni hayo tu.

**Com. Phoebe:** Haya endelea.

**Monica Mumo:** Kwa jina naitwa **Monica Mumo**. Point yangu ya kwanza ni kuhusu hospitali za Serikali, tungeomba Serikali itoe hii kitu inaitwa cost sharing. Kwa sababu tukiangalia kwa udani kabisa, hakuna kitu kama hiyo. Ni kama sisi wenyewe tunajilipia kila kitu kwa hospitali. Kwa sababu ukifika unaambiwa enda ukalipe kadi, unalipa shilling ishirini. Siku hizi ukiangalia unaona wa mama wengi wameacha kuzaa kwa sababu mama akienda huko martanity kuingia hivi kitambo upate mtoto ni elfu moja na mia tano. Governmenthospitals, sasa tumeshidwa Serikali hii cost sharing mnasema ni cost sharing namna gani, si waweke vile ilikua mbeleni.

Point yangu ya pili, ni kuhusu hii, secondary school quata system. Hiyo naye imeumiza district zingine sana, watoto wengi wamepita hawapati nafasi ya kwenda university kwa sababu ya hiyo quata system. Sasa ningepomba Serikali itoe hiyo kitu inaitwa quata system. Ndio watoto wetu wapate nafasi university. Point ya tatu, ni Governmentprimary school. Ningepomba Serikali isaidie primary school education iwe free. Sasa watoto wengi unaona chokora ni kukosa pesa za kwenda shule. Point ya nne. Child Labour: Sasa kama ni mimi sijaolewa nipate watoto, sina mahali natoa pesa, hao watoto lazima nipeane wafanye kazi. Ndio tunaona hii primary school ikiwa free itasaidia sana hii child labour itaisha.

**Com. Pheobe:** Wangapi wanataka kuongea hapa? Watatu ndio tumalize, we nenda kule uongea kule ndio tumalize.

**Com. Ayonga:** Wengine kule wanaendelea kama sita.

**Com. Phoebe:** Wacha wakae hapa, lakini wewe useme haraka.

**Rose** : Nimebakisha point ya tano, ya tano ni kuhusu judges na advocates. Ukienda kortini hao judges and advocates kuna relation wako nayo. Kesi yako kama hujachukua advocates, huyo mtu uko na kesi na yeye ako na advocate hiyo kesi inapelekwa miaka nenda miaka rudi. Na ukiona advocate akienda kwa korti, kunahusiano ako nayo na judges. Ile ingine ni kuhusu Serikali, tunaona Serikali iwe na mashamba ya kulisha watu wale masikini. Sio mambo ya kuomba omba msaada saa yote tunaletewa yellow maize. Kama kungekua na mashamba Serikali kama hiyo Serikali inalima ingekua inalisha watu wake aingekua inaomba misaada saa yote kutoka nje unaletewa yellow maize, unaletewa unga ingine sijui inaitwaaje. Kama hii food, hii ya shule, kama Serikali ingekua na mashamba hatungekua tuonaongojea hiyo ya kutoka nje. Point zangu zilikuwa hizo.

**Com. Phoebe:** Asante sana.

**Com. Ayonga:** Sema majina mama.

**Winfred Joel:** Mimi naitwa Winfred Joel.

**Com. Phoebe:** Hauna jina ya kiafrika.

**Winfred:** Kikamba, ama Wanza Joel, usitie Bwanayangu nyuma, andika yote watatu,  
Winfred Wanza Joel.

**Com. Phoebe:** Umeniambia nisiweke Bwanayako nyuma, siwezi kuweka yeye nyuma, siwezi kuweka yeye nyumba.

**Winfred:** Shida ile niko naye nikuonelea sisi wanawake tunaungana vikundi. Na wakati tunaungana vikundi, tunaendelea na mipango tunatoa pesa kidogo namna hii na hatuoni mtu wa Serikali akitusaidia. Wakati juu inakunja tunagawanyika, kila mtu anakaa kivyake kwa maana hatuna pesa. Hakuna ile madizi unauza.

**Com. Phoebe:** Sasa unataka tufanye namna gani?

**Winfred:** Tunataka wakati tumeungana pamoja, tuwe tunaonwa na hao watu tumewachagua. Serikali iwe inatumia kama ni wanawake wanakikundi wa Kangundo, watumiwe mtu wa Serikali akuje kuwatia moyo.

**Com. Phoebe:** Wale wa social welfare au?

**Winfred:** Ndio wakuje kututia moyo, iwe inapeana mtu mmoja anakuja kama ni Kangundo wakati kama siku hii ya leo tukusanyike, tukuwe moyo.

**Com. Phoebe:** Wasomeshe nyinyi.

**Winfred:** Watusomeshe kitu, yule mtu ambaye hajasoma ajue kuuza madizi wakati mvua imenyeshwa anaweza kujisaidia na nini.

**Com. Ayonga:** Okay. Endelea mama.

**Winfred:** Ya pili naonelea hao wazee, wakati mzee anafanya kazi anafanya kazi, anakua anachoka kama anakuja kuchukua pension na hana transport, na ile transport anapata kama siku ya leo Friday kama leo anakuja, anaambiwa tutaanza kulipa Monday, na hiyo Monday anaambiwa tutalipa Tuesday, na hiyo Tuesday, Thursday, inamalizika wiki moja. Wazee wasaidiwe

pension ikuwe ni siku moja.

Sasa kama mimi nataka kufanya biashara, nakuta mtu wa council akiwa amesimama stage Kangundo. Ananipea ile receipt na unajua mimi sijasoma, naelekea Nairobi sasa. Nikifika Nairobi yule mtu mwingine wa Council akisoma hiyo anasema hiyo ni karatasi. Hataki kusikilizana na yule mtu wa Kandundo. Sasa nataka hiyo kitu iandikwe pamoja. Ile receipt yakutoka Kandungo iandikwe na yule mtu anatoka Nairobi. Wakati huo hiyo karatasi nararua inatupwa nje. Sasa akina mama tuko na shida sana ya biashara. Hatujui tutapitia njia gani. Tunataka Serikali iangalie watu wa kazi wasikilizane pamoja. Hili tuone usaidishi. Mimi namaliza hapo.

**Com. Phoebe:** Wa mwisho kabisa ni huyu. Wewe ndio umeingia saa hii. Wewe uende kusikilizwa kule.

**Monica Muthengi:** Mimi naitwa **Monica Muthengi**. Hata mimi nashangaa kwa hii mambo ya council. Unaona wananyanyasa hao wamama. Mama anatoka kwa nyumba, anachukua kitu kidogo kama ile manaku, anatia kwa kiondo kidogo, halafu akiweka huko chini watu wanakuja wa council wanampea receipt ya shilingi kumi na tano na hiyo kiondo haiweze kutoka hiyo pesa. Pengine shilingi tano tu. Hapo tunashangaa sana. Hata saa zingine tunaenda kununua viazi hapa kwa soko, debe moja. Ukieka kila siku unachukuliwa shilingi kumi na tano, mpaka siku hiyo ingine unakwenda unachukuliwa shilingi kumi na tano, sasa tunashangaa hiyo debe haiwezi kwisha siku hiyo, lazima uuze mpaka wiki moja. Ndio tunataka council isaidie wakina mama.

**Com. Phoebe:** Unataka namna gani tuandike kwa Katiba?

**Monica :** Mimi nataka wasaidie, wawache kunyanyasa namna hiyo.

**Com. Phoebe:** Unataka hiyo mambo ya hiyo pesa itolewe kabisa? Kwa ile biashara ndogo ndogo.

**Monica :** Ndio.

**Com. Ayonga:** Na council itapata aje pesa?

**Monica :** Mama wanatabika sana.

**Com. Ayonga:** Ndio lakini council itapata aje pesa.

**Monica :** Councili iko na pesa nyingi sana.

**Com. Ayonga:** Si ndio inafagia kule soko.

**Monica :** Wapunguze, kwa watu wenye vitu kidogo, kidogo.

**Com. Phoebe:** Unaitwa?

**Anna Mbithe:** Naitwa Anna Mbithe. Yangu ni kuhusu hao wajumbe tunachagua. Sasa siku za siasa ndio tunawaona, na sasa tukiwaona siku za siasa wanatupatia kitu kidogo, kama shilingi elfu tano tungawanye na tukungawana hiyo ndio inakua mwisho wao. Tukiwapatia kura, wanaenda kabisa, hajui vile maisha inakua ngumu, awasaidii na chochote, sasa tutawaona siku zingine za siasa zikikaribia. Watakuja wanasema tutamfanyi hivi na hivi, lakini zikimalizika wanaenda kabisa kabisa. Wanakua na miaka tano kwa bunge, sasa tupunguze ikiwa mtu afanyi kitu chochote kwa bunge, tupunguze iwe miaka tatu ama miaka miwili, wawe wanaendelea ama mtu andelea na kulingana na vile anavyotumikia wananchi.

**Com. Phoebe:** Lakini umesema kitu nataka kuuliza. Umesema wanapatia nyinyi shilingi elfu tano muende mgawane. Sio wanaona wamewanunua sasa hakuna aja ya kurudi.

Anna: Ndio wanatufanyia hivyo.

**Com. Phoebe:** Kwa nini nyinyi mnachukua hiyo pesa?

Anna: Ndio tunafanya makosa.

**Com. Phoebe:** Kama hamkuchukua pesa wangerudi wafanye kazi. Bona mnachukua hiyo pesa?

**Anna:** Unaona kama tuko wengi, inachukuliwa na wanaume ama wanawake wako na nguvu za kuchukua na wanagawanya.

**Com. Ayonga:** Kama wangeleta elfu ishirini ingekua mzuri kidogo. Okay tumesikiza. Asante sana, hiyo ni point imeshafanywa mama. Sasa itakua huyo na ndiye wa mwisho kabisa.

**Justina Mulwa:** Kwa jina naitwa Justina Mulwa, Shida yangu ningependa kuuliza Ministry ya finace kwa wale wa pension, mzee wako akifa unapewa pension kwa miaka mitano, na yule ako hai anaendelea tu na saa zingine unawachwa na watoto wachanga na ukimaliza miaka tano ndio wanafika form one, hizo classes zina fees mingi. Na wale watoto wangu nikiwa sina pesa wanakaa chini na yule ako hai watoto wake wanasoma wanamaliza shule. Tunaomba Serikali itusaidie hili wale wanawachwa hili waendelea na kupokea ile pension wasaidie watoto. Kwa sababu nikiwachwa siwezi kuenda kufanya kazi, na yule amewachwa mwanaume anaweza kwenda kufanya kazi ingine na anaendelea na anakula maisha. Na mimi, kwa sababu

ya uzito wa kazi za nyumba siwezi kwenda kufanya kazi.

**Com. Ayonga:** Mama tumelewa kile ambacho unataka, mtu akifa wale ambao amewacha, kama sasa Bwanaamekufa amewacha bibi yule bibi apata yale malipo ya yule mtu ili aweze kusaidisha watoto wake.

**Justina:** Ndio.

**Com. Phoebe:** Wewe ulikua hapa zamani kweli ama umekuja saa hii?

**Nzisa Mbaluka:** Nukie kwa kya.

**Com. Ayonga:** Useme kiswahili, kama sivyo hatuwezi kuelewana na wewe.

**Nzisa Mbaluka:** Ndisyi Kiswahili.

**Com. Ayonga:** Basi urudi sokoni.

**Com. Phoebe:** Siulikua sokoni?

**Nzisa Mbaluka:** Aiie.

**Com. Ayonga:** Haya sema yale unataka kusema. Majina?

**Translator :** Si uongee kiswahili.

**Com. Ayonga:** Wacha waongee kikamba lakini atwambie majina kwanza.

**Com. Phoebe:** Lakini huyu alikua mbele yako.

**Nzisa:** Aha oka ambithia.

**Com. Ayonga:** Unaitwa nani?

**Nzisa:** Nzisa Mbaluka.

**Com. Phoebe:** Ongea.

**Translator :** Woni waku ndukatutavyie ngewa.

**Nzisa:** Woni wakwa, thina ula twikwona ni wa asee kunywa uki. Mundu amuka kwakya athi kwakya no wioo. Nasya ala maua uki mavingiwe, nikenda mundu alia kuthi ukini niwetela alika mundane aima twona leu wa kuya.

**Translator :** She is proposing that those people who manufacture brews should get stiff penalty, so that men may be productive.

**Com. Phoebe:** Asante sana.

**Com. Ayonga:** Na wewe?

**Ruth Mbithi:** Mimi naitwa Ruth Mbithe.

**Com. Ayonga:** Sema.

**Ruth:** Mimi nasema juu ya biashara kwa wanawake kwa sababu tunabeba vitu halafu tunaleta kwa soko, na tukasumbuka sana juu ya council na tunauliza hii itakua aje.

**Com. Phoebe:** Wewe ndio utwambie.

**Ruth:** Ukibeba vitu ndogo, unalazimika utoe pesa nyingi.

**Com. Ayonga:** Ndio tunakuelewa lakini unataka aje?

**Ruth:** Tunataka ipunguzwe.

**Com. Ayonga:** Tena neno lingine?

**Ruth:** Halafu nitasema juu ya watoto kwa shule. Fees iko juu na tunataka kusomesha nataka Serikali, itoe free education ama ikue chini.

**Com. Phoebe:** Na wewe mama unakaa tu kwa kazi yako, halafu unakuja sasa.



**Nzula Willy:** Nilikua huko nyumbani nikaambiwa wanawake wanakuja hapa.

**Com. Phoebe:** Hebu sema jina lako?

**Nzula Willy:** Jina langu ni Nzula Willy, sasa mimi naona tunaumia sasa, watoto wetu wanamaliza shule na wanakosa kazi. Ikiwa wewe una chifu, ukienda kutafutia mtoto wako kazi unaitishwa.

**Com. Phoebe:** Unapendekeza namna gani kwa Katiba?

**Nzula:** Itengeneze hivi, ikiwa mtoto wako anamaliza shule na anaenda kufafuta kazi, hata akiitishwa pesa na akiwa hana pesa huyo mtoto takaa tu sasa tufanye nini.

**Com. Phoebe:** Ni ambie unataka tufanye namna gani? Pendekeza?

**Nzula:** Murekebishe watu hao wanaitisha watu pesa nyingi, na watu hawana kitu. Si wengine wana pesa, warekebishe. Kwa hivyo, hata ofisini ukienda, ukitafta death certificate ya Bwanayako akiwa amekufa, kutafutiwa ile file unaitishwa pesa na wewe ni masikini. Maofisi yote ataukienda kuitisha kipande unaitishwa pesa.

**Com. Phoebe:** Kwa hivyo tumalize corruption?

**Nzula:** Ndio.

**Com. Ayonga:** Na kama kitu ambacho unataka kusema ni kile ambacho mwenzako amesema tafadhali uanche hayo. Kama unataka kusema kitu sema kile mwenzako hajasema. Mama wewe ni?

**Betrice Mueme:** Mimi jina langu ni Betrice Muema. Changu ni juu ya wanaume wale wanabachika watoto mimba, wengine ni sugardaddy, wengine ni nini, hii sheria irudishwe kama ile ilikua ya zamani, kama mwanaume amebachika msichana mimba achukue chukumu la mtoto.

**Com. Phoebe:** Affiliation Act?

**Betrice:** Ndio.

**Com. Phoebe:** Nanimeandika namna hivyo, kama vile ulisema, thank you.

**Com. Ayonga:** Sasa hiyo ndio kitu kingeni amesema point ambayo haijasemwa lakini kama nikurudia yale mwingine amesema.

**Com. Phoebe:** Unaitwa?

**Monica Mumo:** Naitwa **Monica Mumo**, nitaonge juu ya election.

**Com. Phoebe:** Lakini iwe ni point moja ile imebaki tu.

**Monica :** Ni point moja tu, election be conducted in secret ballots, and votes be counted at the polling station.

**Com. Phoebe:** Hiyo imekubaliwa, sitahesabiwa huko huko tu.

**Monica :** Ile ingine, Constitution should be written in simple language and if possible every citizen should have a copy.

**Com. Phoebe:** In English?

**Monica :** And Kiswahili.

**Com. Phoebe:** Naikipigwa Kikamba?

**Monica :** I do not think whether it will be possible.

**Com. Phoebe:** Constitution ya South Africa, imeandikwa kwa lugha yote ya watu wa

South Africa. Kwa hivyo, wewe upendekeze, unataka nini?

**Monica :** Kikamba, Kiswahili and English.

**Com. Phoebe:** Hapana, Kikuyu au Kijaluo au Kibaluha.

**Monica :** Hao wataona, tena Constitution should prohibit police torture.

**Com. Ayonga:** Sema kitu kigeni.

**Rhoda Syombua:** Hebu kwanza uniangalie kama hii imesemwa. kwa sababu naweza kusema kitu imesemwa.

**Com. Phoebe:** Sema tu, nipe jina kwanza mama.

**Rhoda Syombua:** Niko na shida ya macho, lakini nitajaribu, kwa sababu nimesahau mewani. Jina naitwa Rhoda Syombua.

**Com. Phoebe:** Haya sema Rhoda.

**Rhoda:** Changu cha kusema nataka mageuzi ya Katiba kusiwe na mtu ako juu ya sheria. Inge ya pili, nataka mtu wa kusimamia kura awe akichaguliwa na wabunge vila wanachagua ule amewasimamia.

**Com. Ayonga:** Si mama umeandika?

**Rhoda:** Ndio. Ya nne, niwe ni kisoma, ama niwache?

**Com. Phoebe:** Hapana weka sign hapa, sasa hii ni yetu.

**Com. Ayonga:** Sisi tutachukua hii, kwa maana tumefunga.

**Com. Phoebe:** Wacha huyu awe ni wa mwisho.

**Margret Mbathi:** Kwa jina naitwa Margret Mbathi. Mimi yangu ya kwanza ni juu ya watoto wale hawana wazazi vile wanavyoteseka.

**Com. Phoebe:** Sema vile unataka tuwafanyie.

**Margret:** Tunataka wale watoto wakipewa pesa wawe na mtu wakuwasimamia.

**Com. Phoebe:** Unataka awe nani.

**Margret:** Kama susu (Nyanya). Ile ingine ni juu ya Head Master. Wanakaa kwa shule kwa muda mrefu sana na shule inaaribika, tunataka awe akikaa kwa miaka kumi, ili apewe transfer aende kwa shule nyingine. Ile ingine ni ya uchaguzi. Tunataka kama ni Matungulu tupewe mbunge wetu, ili mashida yetu awe akiyangalia, kwa sababu akiwa mbali hawezi akaangalia. Yale niko nayo ni hayo tu.

**Com. Phoebe:** Asante, kwa hivyo unataka tugawe, Kangundo iwe na constituency mbili, Kangundo na Matungulu.

**Com. Ayonga:** Sawa wamama mmeongea vizuri, lakini bona maneno hayo hamkuongea huko kwa wanaume.

**Com. Phoebe:** Tunaenda chakula nusu saa, halafu tutarudi kuchukua mengine. Si ndio? Bona nyinyi mulichelewa kuja?

**Com. Phoebe:** Kuna mambo mengine hamjasema, yako kwa roho yenu, kuna mengine tumeandika kama unaona iko kitu haijaandikwa, sema sasa ndio tumalize kila mtu. Margret Mbathi alikuja alisema ya mwisho, huyu alikuja na hatukusikilizana, mimi sijui kikamba. Sasa sema.

**Muteo Mutuku:** Nye nisi Kikamba. Nitawa Muteo wa Mutuku, nasya uu, yuyu nosa numba ya kitheka na musee akakwa na akwa yila numba iyi uthinisa kuya nilatitie.

**Translator :** Anataka title deed, kwa sababu bibi akifiwa na Bwanayake anapata shida kupata ile title deed. Iweze kurahisishwa.

**Muteo:** Nienda kuthiniwa kwo kwitwa mbesa. Nenda nzile ikwani na mwene wiva na ndevo. Na yuyu nenda mbesa ila makilie itia vaa na natiwa ni muthei niwisyi ni sya mbaiya. Twenda twone title vaa vakuvi na makwitia tuvesa tunini.

**Translator :** She is proposing they ask for title deed fee to be reduced.

**Com. Phoebe:** Sema jina?

**Translator :** Witawa ata?

**Kavindu Mbevi:** Nitawa Alice Kavindu Mbevi.

**Com. Phoebe:** Nauseme kwa nguvu.

**Kavindu:** Nina syana ndiwa. Yu syana isu nitona kwika ata na ndina mundu.

**Translator :** Ndukatukulyie maukulyo niwe ututavya undu tukwika.

**Kavindu:** Nienda mundavie kana syana isu nitona kusuvia, ukethiwa sukuli nosyatethesywa.

**Translator :** She is proposing free education for orphans.

**Com. Phoebe:** Asante sana, Kavindu. Sasa wewe msichana ulitaka kusema ulikua hapa na haukupata nafasi, unaitwa nani?

**Anasiata Mbatha Kyalo:** Anasiata Mbatha Kyalo.

**Com. Phoebe:** Anasiata, haya.

**Anasiata:** Ndio, maoni yangu ni kwamba sisi wanawake tunaumia sana, mimi niko na watoto wanne, Bwanawangu hafanyi kazi, hapo mbeleni akaoa mwanamke akaniachia wale watoto.

**Translator :** Unataka Katiba ifanye nini kutatua shida za wamama.

**Anasiata:** Wasaidie wanawake wale wanalea watoto mayatima.

**Translator :** Support for orphans.

**Anasiata:** Watoto wasome, wakule, na wavalishwe. Ni hayo tu.

**Com. Phoebe:** Ulisema bwana, yuko, lakini hana kazi na alikua na bibi alikua na watoto wengine mbele.

**Anasiata:** Ndio watoto watatu na bibi akafa.

**Com. Phoebe:** Na wewe uko na wangapi?

**Anasiata:** Mimi niko na mtoto mmoja na hao wote mimi nakaa nao. Sasa niko na shida.

**Com. Phoebe:** Asante, nenda pale uweke sihihi, usiende bila kuweka kidole. Tunamaliza mzee hata imekwisha. Councillor amaita wote waliokua wananugunika tumalize nao maanake wanataka kufika nyumbani mapema, hawataki kurudi saa nane. Kwa hivyo tunamaliza.

**Com. Ayonga:** Kwa hivyo kuna wale ambao hatutasikiza?

**Com. Phoebe:** Ndio, saa hii, kidogo tu.

**Com. Ayonga:** Utanipa karatasi kwa maana, yangu nimeacha kwa gari, mimi nimewatafuta.

**Com. Phoebe:** Endelea. Jina?

**Belita Ndave Wambua:** Belita Ndave Wambua.

**Com. Phoebe:** Sasa sema vizuri tusikie.

**Belita:** Maoni yangu ni kuhusu wamama huko nyumbani mwetu. Sisi wamama hatuna ule utawala wa akina mama nyumbani. Tuseme wa kuuza mali yenye tumetafuta mimi na Bwanayangu. Sasa tuko na watoto. Watoto hao wako mashuleni. Sasa zingine watoto hao wanafuguzwashule, wakifuguzwa shule wananitukuta nyumbani, saa hiyo mzee ameanda. Sasa nikichukua ile mali tumetafuta na mzee wangu nipeleke soko ni shida.

**Com. Phoebe:** Kama kuku au mbuzi. Ni shida mwanaume anakataa mtoto asiende shule.

**Belita:** Anakataa niende niuze, mtoto aende shule na mtoto ni wake.

**Com. Phoebe:** Na hiyo mbuzi ni wewe umelea?

**Belita:** Ndio, ni mimi napea chakula.

**Com. Ayonga:** Kwa hivyo unataka aje?

**Belita:** Mimi nataka sisi wamama tuwe na jukumu ya kufanya—

**Com. Phoebe:** Unasema kama umelea kuku au mbuzi yako mtoto yako anashida anataka kwenda kusoma, mzee anakataa usiuze na hii kuku ni yako. Unataka haki uuze kuku mtoto aende shule.

**Belita:** Ndio.

**Com. Phoebe:** Haya tumeandika hiyo.

**Belita:** Ile ingine nasema juu ya mama, si tunaleta vitu kwa soko, mimi nachukua ikiwa ni sukuma yangu, kufika sokoni, hata saa zingine kabla ya kufika sokoni hata bila chochote kwa mfuko, nikifika tu kwa barabara hiyo gunia inachukuliwa na watu wa council.

**Com. Phoebe:** Wewe unataka tufanya namna gani? Wanawake wamesema mambo hiyo wengi sana. Wewe maoni yako unataka tufanye namna gani.

**Belita:** Muangalie kodi iwe inatolewa baada ya kuuza, na itolewe kitu kidogo kuligana na kile unabeba kutoka nyumbani mwako. Kwa sababu sisi tunajisaidia sana na hiyo mali yetu ya shambani. Tuwe hatuumii sana, kama siku hizi.

**Com. Phoebe:** Tax according to value, asante.

**Belita:** Asante.

**Com. Phoebe:** Nani mwingine anataka kuongea?

**Nduku Kiilu:** Kwa jina naitwa Nduku Kiilu: Ile kitu nataka kuongea ni juu ya video. Kwa sababu hii video inaaribu watoto sana, kwa sababu wanawacha shule wanaenda kuangalia. Hii ndio nataka ifungwe.

**Com. Ayonga:** Lakini ni video yote mama, lazima pia ufafanue.

**Com. Phoebe:** Ni ya kanisa, elimu.

**Nduku:** Kunaingine ile mbaya ya weekend kama vile Jumamosi.

**Com. Ayonga:** Ya weekend, okay, zile video chafu. Kwa maana si kila video ni mbaya.

**Nduku:** Ile ingine ni masomo ya watoto. Wazazi wengine hawana pesa, kwa hivyo watoto wao hawaendi shule.

**Com. Ayonga:** Kwa hivyo wapewe free education.

**Nduku:** Ndio, ni hayo tu.

**Com. Phoebe:** Asante, nenda kule iko register uandike jina lako tafadhali. Kama unakitu umesikia mtu amesema, hakuna haja kurudia.

**Com. Ayonga:** Sema yako, kama huyo amesema video amesema vizuri sana.

**Com. Phoebe:** Jina.

**Grace Nzeki:** Grace Nzeki.

**Com. Phoebe:** Utasema kwa Kizungu?

**Grace:** Kikamba.

**Com. Phoebe:** Kwa nini, na wewe ni mtoto mdogo namna hii?

**Grace:** I will speak English.

**Com. Phoebe:** That's better. You do not have to translate.

**Grace:** Am talking of school fees. Many parents have no money to pay for the school fees for their children. The Governments should reduce school fees.

**Com. Phoebe:** Another one?

**Grace:** Hospital, when you take a patient to the hospital, for exmple Kangundo and you have no money, you have to stay there without being attended to.

**Com. Phoebe:** You want free health services? Sema wewe mwenyewe. Inginge.

**Grace:** Enough.

**Com. Phoebe:** Nenda kule uandike tafadhali usikose kuandika. Yes.

**Nduku Mutua:** Nduku Mutua.

**Com. Phoebe:** Jina ya kikristo?

**Nduku:** Celestine.

**Com. Phoebe:** Kwa nini haukutaka kusema hiyo?



**Nduku:** Nyeninena Kikamba.

**Com. Phoebe:** Ndio mzuri.

**Nduku:** yu yithie ene nzi nitwethiwe twina thina, nundu wa yu tayu tukite kukampeini uyisa kwithiwa ethiwa ni twakampainia mundu na nitwamina kumunenga kula, we athi ndatusyokia ingi.

**Translator :** We as the citizens are faced with problems with politician, because everytime they campaign and we give them votes when they go they do not come back.

**Nduku:** Nikenda tukekumunenga mathina maitu.

**Translator :** They do not want to listen to us.

**Nduku:** Ala twina mono kwa kavinda kala twamina kumsakua.

**Com. Phoebe:** Tufanye nini?

**Nduku:** Nasya ati, andu asu tusakua makathi na mailia kwosa mavata maitu, ithie kativa katwika ni kakwandikika yaani mathai nitwithiawa na thina. Vatoneka. Nenda andu aya twamina kumasakua mumatavie ati, kana yiywe tumutaviati tatai na vinya mutungamie nikenda wise kuthiwa nimeutumanya.

**Translator :** Nukwenda makavutwa ona miaka itano itenzelu.

**Nduku:** Nikwenda makavutwa itina ya miaka itano itemithelu.

**Translator :** She is suggesting they should be able to recall they MPs. If an MP does not function or a councillor the electorate should be able to recall him and elect another person.

**Nduku:** Kila kingi Yithie twina syana na twina syana asyii nitwalikile thinani. Nundu ethiwa ni kana nitwakasomethia na itina wa kukasomethia. Kaisa kwithiwa kakwata wia. Uyisa kwithiwa yu kwa ngalakanyo ve saa mutulekye ukesa kwithia twina thina twinukite.

**Translator :** She is concern that there is a problem of an employment for which she thinks should be everybodies right, and

she even says there are times when they be able to come out of this place and they may not be safe on their way home because there many un employed youth.

**Nduku:** Nivika vau.

**Com. Phoebe:** Asante mama. Na wewe ulikua umesema?

**Benignas Wambua:** Sija sema nilikua namsaidia yule mama.

**Com. Ayonga:** Tafadhali wamama muwache, sisi ndio tunaongoza.

**Com. Phoebe:** Sema jina, mimi ndiye nilipa kazi alikua hajaongea yake.

**Benignas Wambua:** Sasa ningependekeza Katiba hii iongea na wanaume watupatie ruhusa ya kwenda kwa kazi. Sasa saa zingine umeolewa, ulikua unafanya kazi hawataki uendelea na kazi, wanataka ukae nyumbani. Na nyumbani iko na shida nainataka usaidishi wa watu wawili. Kwa hivyo ningeponelea wanaume watupatie ruhusa ya kufanya kazi sisi wakina mama.

Ile ingine ningeponelea ni vizuri saa zile unasikia watu wanatukikana kwenda kwa jeshi ama kwa polisi. Sasa umepeleka mtoto wako na hauna pesa za kuwapea. Unasikia hatutaki mtu mwenye ni mrefu kiasi gani lakini dakika ya mwisho watu wengine wanachaguliwa wengine wanechukuliwa, haujui ni kwa nini, kwa hivyo pesa ya mangendo saa ya kuandikwa sana sana kwa Serikali ikome.

**Com. Phoebe:** Mama wewe ulikua hapa, wewe unaitwa.

**Easher Ndunge Munuve:** Easher Ndunge Munuve.

**Com. Phoebe:** Easher Ndunge, haya sema.

**Easher:** Ninena kikamba. Nasya ati, ethiwa nikutwikike kativa kavindue.

**Translator :** She is saying that now it has been said the Constitution is being reviewed.

**Easher:** Nitwithiitwe na thina mwito. Yulu wa syindu syitu ile tukwataa mbesa nasyo. Nitwosaa tukauwa mashamba tukaima miunda yitu , na muinda isu tukanoa twitethia wiya na tukanoa twitwaa vala tutwaa nikana twetewe mbesa. Na itina wa kukuetele twilia kwona mbesa. Na twakulilya twiwaa thina umanaa na vala kaawa witu utesawa. Kutoneka Serikali nitwikila

ethiwa nivangie mavindue kativa makunikilye muno muimi ethiwe na kindu kya kumutethia.

**Translator :** She is proposing that the Government should be able to look into the issues that are affecting the small scale farmers more so the coffee act.

**Esher:** Kitumi numba nene na aka ndiwa na syana ndiwa na syitethasya na kaawa. Na nitweyumbanisi tusuvie miunda indi syoka kutwika mbesa ianangika.

**Translator :** yuwenda kwikwe ata andu ala mesaa mbesa sya andu angi.

**Eashter:** Serikali ndi undu itatona, ivangiti ethiwa mundu ni waiwa kinduni kya andu na niwananga onaethiwa ni muthukumi aile ni kwinuka na ethiwa ni wie mbesa sya aimi ailitwe kwiva ndailite kuthi nasyo.

**Translator :** She is proposing that anyone who mis-appropriates the public resources should be taken to court, should pay what he has stolen.

**Com. Phoebe:** She is has actually referring to people in the coffee industry. Unafikiria mama juu ya hao watu wakubwa wa co-operative wakiiba pesa ya watu.

**Translator :** Wikulywa winena wisilia uvoa wa andu ala methiawa mongamite covalativu. Maya mbesa.

**Easther:** Yi kuya kaawa utesawa.

**Com. Phoebe:** Asante sana. Wacha amalize halafu utakuja. Jina lako?

**Ndunge Mutua:** Ndunge Mutua.

**Com. Ayonga:** Endelea mama.

**Ndunge Mutua:** Mimi nataka, niulize sasa watoto wetu wanasoma na wanamaliza shule natumepeleka watoto wetu college na wanamaliza. Na kuna wale waliomaliza na sasa kunawale wanamaliza juzi juzi na wanapata kazi na wale wazamani hawajaandikwa. Sasa hiyo ni nini? Na mtu akienda kuuliza naambiwa atoe kitu na kitu si kitu kidogo. Ni shilingi elfu ishirini.

**Com. Phoebe:** Kazi gani hiyo?

**Ndunge:** Ya walimu. Sasa hao watoto watatoa pesa wapi, na ndio wanamaliza shule na hawana pesa. Sasa wanatakiwa wauze shamba ile wanalima au wanatakiwa wafanye nini.

**Com. Phoebe:** Wewe unataka namna gani?

**Ndunge:** Serikali iangalie kutoka watoto wale walianza, wanzie kuandika hivi. Na mtu asilipe ile pesa ya hongo. Yangu ndio hiyo na leo ni leo, kwa sababu nimekuona na macho.

**Com. Phoebe:** Asante tumeshukuru sana Mungu akubariki. Tuambie jina mama.

**Malisera Nthikwa:** Naitwa Malisera Nthikwa.

**Com. Phoebe:** Haya Malisera sema tusikie.

**Malisera:** Malisera asya ena syana na niwasomethisi syana na kisio, nanasomethia ila syana na kisio ili nisyoyavitukie syatwika syakundethia, ila ingi syatwikie sya chang'aa na kiwuiawa vau kwakwa na asikali moka makitawa kunengwa mbesa. Mbunge ikunikilye uvoo wa Serikali asikali nimekie ukwatana momakitaa kunewa mbesa na nanena ndiwa "mama wacha". Kimea makue syana matwe kwiwa neke, nundu nimanewa mbesa. Yu syana hii nivia ku naitwikie ila syoo masyie nasyo ilikile ukini. Nenda selikali iwe yeke kuongwa ikwate andu ma chang'aa kivingwe kyeke kuwa.

**Translator :** She is proposing the Government should take the issue of corruption because most of the traditional brews and chang'aa brewers give bribe to policemen. Everytime the administration police or the chiefs come to arrest the brew brewers are given some money and they go.

**Com. Phoebe:** Kwa hivyo unaona tufanye namna gani mama?

**Translator :** Wasya kativa kasyie ata?

**Malisera:** Kativa, kasyie asikali mavakue chang'aa meke kunewa mbesa. Nundu moka kukwata chang'aa mayukwata mekita kunewa mbesa. Mayeka chang'aa na syana ni syanakingie vyiu.

**Translator :** Brewing of chang'aa and traditional brew should be banned.

**Com. Phoebe:** We charge the person who brews and the one who drinks. Na tuna-abolish hii mambo ya chang'aa.

**Malisera:** Ye kyeke uwa kivingwe vyuu. Syana isove na isyoke sukuli ningi ila syi sukuli ni syaekie. Inywe chang'aa na syonthe syanangika kuvika sya etiu.

**Com. Phoebe:** Okay, asante sana. Umefanya mzuri. Wewe unaitwa.

**Catherine Syombua Maingi:** Catherine Syombua Maingi.

**Com. Phoebe:** Ulikua huja ongea?

**Catherine:** Hapana, na mimi jambo nataka kuzugumzia ni juu ya wasichana. Unajua saa zingine sio msichana aolewe na ako nyumbani na ako na ndungu zake. Ndugu zake hawataki kujua kama wametoka tumbo moja. Wanataka wamfuguze. Sasa msichana wa namna hiyo afanye nini.

**Com. Phoebe:** Wewe utwambie ungependekeza naman gani?

**Catherine:** Mimi napendekeza hivi msichana wa aina hiyo, kama ana ndugu zake wajue amezaliwa kama vile wao wamezaliwa na kama kuna uridhi wanaogawiwa wagawiwe pamaoja. Hata msichana ako na watoto tuseme wawili, ama watatu, nao watoto wote amezaa na mtu mmoja na huyu mtu alikua anamdaganya nitakuowa nitakuowa mpaka amefikisha watoto watatu, halafu akishafikisha kiwango hicho anamtoroka. Huyu mtu anaweza kuadhibiwa.

**Com. Phoebe:** Kuna wanawake wametwambia turudishe ile affiliation bill ya zamani ili huyo mwanaume ashtakiwe na awe akilipa pesa za kusomesha hao watoto. Ungependekeza vile wale wengine wa mbele wamependekeza?

**Catherine:** Ndio, mimi nina hayo tu.

**Com. Phoebe:** Conversion between commissioners. Mama sema.

**Francisca Mwikali:** Ninena kikamba.

**Translator :** Witawa ata?

**Francisca Mwikali:** Nitawa Francisca Mwikali.

**Translator :** Anaitwa Francisca Mwikali.

**Francisca:** Ninena yulu wa syindu ila tumaanza na mutumia wakwa.

**Translator :** Anaongea juu ya mali ya familia ama jamii.

**Francisca:** Niweta Serikali niyale kusyovyia kativa maundu amwe ma musyi. Nitumaanza syindu kuya musyi na twamanza syindu isu, kila kindu uisa ithiwa ethiwa wina muimiu ni wata na dwisyi, isu ata ndekwetee musyi. Niweta mbesa sya kaawa. Nianakaawa wakwa, niwakunengia namba na esyoka evulanya mavuku, mbesa ayosa ewe na ndukamanya kila kyuma vo na nuthukuma uu kaawani.

**Translator :** Amefurahi kwamba Serikali imeona umuhimu watu washiriki kurekebisha katiba. Yeye anaona kwamba mashida za ki nyumbani, kama vile mzee ndiye anauwezo wa ku-control zile resources wametafuta na mama kwanyuma. Angeonelea ni vizuri, tusema ni kama kahawa vile wako na shares za kahawa kuna wanaume wana patia mabibi zao shares, lakini ikifika kwa kuchukua zile pesa wao ndio wanachukua wanaenda kuchukua pesa bila kuwaarifu mabibi zao na wanatumia vile wanavyotaka.

**Francisca:** Na wakulya ukwithiwa kwikao na munamanthie imwe.

**Com. Phoebe:** Ungependekeza namna gani mama.

**Francisca:** Nenda Serikali ethiwa ni yonie isovie kativa kindu kitewa ethiwa ni ta mundu kya tewa kiale kutwawa undu kitesikie na kiale utewa mundu auwe evithanitie na we uyisa kwiwa athuka vaa ninauwie. Kila kindu kitewa withiwe ni kisikii. Nutano kutia ng'ombe nza ethiwa ni savali wathi uyuka ukethia ila ng'ombe nitewe na nduona kula mbesa isu syiendie.

**Translator :** Anataka mali yote ya jamii iwe imeandikishwa katika majina ya mzee na bibi yake.

**Com. Phoebe:** Asante sana kuna mwingine? Sema jina?

**Paulina Monthe:** Nitawa Paulina Monthe.

**Translator :** Naitwa Paulina Monthe.

**Paulina:** Nitwithiawa na thina mwingi asyia, wilyi ati, yu nthini wa selikali yitu, ukwithia mwana ula wa nya afitia twiundu umwe na ula wa muthui. Wa nya ethinani nundu huu wa muthui enewa mwanya athi aungame na aungama huu wa nya ayovywa mana. Yu kindu kyu ithie ta ene nthi, nundu ithie nitweiwe nitwanengiwe uhuru, nitwali kuweta mathina maitu onthe tukawetea selikali vatoneka.

**Translator :** She is suggesting that the law should be applied equally on all citizens, because she recognizes there is difference in application of the law between the rich and the poor.

**Paulina:** Undu ula ungi, ngya syithinia kuu na mwingo nitwiwaa ngewa tukewa ndumantha muthui na ngya. Indi ngya syi thinia kuu thina ula munene. Vailie at ngya ni no, nina mundu wa kumitethia na yioyongela kuwaa ti ya kukwa na yi yaiwa ni leu. Na iyaiwa ni ngua. Nasya ati yu kativa muisovia andu ala me mavukuvi kisioni ma savu chivu na ma-councillor aa tusakuite methiawe maisisia thina ula wikisioni kyoo na maisiasya. Kila kyutumwa nasya mwisiasya nandu aiingi kakwonya huu na huu akilitaa vuu na aikilita vuu asyatie mundu atakwa nakwa ndithukumaa, kana kala kothukuma ni kamwe na kena muka. Nenda kativa andu asu me kisioni kyoo.

**Translator :** She is proposing the Government should be able to assist the poor people with their basic needs, and she says the chief and the assistant chief should be able to identify people who are in need in their area of jurisdiction.

**Paulina:** Repetation. Nenda syana ikasoma mana na kila kindu ki mokoni ma selikali, nundu mbinge inaandu syikita kusaitiwa ou.

**Translator :** She is proposing free education for all children.

**Paulina:** Nayu nusyaa etu na ukasyaa aume, na mwitu usu aiaa mume naaitwika we titosyanitwe na andu na aitwika ithe titamai kindu, aikai uthinia vau. Yu indi kativa kayovwa usu ni mwana ta uu wa mundume aa muume na aa kyau ethiwe na kindu taala angin na aume aa maikanene masyaitwe undu umwe.

**Translator :** Girls who end up not getting married should share, equally the family property with their brothers.

**Com. Phoebe:** Asante sana mama.

**Com. Ayonga:** Majina yako?

**Rose Kalondu: Rose** Kalondu. Ninena yulu wa syana

**Com. Phoebe:** Unajua unazungumza kwa hii machine. Hii machine inashika sauti yako.

**Rose :** Ninena yulu wa sukulu syaanani syitu. Thina wivo nikwathiwa nthina ya alimuni, mwalimu aoza ethiwa ni mwakosana na musyai, uthuku usu wonthe akakua sukuli, akathi kutwika kana ikosa isu nutona kwisyilia kanani kakwu. Nenda kativa

kaandikwe ati, mwalimu usu aosewe atua. Yila ukivikia ikosana na kana ka musyii uyu kwisila syanani. Kana kaivikya onakwisa kulea sukulu, withie kaisakwitikila kusoma ingi. Mwalimu usu afutwe.

**Translator :** She is proposing that any teacher that unnecessarily punishes the pupil, should be sacked. Like corporal punishment, because, there some teachers because of family fuse end up transferring their anger on the students.

**Com. Phoebe:** Lakini corporal punishment imefungwa kenya waalimu hawapinge watoto.

**Rose :** Nina thinaungi, mwana avikia kutwana, akatwaa muka wake na akwithiwa kila chang'aa nunywiti. Mwanaa uu atona kwikala vakuvi miaka miongoli atatheo muka.

**Translator :** She is suggesting that marriages should be formalized as early as possible.

**Com. Phoebe:** Tumeambiwa asubuhi kwamba, ile mbuzi tatu ikishatolewa lazima inakua na certificate ya Serikali ya kusema huyo mtu ameo huyo bibi.

**Com. Phoebe:** Wewe ulisema, hauwezi kurudia. Haya mama asante sana.

**Frascisca Nthenya:** Kwa majina naitwa Franscica Nthenya?

**Com. Phoebe:** Usikose kuweka sahihi uko mbele. Did you sign?

**Frascisca:** Yangu ni kuhusu waalimu wale wanakataza watoto kufanya mtihani. Mwalimu akikataza mtoto kufanya mtihani adhibiwe. Hosipitali iwe ya bure na mashule. Yangu ni hayo tu.

**Com. Phoebe:** So free education, free health services. Mwingine? Hakuna mumekwisha wote. Sasa mtu atatuomba. Ulikua unataka kusema na umekaa tu? Sema jina lako.

**Rose mary Nzula:** Rose mary Nzula.

**Com. Phoebe:** Rose mary Nzula, Haya sema Rose mary.

**Rose mary:** Mimi ile kitu nataka Serikali iangalie ni maneno ya wanawake, kwa sababu wanawake ndio wamebamba maendeleo ya nyumbani, na unaweza kuolewa na mtu na ataakiwa na kazi yenye iko na pesa nyingi, anaenda akakunywa pesa zote unabaki na shida. Saa hii, kama wanawake tungeelimishwa wote hata hiyo shida ikikuwa unaendeleza tu mambo yako ya



nyumbani.

**Eunice Mutheo Mbaluka:** Kwa jina naitwa Eunice Mutheo Mbaluka. Nasema juu ya hao watu wanachaguliwa na wananchi kama Councillor na MPs. Nataka Katiba iangalie kama sio hii miaka tano wanasema, kwa sababu wakiambiwa miaka mitano wanaenda wanakaa fuua na hawatutetei sisi wananchi. Kwa sababu wanajua wanakaa pale pale miaka tano. Kwa hivyo akae kwa kiti kwa matendo yake. Na vile anavyoendelea kutetea wananchi.

**Com. Ayonga:** Hayo ndio maoni? asiambiwe ni miaka mitano?

**Eunice:** Iangalie iwe anakaa kwa kiti kwa vile anatetea watu. Ata anaweza kukaa hata kumi tu, lakini akiwa mbaya, miwili hata mmoja.

**Com. Phoebe:** Na wewe unaitwa aje?

**Sera Novi:** Naitwa Sera Novi. Mimi nasema kuhusu hao watu walemavu, sasa nasema kwa nini hao watu walemavu, wengine hawana miguu, kwa nini hawasaidiwi?

**Com. Phoebe:** Wewe utwambie unataka wasaidiwe namna gani?

**Sera:** Nataka wasaidiwe, kama vile wapatiwe pesa za kusaidia na hao hawana miguu wapatiwe miguu za kwenda, wengine wanashida sana, unaona mtu hawezi akasimama, awezi akafanya chochote lakine yeye anataka kufanya kazi. Lakini hata hawezi kwenda kufanya. Wengine ni hao wanakaa kwa street, unaona mtu anakaa kwa street anaomba pesa kila wakati, kwa nini wasipatiwe kitu kidogo hili wasiombe huku nje nje. Wakae mahali ama wapatiwe pesa kidogo waseme, kuna siku moja watapatiwa kitu, wakuje hapa wapatiwe, kama kitu kidogo hivi wasiwe wanakaa nje kuomba kila wakati na wengine hata wanaletwa hapa na watu wao wanawekwa kwa njia wanaambiwa kaa hapa uombe, kwa nini sasa? Kwa hivyo wasaidiwe, tuseme wapewe kitu kidogo huku hili wasiombe.

**Com. Phoebe:** Lakini kitu umesema ya muhimu, unasema wanaletwa, kitu ungesema tufanye investigation tujue, background yao, halafu wapatiwe usaidishi.

**Com. Phoebe:** Tumeshukuru sana, na hatuwezi kuenda bila maombi. Wanawake hawawezi kwenda bila maombi lazima tuombe. Nani atatuombea. Kujeni tuombeni. Tuliombewa na councillor sasa vice atafunga kwa maombi, songa karibu mama utuombea ndio tupate baraka ya Mungu kwa mambo hayo yote tuliyoyasikia leo.

**Prayer:** Bwanatunajiweka mikononi mwako, asante sana kwa yale ambayo umetufanyia tangu asubuhi, uliongoza sisi kutoka

